
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA MAJI

FUNGU 49

**RANDAMA YA MPANGO NA BAJETI
YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA
2014/2015**

DAR ES SALAAM – APRILI 2014

YALIYOMO

1.0	UTANGULIZI	1
1.1	MALENGO NA SERA ZA KITAIFA NA KIMATAIFA	1
1.2	PROGRAMU YA KUENDELEZA SEKTA YA MAJI	2
1.3	MAHITAJI YA FEDHA KATIKA KUTEKELEZA WSDP AWAMU YA KWANZA	3
2.0	DIRA, DHIMA, MAJUKUMU NA MADHUMUNI YA WIZARA.....	3
2.1	DIRA.....	3
2.2	DHIMA.....	3
2.3	MAJUKUMU YA MSINGI YA WIZARA YA MAJI.....	4
2.4	MADHUMUNI	4
2.5	USHIRIKI WA WADAU	5
3.0	TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KWA WIZARA YA MAJI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2012/2013 NA MPANGO WA MWAKA 2013/2014.....	7
4.0	MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2013/2014	14
4.1	UKUSANYAJI WA MADUHULI	14
4.1.1	<i>Makusanyo ya Maduhuli katika Makao Makuu ya Wizara</i>	14
4.1.2	<i>Makusanyo ya Maduhuli ya Bodi za Mabonde ya Maji</i>	14
4.2	UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MPANGO WA MAENDELEO.....	15
4.2.1	<i>Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara ya Maji</i>	15
4.2.2	<i>Miradi ya Maendeleo</i>	16
4.2.2.1	<i>Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa</i>	17
5.0	MALENGO, MAFANIKIO NA CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA WAKATI WA UTEKELEZAJI KATIKA MWAKA 2013/2014.....	21
5.1.	MALENGO.....	21
5.1.1	<i>Idara ya Utawala na Utumishi</i>	21
5.1.2	<i>Kitengo cha Fedha na Uhasibu.....</i>	21
5.1.3	<i>Idara ya Sera na Mipango.....</i>	21
5.1.4	<i>Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano.....</i>	21
5.1.5	<i>Kitengo cha Sheria</i>	22
5.1.6	<i>Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi</i>	22
5.1.7	<i>Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)</i>	22
5.1.8	<i>Kitengo cha Ukaruzi wa Hesabu za Ndani</i>	22
5.1.9	<i>Idara ya Rasilimali za Maji</i>	22
5.1.10	<i>Bohari Kuu ya Maji.....</i>	23
5.1.11	<i>Idara ya Huduma za Ubora wa Maji</i>	23
5.1.12	<i>Idara ya Huduma za Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mijini.</i>	23
5.1.13	<i>Idara ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini</i>	23
5.1.14	<i>Kitengo cha Uratibu wa Programu.....</i>	24
5.2.	UTEKELEZAJI NA MAFANIKIO	24
5.2.1	PROGRAMU YA UTUNZAJI NA UENDELEZAJI WA RASILIMALI ZA MAJI	24
a)	Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji.....	24
b)	<i>Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji na Usimamizi wa Mfumo wa Ikolojia</i>	31
5.2.2	HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI	34
a.)	Ujenzi wa miradi mipyaa	35
b.)	Miradi yenye kuleta matokeo ya haraka.....	37
5.2.3	UBORESHAJI WA HUDUMA ZA MAJI MIJINI	39
5.2.4	KUWAJENGEA UWEZO WATUMISHI NA KUIMARISHA TAASISI	55
5.2.4.1	Uratibu wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji	55

5.2.4.2	Habari, Elimu na Mawasiliano	56
5.2.4.3	Ujenzi na ukarabati wa majengo ya Wizara	57
5.2.4.4	Chuo cha Maendeleao na Usimamizi wa Rasilimali za Maji (<i>WDMI</i>)....	57
5.2.4.5	Maendeleo ya Rasilimali Watu.....	58
5.2.4.6	UKIMWI.....	58
5.2.5	<i>CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KATIKA UTEKELEZAJI NA HATUA ZINAZOCHUKULIWA</i>	58
5.2.5.1	Upatikanaji wa fedha kwa wakati	58
5.2.5.2	Upungufu wa Wataalam katika Sekta ya Maji	59
5.2.5.3	Upatikanaji wa takwimu sahihi na taarifa za utekelezaji kwa wakati.....	59
5.2.5.4	Kuongezeka kwa idadi ya watu kusikoendana na kasi ya uwekezaji	60
5.2.5.5	Hujuma kwenye miundombinu ya maji	60
5.2.5.6	Mabadiliko ya tabianchi.....	60
6.0.	MALENGO KATIKA KIPINDI CHA MUDA WA KATI NA MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015.....	62
6.1	MUHTASARI WA MALENGO MAKUU YA KIPINDI CHA MUDA WA KATI (MTEF)	62
6.2	MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2014/2015.....	63
6.2.1	<i>Makadirio ya Katika Makao Makuu ya Wizara</i>	63
6.2.2	<i>Makadirio ya Maduhuli ya Bodi za Mabonde ya Maji</i>	63
6.3	BAJETI YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA WIZARA YA MAJI 2014/2015	64
6.3.1	<i>Malengo ya Kipindi cha Muda wa Kati, Kazi zitakazotekelawa na Gharama Kifungu kwa Kifungu kwa Mwaka 2014/2015.....</i>	65
6.3.1.1	<i>Kifungu 1001 – Utawala</i>	65
6.3.1.2	<i>Kifungu 1002 – Uhasibu na Fedha</i>	66
6.3.1.3	<i>Kifungu 1003 – Sera na Mipango</i>	67
6.3.1.4	<i>Kifungu 1004 – Habari, Elimu na Mawasiliano</i>	69
6.3.1.5	<i>Kifungu 1005 – Sheria</i>	70
6.3.1.6	<i>Kifungu 1006 – Usimamizi wa Ununuzi.....</i>	70
6.3.1.7	<i>Kifungu 1007 – Mfumo wa Taarifa za Kimenejimenti</i>	71
6.3.1.8	<i>Kifungu 1008 – Ukaguzi wa Ndani</i>	72
6.3.1.9	<i>Kifungu 2001 – Usimamizi Rasilimali za Maji</i>	73
6.3.1.10	<i>Kifungu 2002 – Bohari Kuu ya Maji.....</i>	75
6.3.1.11	<i>Kifungu 2003 – Huduma za Ubora wa Maji</i>	75
6.3.1.12	<i>Kifungu 3001 – Huduma za Majisafi na Usaifi wa Mazingira Mijini.....</i>	77
6.3.1.13	<i>Kifungu 4001 – Huduma za Maji na Usaifi wa Mazingira Vijijini</i>	78
6.3.1.14	<i>Kifungu 4002: Uratibu wa Programu.....</i>	79
6.4	MAKADIRIO YA BAJETI YA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2014/2015.....	80
6.4.1	MGAWANYO WA BAJETI YA MAENDELEO KIPROGRAMU.....	80
6.4.1.1	MCHANGANUO WA BAJETI YA MAENDELEO KIPROGRAMU NA KIMRADI	81
6.4.2.1	<i>KIFUNGU 1001: UTAWALA NA RASILIMALI DATU.....</i>	83
6.4.2.2	<i>KIFUNGU 1003: SERA NA MIPANGO</i>	84
6.4.2.3	<i>KIFUNGU 2001: USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA MAJI</i>	87
6.4.2.4	<i>KIFUNGU 2003: HUDUMA ZA UBORA WA MAJI.....</i>	92
6.4.2.5	<i>KIFUNGU 3001: HUDUMA ZA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MIJINI</i>	94
6.4.2.6	<i>KIFUNGU 4001: HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJJINI</i>	100
7.	VIAMBATISHO.....	102
7.1.	KIAMBATISHO NA. 1: TAARIFA YA KINA JUU YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA VIJJINI 10 KWA MWAKA WA FEDHA 2013/14	102
7.2	KIAMBATISHO NA. 2: MCHANGANUO WA FEDHA ZILIZOPELEKWA KWENYE MIRADI YA MAJI VIJJINI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/14.....	103

7.3	KIAMBATISHO NA. 3: MCHANGANUO WA MAHITAJI YA WATAALAM WA KADA MBALIMBALI KATIKA SEKTA YA MAJI.....	109
7.4	KIAMBATISHO NA. 4: MCHANGANUO WA MAKADIRIO YA FEDHA KWA AJILI YA KUBORESHA HUDUMA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15	110
7.5	KIAMBATISHO NA. 5: MCHANGANUO WA MAKADIRIO YA FEDHA KWA AJILI YA KUBORESHA HUDUMA YA MAJI KUPITIA MIRADI YA MATOKEO YA HARAKA KATIKA MIJI MIDOGO 47 KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15.....	128
7.6	KIAMBATISHO NA. 6: MGAWANYO WA FEDHA ZA NDANI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2013/14 KWA MAJI MIJINI HADI MWEZI MACHI, 2014	129
	KIMBATISHO NA 7: VITUO VYA KUPIMA MTIRIRIKO WA MAJI KWENYE MITO (<i>HYDROMETRIC STATIONS</i>), HALI YA HEWA (<i>METEOROLOGICAL/WEATHER STATIONS</i>) NA MVUA	131

**RANDAMA YA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA YA MAJI ILIYOWASILISHWA
KWENYE KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KWA
MWAKA 2014/2015**

1.0 UTANGULIZI

Maji ni rasilimali muhimu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa nchi yoyote. Upatikanaji wa maji safi, salama na ya kutosha una mchango mkubwa katika kuboresha maisha ya jamii husika na kusaidia katika ukuaji wa uchumi. Kama jitihada mojawapo ya kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 (*Tanzania Development Vision - TDV*) 2025, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, umebainisha maji kama kipaumbele kimojawapo katika kukuza uchumi hasa kwa kuchangia katika uzalishaji wa umeme, kilimo cha umwagiliaji, viwanda na kupunguza umaskini.

Pamoja na Tanzania kuwa na rasilimali za maji za kutosha, mgawanyo wa rasilimali hizo haupo katika uwiano sawa katika maeneo mengi nchini, hivyo kuwa na uhaba mkubwa wa maji katika maeneo kame. Mahitaji ya maji yanazidi kuongezeka siku hadi siku kutokana na ongezeko la watu nchini, ukuaji wa shughuli za uzalishaji mali katika sekta mbalimbali hususan kilimo cha umwagiliaji, uzalishaji wa umeme, uzalishaji viwandani, utalii, uchimbaji madini, ufugaji, uvuvi na wanyama pori. Vilevile, uharibifu wa mazingira, uhaba wa mvua unaotokana na mabadiliko ya tabianchi, na matumizi mabaya ya maji husababisha kupungua au kukauka kwa maji katika vyanzo.

Katika kukabiliana na changamoto katika eneo la rasilimali za maji sambamba na jitihada za usambazaji maji, Wizara inaendelea na jitihada mbalimbali za kuendeleza na kutunza rasilimali za maji, kuongeza upatikanaji wa majisafi na salama na kuhimiza matumizi bora ya maji. Katika kufikia malengo hayo, Wizara ya Maji inatekeleza Sera ya Maji ya Mwaka 2002 ambayo imeweka mfumo madhubuti na endelevu wa kuendeleza na kusimamia rasilimali za maji nchini. Sera inaelekeza ushirikishwaji wa wadau wa sekta ya maji katika hatua mbalimbali za utekelezaji ikiwa ni pamoja na kubuni, kupanga, kujenga, kusimamia, kuendesha na kuifanya matengenezo miundombinu ya maji pamoja na kuchangia gharama za huduma za maji. Sera hiyo inatekelezwa kuititia Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Maji (2006-2015) na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (2006-2025). Aidha, utekelezaji wa Sera hiyo unasimamiwa na Sheria **Na. 11** ya Mwaka 2009 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji pamoja na Sheria **Na. 12** ya Mwaka 2009 ya Utoaji wa Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira.

1.1 Malengo na Sera za Kitaifa na Kimataifa

Utekelezaji wa majukumu katika sekta ya maji unazingatia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 ambayo yamezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA II). Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inalenga kufikisha huduma ya majisafi na

salama kwa wananchi waishio mijini kwa **asilimia 100** na **asilimia 90** kwa wananchi waishio vijiji ni ifikapo mwaka 2025.

Kwa lengo la kuhakikisha tunafikia malengo ya Milenia, Serikali iliandaa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania (MKUKUTA II 2010/2011 – 2014/2015). Katika mkakati huo, Sekta ya Maji imepewa jukumu la kuwapatia wananchi maji safi na salama karibu na makazi yao kwa kuongeza idadi ya wananchi waishio vijiji ni wanaopata huduma hiyo kutoka **asilimia 57.8** ya mwaka 2009 hadi **asilimia 65** ifikapo mwaka 2015 na kuongeza huduma ya maji safi na salama katika miji mikuu ya mikoa 19 kutoka **asilimia 84** ya mwaka 2010 hadi **95** ifikapo mwaka 2015 na kwa Jiji la Dar es Salaam, Kibaha na Bagamoyo huduma kuongezeka kutoka **asilimia 68** ya mwaka 2010 hadi **asilimia 75** ifikapo mwaka 2015.

Katika kuhakikisha malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo katika sekta ya Maji yanafikiwa, Wizara inaendelea na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji iliyoanza rasmi mwaka 2007/2008 na inatekeleza Mpango wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa (*BRN*) ulioanza Julai mwaka 2013, ambapo awamu ya kwanza ya miaka mitatu ya mpango huo inaisha 2016.

1.2 Programu ya Kuendeleza Sekta ya Maji

Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*Water Sector Development Programme – WSDP*) ya mwaka 2006 hadi 2025 inatekelezwa kuitia Programu ndogo **4** kama ifuatavyo:-

- (i) Programu ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji inatekelezwa na Wizara ya Maji katika mabonde 9 ya maji nchini. Utekelezaji unalenga kuweka utawala bora wa kusimamia na kutunza rasilimali za maji katika mabonde ya maji ikiwa ni pamoja na kuhakikisha rasilimali hiyo inalindwa dhidi ya uchafuzi na inatumika kwa njia endelevu kwa manufaa ya kiuchumi na kijamii kwa ajili ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo;
- (ii) Programu ya maji na usafi wa mazingira vijiji ni inatekelezwa katika Halmashauri zote nchini chini ya usimamizi na uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI. Utekelezaji unalenga kuboresha utoaji huduma ya majisafi na salama kwa wananchi waishio vijiji ni kwa kusogea huduma hizo karibu na makazi yao na pia kuboresha usafi wa mazingira katika maeneo yao;
- (iii) Programu ya majisafi na usafi wa mazingira mijini inatekelezwa na Wizara ya Maji katika mamlaka za maji za miji mikuu ya mikoa, miji mikuu ya wilaya, miji midogo na katika miradi ya maji ya kitaifa ya Chalinze, Maswa, Mgango-Kiabakari, Wanging’ombe, Makonde, Masasi – Nachingwea, Handeni Trunk Main na Mradi wa maji wa Kahama-Shinyanga; na
- (iv) Programu ya kuzijengea uwezo na kuimarisha Taasisi zinazosimamia na kuratibu Programu ya Maji.

Programu hiyo inatekelezwa kwa awamu ya miaka mitano mitano ambapo Awamu ya Kwanza ilianza kutekelezwa mwaka wa fedha 2007/2008 na ilipangwa kukamilika mwaka 2011/2012. Baada ya kubainika kuwa kuna umuhimu wa kuongeza muda ili kukamilisha kazi ambazo zimeanza lakini zisingeweza kukamilika katika kipindi muafaka, wadau wa sekta walikubaliana kuongeza muda wa utekelezaji wa Awamu ya Kwanza na kwa sasa itakamilika mwezi Juni mwaka 2014. Maandalizi ya Awamu ya Pili ya Programu hiyo (*WSDP Phase II*) yako katika hatua za mwisho za ukamilishaji na utekelezaji wake unatarajiwa kuanza mwezi Julai mwaka 2014.

1.3 Mahitaji ya fedha katika kutekeleza WSDP Awamu ya Kwanza

Katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa *WSDP*, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa maendeleo waliahidi kuchangia kiasi cha **Dola za Marekani milioni 1,691.8**. Kati ya fedha hizo, Serikali iliahidi kuchangia **Dola za Marekani milioni 540.2** na Washirika wa Maendeleo waliahidi kuchangia kiasi cha **Dola za Marekani milioni 1,151.6**. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 kiasi cha **Dola za Marekani milioni 1,156.8** zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji nchini, ambapo kiasi cha **Dola za Marekani milioni 255.7** kimetolewa na Serikali na kiasi cha **Dola za Marekani milioni 901.1** kimetolewa na Washirika wa Maendeleo. Kiasi cha **Dola za Marekani milioni 250.5** ambazo hazijatolewa mpaka sasa kwa upande wa Washirika wa Maendeleo ni ahadi za wale wanaopeleka fedha zao moja kwa moja kwenye miradi (*earmarked projects*). Washirika wa Maendeleo wanaochangia kupitia mfuko wa pamoja (*basket*) wamekamilisha ahadi zao za awali kiasi cha **Dola za Marekani milioni 435.3**. Aidha, baadhi ya miradi iliyopangwa kutekelezwa kupitia fedha za Washirika wa Maendeleo wanaofadhili kupitia mfuko wa pamoja (*basket*) haijakamilika na kupelekea kuwepo mahitaji ya ziada yasiyoepukika kulingana na mikataba kiasi cha **Dola za Marekani Milioni 162.98** kwa ajili ya kukamilisha miradi hiyo kufikia mwezi Juni, 2014 kabla ya kuanza utekelezaji wa awamu ya pili ya *WSDP*. Hadi sasa ahadi iliyopo kutoka kwa wafadhili wa *Basket* katika kugharamia mahitaji hayo ya ziada ni **Dola za Marekani Milioni 73.3**, hivyo kuwa na upungufu wa **Dola za Marekani Milioni 89.68**.

2.0 DIRA, DHIMA, MAJUKUMU NA MADHUMUNI YA WIZARA

2.1 Dira

Dira ya Wizara ya Maji ni kuwa na mfumo endelevu wa kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

2.2 Dhima

Dhima ya Wizara ya Maji ni kuhakikisha rasilimali za maji zinasimamiwa, zinaendelezwa na zinatumika kwa njia endelevu na shirkishi ili kukidhi mahitaji ya sekta mbalimbali kwa kuweka

mfumo madhubuti wa kitaasisi wa kusimamia rasilimali za maji, kuboresha miundombinu ya usambazaji majisafi na usafi wa mazingira vijijini na mijini.

2.3 Majukumu ya Msingi ya Wizara ya Maji

Majukumu ya msingi ya Wizara ya Maji ni yafuatayo:-

- (i) Kutayarisha na kusimamia utekelezaji wa Sera, Mikakati na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji;
- (ii) Kutayarisha na kusimamia sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia Sekta ya Maji;
- (iii) Kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji;
- (iv) Kukusanya, kuchambua, kutafsiri na kuhifadhi takwimu muhimu za Sekta ya Maji;
- (v) Kutoa miongozo ya kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za maji;
- (vi) Kutoa miongozo ya utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira mijini na vijijini;
- (vii) Kutoa mafunzo kwa wataalam wa Sekta ya Maji katika ngazi na kada mbalimbali za utekelezaji;
- (viii) Kuendeleza tafiti kuhusu teknolojia zinazotumika katika kutoa huduma ya maji; na
- (ix) Kuratibu majukumu na kutekeleza ushauri wa Bodi ya Taifa ya Maji.

2.4 Madhumuni

Madhumuni ya Wizara ya Maji katika kipindi cha Mpango cha 2012/2013-2014/2015 ni yafuatayo:-

- (i) Kuhakikisha rasilimali za maji zinasimamiwa na zinatumika kwa njia endelevu na shirikishi na utunzaji wa mazingira kwa manufaa ya kijamii na kiuchumi;
- (ii) Kuhakikisha makundi ya jamii vijijini, mijini na pembezoni mwa miji yanapata huduma ya majisafi na usafi wa mazingira;
- (iii) Kuboresha mazingira ya kazi na kuendeleza watumishi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi;
- (iv) Kusimamia kazi, uwajibikaji na kudhibiti mianya ya rushwa; na
- (v) Kuimarisha utoaji wa huduma na elimu kwa watumishi wa Wizara na Taasisi zake kwa lengo la kupunguza maambukizi ya UKIMWI.

Katika kutimiza madhumuni ya Wizara, mgawanyo wa fedha za bajeti kwa mwaka 2014/2015 umezingatia maeneo muhimu yaliyopewa kipaumbele katika Mpango wa Muda wa Kati (*Medium Term Expenditure Framework - MTEF*). Maeneo hayo ni pamoja na yale yaliyoainishwa katika Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambayo ni:-

- (i) Kukamilisha na kutekeleza mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika mabonde yote tisa;
- (ii) Kukarabati na kujenga miundombinu ya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi;
- (iii) Kuimarisha uwezo wa Ofisi za Mabonde yote tisa pamoja na maabara za maji ili ziweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu;
- (iv) Kujenga mabwawa ya kimkakati kwa ajili ya kuongeza uwezo wa kuhifadhi maji na kukarabati mabwawa yaliyopo kwa ajili ya matumizi mbalimbali hususan katika maeneo kame;
- (v) Kukarabati na kujenga miradi ya maji na usafi wa mazingira vijiji kupitia mpango wa “Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa” (BRN)
- (vi) Kuboresha huduma ya maji katika miji mikuu ya mikoa, miji ya wilaya na miji midogo kwa kukarabati na kujenga miundombinu ya majisafi na majitaka;
- (vii) Kuimarisha huduma ya maji na usimamizi wa miradi ya kitaifa (Wanging’ombe, Maswa, Mugango-Kiabakari, Handeni Trunk Main-HTM, Masasi – Nachingwea, Chalinze, Makonde na Kahama-Shinyanga);
- (viii) Kutekeleza mpango maalum wa kuboresha utoaji wa huduma za majisafi na uondoaji wa majitaka Jijini Dar es Salaam; na
- (ix) Kuimarisha uwezo wa taasisi katika ngazi ya Wizara, Mikoa, Halmashauri, Mamlaka za Maji Mijini, Ofisi za Mabonde na sekta binafsi katika utoaji na usimamizi wa huduma za maji.

2.5 Ushiriki wa Wadau

Sera ya Sekta ya Maji inahimiza ushiriki wa wadau mbalimbali katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji. Ushiriki huo wa wadau unalenga kuainisha majukumu na uwajibikaji wao. Wadau wakuu katika Sekta ya Maji ni wafuatao:-

- (i) Wizara na Taasisi za Serikali ikiwa ni pamoja na wizara zinazosimamia sekta za viwanda, maliasili, kilimo, nishati na madini, afya na elimu, mazingira na TAMISEMI;
- (ii) Serikali za Mitaa;
- (iii) Taasisi za utafiti na mafunzo;
- (iv) Sekta binafsi;
- (v) Jumuiya za Maendeleo za Kimataifa ambazo nchi yetu ni mwanachama kama vile *SADC* na *EAC*;
- (vi) Nchi wahisani na mashirika ya misaada ya maendeleo;
- (vii) Mashirika na taasisi zisizo za kiserikali; na
- (viii) Makundi mbalimbali ya kijamii.

3.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KWA WIZARA YA MAJI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2012/2013 NA MPANGO WA MWAKA 2013/2014

1. Nyongeza ya Fedha

Agizo/Ushauri

*Kamati inaomba Serikali kuiongezea fedha Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake ya msingi na kupunguza tatizo la maji hasa maeneo ya Vijijini ambako tatizo ni kubwa zaidi. Kamati inashauri Serikali kuiongezea Wizara kiasi cha **shilingi bilioni 184.5** za ziada.*

Utekelezaji

Wizara inaishukuru Kamati kwa jitihada zilizofanyika kuiwezesha Wizara kupata nyongeza ya fedha za ndani za miradi ya maendeleo kiasi cha **shilingi bilioni 184.5**. Hatua hiyo imefanya bajeti ya fedha za ndani za miradi ya maendeleo kwa Wizara ya Maji kuongezeka kutoka **Shilingi bilioni 140.1** mwaka 2012/2013 hadi **Shilingi bilioni 312.1** mwaka 2013/2014, sawa na ongezeko la **asilimia 123**. Kati ya fedha hizo zilizoongezwa, kiasi cha **Shilingi bilioni 160.9** sawa na asilimia **87.2** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji vijijini.

2. Kodi za Madawa ya Maji

Agizo/Ushauri

Kamati inaipongeza Serikali kwa kupunguza Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye madawa ya kutibia maji kutoka 18% hadi 9.9%. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuiondoa kabisa kodi hii na kuwa 0% (zero rated) ili gharama za maji zipungue.

Utekelezaji

Katika kushughulikia suala hili, Wizara imepeleka maombi Wizara ya Fedha kusisitiza kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwenye ununuzi wa dawa hizo ifutwe kabisa (*zero rated*). Suala hili linafanyiwa kazi Wizara ya Fedha chini ya Kikosi Kazi cha Taifa (*National Revenue Task Force*) kinachoandaa mapendekezo ya kodi kwa mwaka wa fedha 2014/15.

3. Mgawanyo wa Bajeti

Agizo/Ushauri

Kamati imebaini kuwa kuna tofauti kubwa sana kati ya bajeti inayotengwa kwa ajili ya maji Mijini na Vijijini. Matokeo yake ni kwamba, watu wanaopata maji safi na salama mijini ni

asilimia 86 na vijijini ni asilimia 58.6 tu ikizingatiwa kwamba asilimia 80 ya Watanzania wanaishi Vijijini. Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti ya maji Vijijini ili kupunguza tatizo kubwa la maji linalokabili maeneo mengi.

Utekelezaji

Wizara imezingatia ushauri wa Kamati wa kuongeza fedha za ndani za miradi ya maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji vijijini. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, **asilimia 53** zimetengwa kwa ajili ya huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini, **asilimia 34** ni kwa ajili ya huduma ya maji na usafi wa mazingira mjini, **asilimia 9** ni kwa ajili ya utunzaji wa vyanzo vya maji na **asilimia 4** ni kwa ajili ya kujenga uwezo na kuimarisha taasisi zinazotekeliza WSDP.

4. Utunzaji na Uendelezaji wa Vyanzo vya Maji

Agizo/Ushauri

Kwa kuwa mahitaji ya maji yanaongezeka siku hadi siku kutokana na ongezeko la watu, mifugo pamoja na shughuli za kiuchumi na kijamii, vyanzo vingi vya maji nchini vimeanza kukauka. Kamati inaishauri Serikali pamoja na wananchi kutunza vyanzo vyake vya maji.

Utekelezaji

Katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya **vyanzo 174** vilitambuliwa kuwa katika hatari ya kuharibiwa na kuathiriwa kutokana na shughuli za kibinadamu zinazofanyika kwenye maeneo ya vyanzo hivyo. **Vyanzo 59** kati ya hivyo vimebainishwa kwa ajili ya taratibu za kuvitangaza kuwa maeneo tengefu ya vyanzo vya maji. Mapendekezo ya **vyanzo saba (7)** katika Bonde la Ziwa Rukwa tayari yamewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuvitangaza rasmi kuwa maeneo tengefu. Maeneo hayo ni maeneo ya vyanzo vya maji chini ya ardhi yaliyoko Chokaa, Kidole, Kiswaga, Matundasi A, Matundasi B, Mkola na Bwawa la Milala.

Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wananchi na kuweka mipaka maeneo ya vyanzo vya maji ili kuvikinga dhidi ya uharibifu wa mazingira pamoja na kutangaza vyanzo vya maji vilivyobainishwa kuwa maeneo tengefu. Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maji imeandaa Mpango Maalum wa miaka mitano wa kuhifadhi na kutunza vyanzo vya maji utakaoanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2014/2015.

5. Uvunaji wa Maji ya Mvua Agizo/Ushauri

Kwa kuwa uhaba wa maji ni tatizo kubwa kwa nchi yetu, Kamati inaishauri Serikali iendelee kuhimiza na kuhamasisha jamii kwa kutoa elimu ya utaratibu wa uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mabwawa, malambo na uvunaji wa maji ya paa. Aidha, Serikali ihimize Halmashauri kutunga sheria ndogo ili kuwepo na utaratibu wa uvunaji wa maji ya mvua.

Utekelezaji

Katika kipindi cha utekelezaji wa WSDP I mwaka 2007-2014, Serikali imehamasisha uvunaji wa maji ambapo hadi kufikia Machi 2014, jumla ya matanki **675** ya uvunaji wa maji ya mvua yamejengwa. Matanki haya yamejengwa kwenye maeneo mbalimbali zikiwemo Taasisi kama shule na hospitali. Katika kuendeleza juhudhi hizo, mafunzo yataholewa kwa mafundi **wawili** kwa kila kijiji ili kuendeleza ujenzi huo na kuwapa fursa wananchi kuona, kuiga na kutumia teknolojia hiyo. Vilevile, Wataalam Washauri wanaosimamia utekelezaji wa mradi wa **vijiji 10** wamepewa jukumu la kuhamasisha wananchi kuhusu uvunaji wa maji ya mvua. Aidha, Serikali inaendelea kuhamasisha na kushauri kila Halmashauri kutunga sheria ndogo ndogo ambazo zitahakikisha kuwa nyumba zote zinazojengwa zinawekewa miundombinu kwa ajili ya uvunaji wa maji ya mvua. Tayari Halmashauri za Manispaa za Iringa na Wilaya ya Iringa zimetunga sheria hizo.

6. Mradi wa Maji katika Vijiji 10 kwa kila Halmashauri

Mradi huu ulipoanzishwa ulionekana wenye tija na kwamba ungepunguza tatizo la maji Vijijini kwa kiwango kikubwa. Aidha, visima vinavyochimbwa ni vichache na baadhi havitoi maji na vingine hutoa maji kwa muda mfupi. Kamati inasisitiza Serikali kufanya yafuatayo:-

a) Agizo/Ushauri

Serikali ione umuhimu wa kuongeza fedha za ndani ili kuharakisha utekelezaji wa mradi huu.

Utekelezaji

Serikali imeendelea kuongeza fedha za ndani za miradi ya maendeleo katika bajeti ya sekta ya Maji kwa kadri hali ya fedha inavyoruhusu kila mwaka. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya **shilingi bilioni 312.1** zilitengwa kwenye bajeti ya Wizara ya Maji, sawa na ongezeko la **asilimia 123** ikilinganishwa **shilingi bilioni 140.1** zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2012/2013. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2013/2014, mradi wa vijiji 10 kwa kila Halmashauri umetengewa jumla ya **shilingi bilioni 75.34**

Hata hivyo, utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2013/14 umekumbana na changamoto ya upatikanaji wa fedha. Kwa upande wa fedha za ndani, hadi sasa kiasi kilichotolewa ni **shilingi bilioni 86.0** (sawa na **asilimia 27.6**) ambapo kati ya hizo, **shilingi bilioni 48.8** zimepelekwa Maji Vijijini na miradi wa Vijiji 10 umepelekewa **shilingi bilioni 34.3**.

b) Agizo/Ushauri

Serikali iangalie namna ya kupunguza gharama kwa kuipa kampuni moja kufanya kazi ya upimaji na uchimbaji. Utaratibu huu utarahisisha uwajibikaji iwapo maji hayatapatikana na hata gharama zitapungua.

Utekelezaji

Wizara inakubaliana na ushauri wa Kamati. Matayarisho ya awamu ya pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji yanaendelea ambapo mapendekezo ya muundo wa awamu hiyo yatakamilika mwezi Juni, 2014. Katika awamu hiyo, Serikali itaweka kipaumbele katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi kwa kuhakikisha mkandarasi anayepatikana anafanya kazi za upimaji na uchimbaji ili kama maji hayatapatikana awajibike yeze kutafuta mahali pengine.

c) Agizo/Ushauri

Serikali ipitie upya Sheria ya Ununuzi (PPA, 2004) ili kupunguza gharama za miradi na urasimu.

Utekelezaji.

Kutokana na kuonekana kwa mapungufu katika baadhi ya vipengele vya Sheria ya Ununuzi (PPA 2004) na kanuni zake (PPR 2005), Serikali imefanya mabadiliko ambayo yametoa sheria mpya (PPA 2011) na kanauni zake (PPR 2013). Mabadiliko yaliyofanywa yamelenga kupunguza gharama za miradi pamoja na urasimu.

Baadhi ya mabadiliko yaliyofanyika ni kupunguza muda wa kutangaza zabuni kutoka siku **45** hadi siku **30** kwa zabuni kubwa (*International Competitive Bidding*) na kutoka siku **30** hadi siku **21** kwa zabuni za ndani (*National Competitive Bidding*).

Vilevile, Sheria na kanuni mpya zimeongeza viwango vya gharama kwa njia mbalimbali za Ununuzi. Kwa mfano, – Ununuzi wa kazi (*Works,*) Viwango vya kutangaza kwa “*National Competitive Bidding*” vimeongezeka kutoka kiwango cha mwisho cha **shilingi bilioni 3** hadi **5**. Pia Sheria imetoa mwongozo kuwa mwenye gharama ndogo sana aweze kunyimwa *Tender* iwapo inaonekana kuwa hataweza kutekeleza kazi inavyostahili.

Katika utekelezaji wa miradi ya maji, taratibu za ununuzi wa wakandarasi na watalaam washauri zimepungua kutoka siku **315** hadi siku **90** baada ya kuondolewa utaratibu wa Halmashauri kufuatilia *No objection* Wizarani.

Utangazaji wa *Tender*.

Awali ilikuwa lazima kutangaza katika magazeti lakini katika Sheria ya 2011 na Kanuni za 2013, utangazaji unafanyika katika *Formal Tender Portal* na tovuti/ubao wa matangazo wa taasisi husika.

Sheria ya 2011 na Kanuni zake za 2013 imeruhusu kugawa *package* ndogo ndogo kwa ajili ya kujenga uwezo wa wafanyabiashara wazawa. Kabla ya hapo kugawa zabuni kubwa katika vipande vidogo vidogo ilikuwa hairuhusiwi. Hii itasaidia ukamilishaji wa taratibu za ununuzi mapema zaidi, pia hata kazi kutekelezwa na wazabuni wengi kuliko awali. Hatua hii itapunguza “risk” ya kutoa kazi yote kwa mzabuni mmoja.

Matumizi ya Kanuni za *MTB* kwa kutumia *Circular Resolution* yameruhusiwa kwa manunuzi yote. Awali Ununuzi wa *Consultancy Services* haukuwa na hiyo nafasi.

Attorney General amepewa muda maalumu wa kupitia mikataba (Siku **21**). Kabla ya hapo hakuwa amepangiwa muda wowote hivyo angeweza kukaa na mikataba kwa muda anaotaka na hivyo kuchelewesha kazi.

Evaluation Report inapaswa kukamilika ndani ya siku **14** na kupelekwa *Tender Board*. Awali hapakuwa na muda maalumu uliowekwa kisheria. Hivyo mabadiliko mengi yamefanyika kuzingatia uwazi, ushindani na urahisi wa kufanya ununuzi bila kutumia gharama kubwa na kupunguza urasimu katika mchakato wa ununuzi.

d) Agizo/Ushauri

Kwa kadri inavyowezekana, Serikali inashauriwa kutumia Wataalam Waelekezi wetu badala ya kutumia wataalam toka nje kwa nia ya kupunguza gharama.

Utekelezaji

Wizara imezingatia ushauri wa Kamati ambapo katika mfumo wa *BRN*, utekelezaji wa miradi umegawanywa kwenye makundi kama ifuatavyo:-

Kundi la 1: Miradi yenye gharama isiyozidi **shilingi milioni 200** itasanifiwa na Wahandisi wa Halmashauri na kujengwa na Mafundi wa Halmashauri;

Kundi la 2: Miradi yenyne gharama inayozidi **shilingi milioni 200** na chini ya **shilingi bilioni moja** itasanifiwa na Wahandisi wa Halmashauri na kujengwa kwa kutumia wakandarasi wadogo wadogo wakisimamiwa na Wahandisi wa Halmashauri.

Kundi la 3: Miradi yenyne gharama inayozidi **shilingi bilioni moja** itasanifiwa na Wahandisi Washauri wa ndani na nje watakaoajiriwa na Halmashauri na kujengwa kwa kutumia wakandarasi wakubwa wa ndani na nje wakisimamiwa na Wataalam washauri.

Mfumo huo wa utekelezaji umezingatia matumizi ya wataalam wa ndani ya nchi kwenye kundi 1 na 2.

e) Agizo/Ushauri

Maeneo yenyne madini kama chumvi na fluoride, yaangaliwe namna ya kupata maji kwa njia nyingine kama mabwawa ili kupunguza athari zinazoweza kutokea kutokana na matumizi ya maji hayo.

Utekelezaji

Ushauri wa Kamati umezingatiwa. Aidha, Wizara inaendelea na zoezi la kubaini vyanzo vyenye kiwango cha juu cha madini ya *fluoride* na chumvi chumvi na takwimu hizo zitatumika kuandaa ramani inayoonyesha maeneo yanayofaa kuendelezwa kwa miradi mipya ya maji. Katika kipindi cha 2014/2015, Wizara imetenga fedha kwa ajili ya shughuli za utafiti ambaa utasaidia kuanisha vyanzo mbadala kwenye maeneo ambayo maji hayana ubora unaokubalika.

f) Agizo/Ushauri

Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi kuhusu ubora na utunzaji wa pampu za maji ili kuepuka uharibifu unaotokana na matumizi yasiyo sahihi.

Utekelezaji

Wizara imepokea ushauri na inaendelea kutoa mafunzo ya uendeshaji na utunzaji wa pampu kwa wananchi kwenye maeneo ya miradi na kusimamia uagizaji wa pampu zilizo na ubora utakaowezesha matumizi sahihi kwa wananchi ili kupunguza uharibifu wa mara kwa mara. Hadi mwezi Machi 2014, mafunzo yametolewa kwa mafundi **wawili** kwa kila mradi kwa miradi **228** iliyokamilika.

7. Uharibifu wa Miundombinu ya Maji

Agizo/Ushauri

Kamati imebaini kuwa maeneo mengi ambayo miundombinu yake imeharibiwa ni kwa sababu pamoja na mambo mengine ya biashara ya chuma chakavu ambapo wahalifu wanabomoa miundombinu ya maji. Kamati inashauri Serikali kuangalia uwezekano wa kujenga miundombinu isiyotumia chuma.

Utekelezaji

Suala hili litaendelea kuzingatiwa katika ujenzi wa miradi. Kwa maeneo ambayo yameathirika yanarekebishwa kwa kuzingatia ushauri wa Kamati.

Wizara ya Maji imeendelea kuelekeza matumizi ya bomba na vifaa vya *plastic* aina ya *High Density Polyethylene (HDPE)*, *Polyethylene 100 (PE 100)* kwenye ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji ili kudhibiti uvujaji na uharibifu wa miundombinu ya maji inayosababishwa na biashara ya chuma chakavu. Aidha, Mamlaka za Maji zimeelekezwa kuendelea kuwashirikisha na kuwaelimisha wananchi kuhusu hasara itokanayo na uharibifu na kutakiwa kubaini wahalifu wa miundombinu ya maji ili hatua za kisheria zichukuliwe.

8. Miundombinu Chakavu

Agizo/Ushauri

Kamati imebaini kuwa maji mengi hupotelea njiani kabla ya kumfikia mtumiaji kwa sababu ya miundombinu chakavu. Kamati inaishauri Serikali kufanya ukarabati wa miundombinu hiyo na kudhibiti wizi wa maji.

Utekelezaji

Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuweza kudhibiti na kupunguza maji yasiyolipiwa ikiwepo upotevu na wizi wa maji. Hatua hizo ni pamoja na ukarabati wa miundombinu ya maji ili kuondoa uvujaji, ufungaji wa mita (dira za maji) kwa wateja wote na ukamataji wa watu waliojiunganishia huduma ya maji bila kufuata sheria. Mamlaka za maji nchi nzima zimeelekezwa na zinafuatiliwa kuzingatia matumizi ya mita kwa wateja wote. Vile vile, Mamlaka zote zimeelekezwa kuunda timu za kufuatilia upotevu wa maji ili kutoa taarifa zinazosaidia kuchukua hatua za haraka. Kutokana na hatua hizo, uvujaji na upotevu wa maji kwa Mamlaka za Maji umeendelea kupungua kutoka asilimia **51** Julai, 2011 hadi kufikia asilimia **36.3** Juni 2013; na unatarajiwa kupungua hadi asilimia **25** ifikapo Juni, 2016.

4.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2013/2014

4.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

4.1.1 Makusanyo ya Maduhuli katika Makao Makuu ya Wizara

Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 jumla ya **shilingi 160,231,456** zilikadiriwa kukusanya kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato vya Wizara. Hadi kufikia Machi 2014 makusanyo ya maduhuli yalifikia **shilingi 95,258,066** sawa na **59%** ya makadirio. Mchanganuo wa makusanyo ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 4.1**.

Jedwali Na. 4.1: Makusanyo ya Maduhuli katika Makao Makuu ya Wizara

Kifungu	Jina la Idara	2012/2013			2013/2014		
		Makadirio	Makusanyo	% ya Makusanyo	Makadirio	Makusanyo	% ya Makusanyo
1001	Utawala na Rasilimali Watu	36,233,000	46,282,246.45	128	40,231,456	13,354,466	33
2003	Huduma za Ubora wa Maji	86,460,000	79,266,205.00	92	120,000,000	81,903,600	68
Jumla		122,693,000	125,548,451.45	102	160,231,456	95,258,066	59

4.1.2 Makusanyo ya Maduhuli ya Bodi za Mabonde ya Maji

Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji **Na. 11** ya mwaka 2009, Bodi za Maji za Mabonde zinaruhusiwa kukusanya na kutumia mapato yatokanayo na ada za kutumia maji, utafiti na upimaji wa maji. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, jumla ya **shilingi 1,768,887,117** zilikadiriwa kukusanya. Hadi kufikia Machi 2014, makusanyo ya maduhuli yalifikia jumla ya **shilingi 1,527,245,592.9** sawa na **asilimia 86** ya makadirio. Mchanganuo wa makusanyo ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 4.2**.

Jedwali 4.2: Makusanyo ya Maduhuli ya Bodi za Maji za Mabonde

Na	Bonde	2012/2013			2013/2014		
		Makadirio	Makusanyo Hadi 14 Juni, 2013	% ya Makusanyo	Makadirio	Makusanyo Hadi 31 Machi, 2014	% ya Makusanyo
1.	Pangani	146,000,000	150,000,000	103	178,500,000	282,580,175	158
2.	Wami/Ruvu	560,000,000	159,517,254	28	412,172,117	130,463,955	32
3.	Mto Rufiji	130,000,000	220,000,000	169	325,000,000	429,123,701	132
4.	Ruvuma na	105,000,000	75,324,352	72	178,395,000	54,906,164	31

Na	Bonde	2012/2013			2013/2014		
		Makadirio	Makusanyo Hadi 14 Juni, 2013	% ya Makusanyo	Makadirio	Makusanyo Hadi 31 Machi, 2014	% ya Makusanyo
	Pwani ya Kusini						
5.	Ziwa Nyasa	61,000,000	52,541,090	86	104,320,000	65,900,000	63
6.	Bonde la Kati	90,000,000	87,596,219	97	151,000,000	146,572,046.90	97
7.	Ziwa Rukwa	53,000,000	44,382,614	84	82,500,000	161,203,263	195
8.	Ziwa Tanganyika	40,000,000	47,376,520	118	140,000,000	25,770,000	18
9.	Ziwa Victoria	115,000,000	94,580,996	82	197,000,000	230,726,288	117
Jumla		1,300,000,000	931,319,045	72	1,768,887,117	1,527,245,592.9¹	86

4.2 Utekelezaji wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Mpango wa Maendeleo

4.2.1 Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara ya Maji

Katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya **shilingi 29,652,654,000** zilikasimiwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **shilingi 16,332,777,000** sawa na **asilimia 55.1** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC), na **shilingi 13,319,877,000** sawa na **asilimia 44.9** zilitengwa kwa ajili ya mishahara ya watumishi (PE). Hadi kufikia mwezi Machi, 2014, jumla ya shilingi **14,888,240,948** zimetolewa. Kati ya fedha zilizotolewa, **shilingi 4,817,732,878** ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC) na **shilingi 10,070,508,069** ni fedha za Mishahara (PE) (Jedwali 4.3)

Jedwali Na. 4.3: Muhtasari wa Matumizi ya Kawaida kwa kila Kifungu na kiasi kilichotolewa hadi mwezi Machi, 2014

KIFUNGU	IDARA/KITENGO	Bajeti ya Mwaka 2013/2014 iliyoidhinishwa			Jumla ya Fedha zilizotolewa hadi 31 Machi 2014			% OC	% PE
		OC	PE	Jumla	OC	PE	Jumla		
1001	Utawala	1,948,705,000	1,712,591,000	3,661,296,000	736,212,529	1,250,307,240	1,986,519,769	38	73
1002	Uhasibu	599,199,000	883,930,000	1,483,129,000	213,372,663	562,268,921	775,641,585	36	64
1003	Sera na Mipango	2,125,917,000	326,282,000	2,452,199,000	1,585,758,771	273,903,240	1,859,662,011	75	84
1004	Habari na Mawasiliano	310,686,000	49,324,944	360,010,944	78,280,597	43,460,865	121,741,462	25	88
1005	Sheria	323,560,000	100,473,008	424,033,008	67,619,866	61,823,741	129,443,607	21	62

- ¹ NB: 1. Mrahaba kutoka TANESCO umechangia kuongeza asilimia za makusanyo kwa mabonde ya Rufiji na Pangani
 2. Viwango vipyta vya tozo la matumizi ya maji vilivyoanza kutumika mwaka wa fedha wa 2013/2014 vimechangia kupanda kwa asilimia za makusanyo.
 3. Changamoto kwa baadhi ya maeneo ambayo hati za madai zenyetivango vya awali ziliikuwa zimewasilishwa kwa wateja hivyo kulazimika kulipa kwa viwango vya awali imechangia kutoongeza kwa haraka asilimia za makusanyo.
 4. Changamoto nyingineni ni kuwa wateja wengi hulipa mwishoni mwa mwaka wa fedha hivyo asilimia za makusanyo zinatarajiwa kuongezeka zaidi ifikapo Juni 2014

KIFUNGU	IDARA/KITENGO	Bajeti ya Mwaka 2013/2014 iliyoidhinishwa			Jumla ya Fedha zilizotolewa hadi 31 Machi 2014			%-OC	%-PF
1006	Usimamizi wa Manunuzi	567,019,000	548,059,856	1,115,078,856	109,696,874	262,768,928	372,465,802	19	48
1007	Mfumo wa Habari	320,285,000	89,477,043	409,762,043	78,633,391	74,265,020	152,898,411	25	83
1008	Ukaguzi wa Ndani	495,243,000	103,067,812	598,310,812	99,236,038	72,794,585	172,030,624	20	71
2001	Rasilimali za Maji	952,889,000	4,954,215,957	5,907,104,957	282,390,257	3,865,973,341	4,038,363,598	30	78
2002	Bohari	223,012,000	126,379,000	349,391,000	47,807,361	73,972,456	121,779,817	21	59
2003	Huduma za Ubora wa Maji	363,458,000	1,677,971,048	2,041,429,048	120,558,385	1,013,317,128	1,033,875,512	33	60
3001	Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini	4,840,408,000	1,210,159,000	6,050,567,000	898,039,282	1,110,159,000	2,108,198,282	19	92
4001	Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji	2,047,305,000	665,262,332	2,712,567,332	419,810,595	605,262,331	1,085,072,926	21	91
4002	Uratibu wa Programu	396,758,000	0	396,758,000	80,316,269		80,316,269	20	0
5001	Taasisi ya Usimamizi na Maendeleo ya Maji	0	213,255,000	213,255,000	0	190,802,273	190,802,273	0	89
6001	Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa	0	659,429,000	659,429,000	0	609,429,000	659,429,000	0	92
GRAND TOTAL		15,514,444,000	13,319,877,000	28,834,321,000	4,817,732,879	10,070,508,069	14,888,240,948	31	76
	PE-WDMI	818,333,000	0	818,333,000	0			0	0
		16,332,777,000	13,319,877,000	29,652,654,000	4,817,732,878	10,070,508,069	14,888,240,948	29	76

4.2.2 Miradi ya Maendeleo

Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara ilipanga kutekeleza miradi ya maendeleo chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP). Ili kutekeleza miradi hiyo, kiasi cha **shilingi 553,243,220,000** zilitengwa. Kati ya fedha hizo, **shilingi 312,066,164,000** sawa na **asilimia 56** ni fedha za ndani, na **shilingi 241,177,056,000** sawa na **asilimia 44** ni fedha za nje. Mgawanyo wa fedha za maendeleo kwa Programu umeainishwa katika **Jedwali Na. 4.4**

Jedwali Na 4.4: Mgawanyo wa Fedha kwenye Programu kwa Mwaka 2013/2014

Programu	Makisio ya Bajeti (Shilingi)				
	Fedha za Ndani	Asilimia ya Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Asilimia ya Fedha za Nje	Jumla
Programu ya Utunzaji na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji	2,537,887,000	0.8	21,410,256,000	8.9	23,948,143,000
Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira	215,750,840,000	69.1	20,598,522,000	8.5	236,349,362,000

Programu	Makisio ya Bajeti (Shilingi)				
	Fedha za Ndani	Asilimia ya	Fedha za Nje	Asilimia ya	Jumla
Vijijini					
Programu ya Maji safi na Majitaka Mijini	87,612,837,000	28.1	179,383,778,000	74.4	266,996,615,000
Programu ya Kuimarisha Taasisi za Sekta ya Maji na Kujenga Uwezo	6,164,600,000	2.0	19,784,500,000	8.2	25,949,100,000
JUMLA	312,066,164,000	100	241,177,056,000	100	553,243,220,000

4.2.2.1 Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa

Hadi kufikia mwezi Machi, 2014, Wizara imepokea jumla ya **shilingi 126,232,357,750** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **shilingi 86,000,000,000** ni fedha za ndani na **shilingi 40,232,357,750** ni fedha za nje. Aidha, kwa upande wa fedha za WSDP zinazopitia kwenye mafungu mengine kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji safi na usafi wa mazingira vijijini, jumla ya **shilingi 97,300,121,338** zimetolewa. Kati ya fedha hizo, **shilingi 93,880,928,684** zimeelekezwa katika Halmashauri na Mikoa kwa ajili ujenzi na usimamizi wa miradi ya maji; na jumla ya **shilingi 3,419,192,654** zimetumwa kwenda Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa ajili ya Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira.

Jedwali Na 4.6: Hali ya Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo hadi Machi, 2014

Kifungu	Jina la Mradi	Kasma	Bajeti ya mwaka 2013/14 iliyopitishwa		Jumla ya fedha zilizotolewa	
			Ndani	Nje	Ndani	Nje
1001	Kuimarisha Taasisi za Sekta ya Maji na kujenga uwezo	3308	3,595,000,000	2,240,000,000	950,000,000	1,000,000,000
Jumla Ndogo			3,595,000,000	2,240,000,000	950,000,000	1,000,000,000
Idara ya Sera na Mipango						
1003	Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa WSDP	2325	1,842,600,000	7,014,500,000	950,000,000	2,102,623,199
	Kuijigea uwezo Wizara kutekeleza WSDP	3436	727,000,000	10,530,000,000	500,000,000	2,045,097,126
Jumla Ndogo			2,569,600,000	17,544,500,000	1,450,000,000	4,147,720,325
Idara ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji						
2001	EMA Implementation Support Project	6571	0	172,950,000	0	161,986,000
	Kuendeleza na kusimamia Rasilimali za Maji	6545	1,804,887,000	17,487,306,000	1,000,000,000	7,567,423,618
Jumla Ndogo			1,804,887,000	17,660,256,000	1,000,000,000	7,729,409,618
2003	Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji na Usimamizi wa Mfumo wa Ikolojia	3435	733,000,000	3,750,000,000	450,000,000	277,536,000
Jumla Ndogo			733,000,000	3,750,000,000	450,000,000	277,536,000
Idara ya Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini						
3001	Kukarabati na Kupanua Miradi ya maji mijini inayoendelea kutekelezwa	3306	2,912,837,000	84,243,778,000	2,700,000,000	15,868,084,578

Kifungu	Jina la Mradi	Kasma	Bajeti ya mwaka 2013/14 iliyopitishwa		Jumla ya fedha zilizotolewa	
			Ndani	Nje	Ndani	Nje
	Kukarabati na Kupanua Miradi ya maji mijini chini ya WSDP	3307	15,237,000,000	49,230,000,000	6,400,000,000	6,828,508,837
	Kuboresha upatikanaji wa Maji katika makao makuu ya Mikoa mipyta	3309	9,313,000,000	0	4,600,000,000	0
	Mradi wa Maji wa Masasi/Nachingwea	3340	750,000,000	0	200,000,000	0
	Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria - Kahama/Shinyanga na Tabora	3342	450,000,000	0	200,000,000	0
	Mradi wa Maji wa ziwa Victoria - Kahama Shinyanga	3403	900,000,000	0	200,000,000	0
	Kuboresha huduma za Maji Jiji la Dar es Salaam (DAWASA)	3437	40,000,000,000	20,580,000,000	19,000,000,000	0
	Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kidunda	3438	3,000,000,000	3,000,000,000	0	353,873,793
	Mradi wa maji wa Mpera na Kimbiji	3439	15,000,000,000	20,000,000,000	0	2,833,339,167.39
	Kujenga uwezo wa Wizara na Mamlaka za Maji Mijini ili kutekeleza WSDP	6275	50,000,000	2,330,000,000.	50,000,000	100,000,000
Jumla Ndogo			87,612,837,000	179,383,778,000	33,350,000,000	23,150,467,208
Idara ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini						
4001	Kupanua na kukarabati miradi ya maji Vijijini ambayo inaendelea	3216	25,307,722,519	1,389,310,000	7,500,000,000	0
	Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa	3223	24,655,612,813	0	6,800,000,000	0
	Mradi Wa Usambazaji Maji na	3280	142,905,704,668	0	31,700,000,000	0

Kifungu	Jina la Mradi	Kasma	Bajeti ya mwaka 2013/14 iliyopitishwa		Jumla ya fedha zilizotolewa	
			Ndani	Nje	Ndani	Nje
Usafi wa Mazingira	Usafi wa Mazingira					
	Kuboresha Upatikanaji wa maji katika miji ya Same and Mwanga	3341	20,600,000,000	11,400,000,000	2,500,000,000	0
	Kujenga Uwezo wa Halmashauri za Wilaya	6276	2,281,800,000	7,809,212,000	300,000,000	3,927,224,599
Jumla Ndogo			215,750,840,000	20,598,522,000	48,800,000,000	3,927,224,599
Jumla Kuu			312,066,164,000	241,177,056,000	86,000,000,000	40,232,357,750

5.0 MALENGO, MAFANIKIO NA CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA WAKATI WA UTEKELEZAJI KATIKA MWAKA 2013/2014

5.1. Malengo

Katika kipindi cha muda wa kati cha 2013/2014 - 2015/2016 Wizara ya Maji iliendelea na jitihada za kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji kwa kuwashirikisha wadau sambaba na kuboresha upatikanaji wa huduma za maji safi na salama kwa maendeleo ya kiuchumi na Kijamii. Katika kipindi hicho, malengo yafuatayo yalipangwa kutekelezwa:

5.1.1 Idara ya Utawala na Utumishi

- (i) Kupunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa watumishi wa Wizara na Taasisi zake kufikia kiwango cha chini kitaifa;
- (ii) Kuwezesha Mkakati wa Taifa wa Kupambana na rushwa unatekelezwa ipasavyo;
- (iii) Kuweka utaratibu mzuri kuhusu matumizi ya rasilimali na vitendea kazi vya ofisi;
- (iv) Kuwa na utaratibu mzuri kuhusu maendeleo ya watumishi na ustawi wao mahali pa kazi; na
- (v) Kuimarisha Sekta ya Maji kwa kujengea uwezo katika utekelezaji wa WSDP.

5.1.2 Kitengo cha Fedha na Uhasibu

- (i) Kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za Serikali zilizokasimiwa chini ya Wizara ya Maji kulingana na sheria na kanuni za fedha na ununuzi wa umma; na
- (ii) Kutoa huduma kwa watumishi wa Kitengo cha Fedha na Uhasibu kulingana na sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma kila mwaka.

5.1.3 Idara ya Sera na Mipango

- (i) Kuhakikisha kuwa Taasisi za Sekta ya Maji zinawezeshwa ili zitoe huduma stahiki na kuanza kujitegemea;
- (ii) Kubaini maeneo ya kufanya mageuzi (*reforms*) katika Sekta ya Maji na kuyatekeleza; na
- (iii) Kuweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa watumishi wa Idara ya Sera na Mipango;
- (iv) Kuimarisha mfumo wa kuratibu na kufuutilia utekelezaji wa WSDP ; na
- (v) Kujengea uwezo wa kisekta katika kutekeleza Miradi ya Maji.

5.1.4 Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano

- (i) Kuelimisha umma kuhusu masuala yanayohusiana na Sekta ya Maji; na
- (ii) Kuweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa watumishi wa Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano.

5.1.5 Kitengo cha Sheria

- (i) Kuweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa watumishi wa Kitengo cha Sheria; na
- (ii) Kuimarisha usimamizi wa Sheria na kanuni zinazongoza utekelezaji wa Sera ya Maji ya mwaka 2002.

5.1.6 Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi

- (i) Kuhakikisha ununuzi wa vifaa, nyenzo na huduma za ushauri wa kitaalam zinapatikana kulingana na mahitaji kwa muda uliopangwa na kwa uwazi; na
- (ii) Kuweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa watumishi wa Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi.

5.1.7 Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

- (i) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA ili kuboresha utendaji na utoaji huduma;
- (ii) Kuweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa watumishi wa Kitengo cha Mfumo wa Taarifa za Kimenejimenti; na
- (iii) Kuhakikisha TEKNOHAMA inaboreshwa ili kupokea, kuchakata na kusambaza takwimu za Sekta ya Maji

5.1.8 Kitengo cha Ukaguzi wa Hesabu za Ndani

- (i) Kukagua kumbukumbu za fedha za Wizara kwa kuzingatia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2001; na
- (ii) Kuweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa watumishi wa Kitengo cha Ukaguzi wa Hesabu za Ndani.

5.1.9 Idara ya Rasilimali za Maji

Kuzijengea uwezo ofisi za maji za mabonde ili ziweze kujiendesha zenyewe ;

- (i) Kuweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa watumishi wa Idara ya Rasilimali za Maji;
- (ii) Kuziimarisha Bodi za Mabonde yote tisa na kuziwezesha kujiendesha;
- (iii) Kuhakikisha mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa Rasilimali za maji inaandaliwa na kutekelezwa;
- (iv) Kuhakikisha miradi ya kipaumbele iliyoidhinishwa katika Mabonde yote **9** inaendelezwa na kusimamiwa kikamilifu; na

- (v) Kuhakikisha masuala ya Mazingira yanaainishwa kikamilifu kwenye utekelezaji wa miradi ya Maji.

5.1.10 Bohari Kuu ya Maji

- (i) Kuhakikisha vifaa na nyenzo za kutekeleza miradi ya maji nchini vinapatikana kulingana na mahitaji na kwa muda unaotakiwa; na
- (ii) Kuweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa watumishi wa Bohari Kuu ya Maji.

5.1.11 Idara ya Huduma za Ubora wa Maji

- (i) Kuhakikisha programu za usimamizi na uhakiki wa shughuli za ubora wa maji zinatekelezwa;
- (ii) Kuendesha shughuli za utafiti za ubora wa maji;
- (iii) Kuweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa watumishi wa Idara ya Huduma ya Maabara za Maji; na
- (iv) Kuziimarisha maabara zote 16 za maji ili ziweze kujiendesha.

5.1.12 Idara ya Huduma za Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mijini.

- (i) Kuziwezesha Mamlaka za Maji za Miji midogo ili ziweze kujitegemea;
- (ii) Kuweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa watumishi wa Idara ya Huduma za Majisafi na Uondoaji wa Majitaka Mijini;
- (iii) Kuhakikisha miradi ya maji inatekelezwa katika mamlaka za maji ili kuongeza upatikanaji wa maji kwa wakazi wa mijini kutoka **asilimia 86** katika miji mikuu 19 ya mikoa na **asilimia 53** kwa miji ya wilaya na miji midogo mwaka 2011/2012 hadi **asilimia 95** na **asilimia 57** mwaka 2015/2016;
- (iv) Kuboresha miundombinu maji ya DAWASA ili kuongeza upatikanaji wa maji kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam na miji ya Bagamoyo na Kibaha kutoka **asilimia 55** mwaka 2011/2012 hadi **asilimia 75** mwaka 2015/2016; na
- (v) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Programu ya maji (WSDP).

5.1.13 Idara ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini

- (i) Kuweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa watumishi wa Idara ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira; na
- (ii) Kuongeza upatikanaji wa majisafi na salama kwa wakazi wa vijijini kutoka **asilimia 58.7** mwaka 2010/2011 hadi **asilimia 65** mwaka 2014/2015

5.1.14 Kitengo cha Uratibu wa Programu

- (i) Kuwezesha upatikanaji wa taarifa muhimu zinazohusu Sekta ya Maji;
- (ii) Kubaini maeneo ya kufanya mageuzi (reforms) katika Sekta ya Maji na kuyatekeleza; na
- (iii) Kuweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa watumishi wa Kitengo cha Uratibu wa Programu.

5.2. UTEKELEZAJI NA MAFANIKIO

Katika kuhakikisha kuwa malengo makuu ya Sekta ya Maji yanafikiwa, Wizara imeendelea kutekeleza kazi mbalimbali. Utekelezaji wa kazi hizo na hatua zilizofikiwa hadi kufikia mwezi Machi 2014 ni kama ifuatavyo:-

5.2.1 PROGRAMU YA UTUNZAJI NA UENDELEZAJI WA RASILIMALI ZA MAJI

Katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014, Wizara iliendelea kuboresha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika mabonde tisa ya maji nchini ili kuhakikisha kuwa rasilimali za maji nchini zinaendelezwa na kusimamiwa kikamilifu. Yafuatayo yalitekelezwa katika kipindi hicho:-

a) Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

(i) *Ujenzi wa Bwawa la Lugoda/Ndembera*

Kazi ya usanifu wa Bwawa la Lugoda inaendelea ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2014, Mtaalam Mshauri amewasilisha ripoti ya kwanza (*Interim report 1*). Ripoti hiyo imejadiliwa na wadau mbalimbali na kwa sasa Mtalaam Mshauri anaendelea kuboresha rasimu hiyo kulingana na maoni yaliyotolewa. Aidha, kazi ya kufanya tathimini ya athari za kimazingira na kijamii zitakazotokana na ujenzi wa bwawa la Lugoda na Kituo cha kuzalisha umeme cha Malulumia kinachotarajiwa kujengwa inaendelea kutekelezwa ambapo Mtaalam Mshauri amewasilisha ripoti ya awali (*Inception report*). Mtaalam mshauri wa ESIA anaendelea na hatua zinazofuata baada ya kupata taarifa alizohitaji kutoka kwenye ripoti ya mtaalam anayefanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Lengo la ujenzi wa bwawa hili ni kuwezesha maji kutiririka kwa mwaka mzima kwenye Mto Ruaha hivyo kuwezesha ikolojia ya Hifadhi ya Ruaha kupata maji kwa mwaka mzima.

(ii) *Ujenzi wa Bwawa la Farkwa*

Katika kutekeleza ujenzi wa bwawa hilo, hadi kufikia Machi 2014, Mtaalam Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa bwawa amewasilisha taarifa ya hatua ya kati (*Interim report No. 1*) na sasa yuko katika maandalizi ya *Interim report No. 2*. Wizara imepitia taarifa hiyo na kuwasilisha maoni kwa Mtaalam Mshauri ili aiboreshe. Mtaalam Mshauri amekamilisha kazi ya uchunguzi wa kina wa miamba katika eneo la bwawa. Aidha, ripoti ya Athari za Kimazingira na Kijamii ESIA imewasilishwa kwenye Baraza la Taifa la Mazingira NEMC kwa ajili ya kupata kibali

cha ujenzi. Bwawa hili litakapokamilika litatumika kama chanzo cha maji kwa ajili ya Manispaa ya Dodoma na maeneo ya jirani.

(iii) ***Ukarabati wa mabwawa***

Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa mabwawa sita ya Nkiniziwa, Itobo na Uchama (Nzega); Engumet I, Engumet II na Lekeni (Monduli) yaliyopo katika Bonde la Kati imekamilika na kuwasilishwa Baraza la Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) kwa ajili ya kupata maoni ya wadau. Maoni hayo yataboresha taarifa na kisha *NEMC* watatoa kibali cha ukarabati.

(iv) ***Utafutaji wa Vyanzo vya Maji Chini ya Ardhi.***

Lengo la utafiti huu ni kubainisha maeneo yenyewe uwezekano wa kuwepo maji chini ya ardhi ili kuziwezesha Halmashauri na wananchi kwa ujumla kujua maeneo yanayofaa kuchimba visima. Hadi kufikia Mwezi Machi 2014, Wizara imefanya utafiti wa vyanzo vya Maji chini ya ardhi katika maeneo **501** yanayofaa kuchimbwa visima vya maji katika mabonde ya Rufiji (**33**), Bonde la Kati (**39**), Pangani (**149**), Wami-Ruvu (**18**), Ziwa Victoria (**40**), Ziwa Rukwa (**73**), Ziwa Tanganyika (**80**) na Ruvuma na Pwani ya Kusini (**69**), pia Wizara imesimamia uchimbaji wa Visima **152** katika mabonde ya Ruvuma (**42**), Wami/Ruvu (**55**), Rufiji (**40**) Bonde la Kati (**3**) Pangani (**4**) Ziwa Victoria (**4**) na Ziwa Tanganyika (**4**).

(v) ***Uchimbaji wa visima kwa ajili ya utafiti katika maeneo kame ya Sanya Juu na Rombo***

Lengo la kazi hii ni kufanya utafiti ili kubainisha maeneo yenyewe maji chini ya ardhi ili kuielimisha jamii iweze kujichimbia visima kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Kazi ya uchimbaji imekamilika, mkandarasi amekamilisha ujenzi wa majukwaa ya matenki ya maji, amekwisha nunua pampu ambapo kazi ya kufunga pampu inasubiri mchakato wa kuunganisha umeme. Mkataba kati ya wamiliki wa ardhi na Wizara ya Maji juu ya uendeshaji wa visima kwa manufaa ya jamii kwa ujumla umesainiwa. Maji ya visima hivyo yatatumika kwa ajili ya matumizi ya binadamu, mifugo na umwagiliaji.

(vi) ***Mradi wa uchimbaji wa visima kwenye wilaya ya Kisarawe na Kilosa***

Mradi huu wenye lengo la kuchimba **visima 55** unafadhiliwa na Serikali ya China. Uchimbaji wa **visima 53** kati ya **visima 55** umekamilika ambapo visima **25** vimechimbwa kwenye vijiji vya Ndumbalume (3) Mb Wade (6) Kivungu (10) na Kondo (6) katika wilaya za Kilosa; na visima **28** vimechimbwa kwenye vijiji vya Mzenga A (5) Mzenga B (7) Mafumbi (2) Vikumburu (7) na Manerumngu (9) katika wilaya ya Kisarawe vimenufaika na ufungaji wa pampu katika visima hivyo upo katika hatua za mwisho. Kazi ya uchimbaji wa visima vilivyobaki itaendelea katika Wilaya ya Kisarawe mwaka ujao wa fedha 2014/2015.

(vii) ***Mradi wa uchimbaji wa visima kwenye Wilaya 6 kame nchini***

Mradi huu wenye lengo la kuchimba visima **70** unafadhiliwa na Serikali ya Misri na unahusu kuwajengea uwezo wataalam wa Wizara pamoja na kuchimba visima kwenye maeneo ya Wilaya za Kiteto, Mwanga, Same, Musoma, Itilima na Bariadi. Mradi huu unatekelezwa kwa awamu ambapo

awamu ya kwanza inahusisha uchimbaji wa visima **30** kama ifuatavyo: visima **10** katika Wilaya ya Kiteto kwenye vijiji vya Namelock (Kinuao), Laalala, Dongo, Chekanao, Osteti, Katikati, Ngapapa, Loltepes, Enguseosidan na Engangongare; visima **8** katika Wilaya ya Same kwenye vijiji vya Kabavungu, Makanya, Mgwasi, Ishinde, Masandare, Gunge Mabilioni, Stealing na Kirinjiko; kisima **1** Wilayani Mwanga kwenye kijiji cha Mikuyuni; **visima 2 Wilayani Bariadi kwenye vijiji vya Nkololo na Sima; na visima 9 katika Wilaya ya Itilima kwenye vijiji vya Sunzula, Kabale, Lagangabilili, Gambasingu, Mwanunui, Nanga, Bumela, Isengwa na Laini.** Maandalizi ya uchimbaji wa visima hivyo yameanza ambapo Mkandarasi amekabidhiwa maeneo ya kazi na ataanza kazi mwezi mei, 2014.

(viii) ***Mradi wa kufanikisha uhakika wa maji kwenye eneo la SACGOT***

Mradi huu unafadibiliwa na Serikali ya Uingereza kupitia shirika lake la *DFID*. Lengo la mradi ni kubaini na kuanzisha mikakati na miundombinu itakayohakikisha upatikanaji wa rasilimali za maji kwa ajili ya kutekeleza miradi ya uwekezaji kwenye eneo la *SACGOT*.

Mradi huu unatekelezwa kwa awamu na Bodi ya Maji ya Bonde la Mto Rufiji ambapo awamu ya kwanza inahusu kujenga ofisi, kununua vitendea kazi, kukusanya takwimu na kujenga vituovya kukusanya takwimu kwenye maeneo yasiyo na mtandao wa vituo. Awamu hii inatekelezwa kwa miaka mitatu kuanzia mwezi Machi 2013.

Kazi zilizofanyika hadi sasa ni pamoja na kujenga vituo **4** vya kupima mwenendo wa hali ya hewa, kujenga vituo **12** vya kupima wingi wa maji mitoni, usanifu wa michoro ya ujenzi wa ofisi ndogo Ifakara, kupima wingi wa maji mitoni wakati wa masika (*high flow measurement*), mkataba wa ununuzi wa magari **3** umesainiwa, uundwaji wa jumuiya **2** za watumia maji, na mchakato wa uundwaji wa jumuiya **2** zingine za watumia maji unaendelea, kufanyika kwa mafunzo kwa wataalamu wa maji chini ya ardhi na kubainisha vyanzo vya maji chini ya ardhi.

(ix) ***Ujenzi wa ofisi za maji za mabonde ya Ziwa Nyasa, Tanganyika, Victoria na Bonde la Kati***

Wizara inaendelea na kazi ya ujenzi wa ofisi za maji za mabonde ya Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Ziwa Victoria na Bonde la Kati ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2014, ujenzi wa ofisi ya Bonde la Ziwa Nyasa umefikia **asilimia 98**. Kazi ya ujenzi wa ofisi za Bonde la Ziwa Victoria, Bonde la Kati na Bonde la Ziwa Tanganyika inaendelea.

(x) ***Utunzaji na Uhifadhi wa Vyanzo vya Maji***

Wizara imebainisha maeneo **161** ya vyanzo vya maji vilivyo katika hatari ya kuharibika na kuathirika kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ya ongezeko la shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo ya vyanzo hivyo. Lengo la zoezi hilo ni kuhakikisha kuwa vyanzo hivyo vinatunzwa, vinahifadhiwa na vinaendelezwa. Kati ya vyanzo vilivyobainishwa, **59** vimekwisha ainishwa kwa ajili ya kuvifanyia taratibu za kuvitangaza kuwa maeneo tengefu.

Hadi kufikia mwezi Machi, 2014, kati ya vyanzo vilivyobainishwa, mapendekezo ya vyanzo **7** katika bonde la Ziwa Rukwa vimewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya

kuvitangaza rasmi kuwa maeneo tengefu. Maeneo hayo ambayo hayakuhitaji fidia ni maeneo ya vyanzo vya maji chini ya ardhi yaliyopo Chokaa, Kidole, Kiswaga, Matundasi A & B, Mkola na bwawa la Milala. Vilevile, katika Bonde la Ruvuma na Pwani Kusini vyanzo vya maji vya chemichemi ya Mbwinji, Ndanda, Mwena na Liputu kwenye miteremko ya milima ya Makonde vimewekewa mipaka kwa lengo la kuvihifadhi. Zoezi la uchoraji wa ramani kwa ajili ya kuwasilisha Wizarani ili kuvitangaza vyanzo hivyo kwenye Gazeti la Serikali linaendelea. Aidha, zoezi la uwekaji mipaka kwenye vyanzo vya maji vya Mitema-Kitangari kwa lengo la kuvihifadhi linaendelea. Vilevile, Wizara inaendelea na taratibu za kulitenga na kulitangaza katika gazeti la Serikali eneo linalozunguka Bwawa la Mtera (*Buffer Zone*) katika Bonde la Rufiji.

(xi) ***Uandaaji wa Kanuni za Sheria ya Rasilimali za Maji***

Wizara imekamilisha kanuni **2** ambazo ni za Usalama wa Mabwawa (*Regulations for Dam Safety*) na za Utafutaji na uchimbaji wa Visima vya Maji (*Groundwater Exploration and Drilling Licensing Regulations*) za Sheria ya Rasilimali za Maji Na. **11** ya mwaka 2009. Vilevile, Wizara imekamilisha uandaaji wa mwongozo wa Usalama wa Mabwawa (*Operational Guidelines for Dam Safety*). Kanuni hizo zimesainiwa na kuanza kutumika. Aidha, Wizara imekamilisha kutafsiri Sheria **Na. 11** ya Mwaka 2009 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji kwa lugha ya Kiswahili ili iweze kueleweka na kutumika na wadau mbalimbali. Rasimu ya tafsiri ya sheria hiyo imewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kutangazwa katika gazeti la Serikali.

(xii) ***Kuanzisha Kamati za kuhifadhi vyanzo vya Maji (Water Catchment Committees)***

Wizara inaendelea kuhamasisha wananchi katika maeneo mbalimbali nchini kuanzisha Kamati za kuhifadhi vyanzo vya maji. Hadi kufikia mwezi Machi 2013, Kamati ya kuhifadhi chanzo cha Maji cha Kihansi imeundwa kwa mujibu wa Sheria **Na. 11** ya Mwaka 2009 ya Usimamizi wa Rasilimali.

(xiii) ***Kufanya Utafiti wa Rasilimali za Maji***

Wizara imeanza kujenga uwezo wa Bodi za Maji za Mabonde katika kufanya tafiti mbalimbali za rasilimali za maji nchini. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014, Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Rukwa ilikamilisha kufanya utafiti wa “*Bathmetry*” ya Ziwa Rukwa. Utafiti huu umewezesha kujua wingi (ujazo) wa maji yaliyomo ziwani na eneo la maji la ziwa kulingana na kina cha maji ya ziwa hilo kutoka usawa wa Bahari.

(xiv) ***Kuunda na Kuimarisha Jumuiya za Watumia Maji***

Wizara imeendelea na jukumu la kuanzisha jumuiya za watumiaji maji katika mabonde yote tisa nchini. Hadi kufikia mwezi Machi 2014, jumla ya jumuiya za watumia maji **99** (*Water User Associations - WUAs*) ziliundwa. Kati ya hizo, jumuiya **18** ziliundwa katika mwaka 2013/2014.

(xv) ***Kutoa Vibali vya Kutumia Maji na Kutiririsha Majitaka***

Wizara kupitia Ofisi za Mabonde imeendelea kutoa vibali vya kutumia maji na kutiririsha majitaka kwa mujibu wa Sheria ya Rasilimali za Maji. Hadi kufikia mwezi Machi 2014, jumla ya vibali vipyta **586** vilitolewa katika mabonde ya Pangani (**105**), Rufiji (**92**), Wami-Ruvu (**112**), Ruvuma na Pwani ya Kusini (**21**), Bonde la Kati (**3**), Ziwa Victoria (**37**), Ziwa Rukwa (**66**), Ziwa Nyasa (**94**) na

Ziwa Tanganyika (**56**). Jumla ya maombi **223** yalipokelewa katika mabonde ya Ziwa Rukwa (**19**), Ziwa Tanganyika (**50**), Wami-Ruvu (**77**), Ziwa Nyasa (**60**) na Ruvuma na Pwani ya Kusini (**17**). Vilevile, usajili wa vibali vya zamani (*re-registration*) ulifanyika ambapo vibali **479** kutoka katika mabonde ya Ziwa Nyasa (**4**), Ziwa Victoria (**370**) na Wami-Ruvu (**105**) vilihakikiwa na kusajiliwa upya ili kuendana na matakwa ya Sheria Na. 11 ya mwaka 2009 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji.

Hadi kufikia mwezi **Machi 2014**, jumla ya vibali **15** vya kutiririsha majitaka vilitolewa katika mabonde ya Ziwa Victoria (**10**), Ziwa Rukwa (**3**) na Pangani (**2**). Aidha, zoezi la kuwatambua watumiaji maji kwa matumizi mbalimbali lilifanyika ili waweze kupatiwa elimu na hatimaye kuweza kufuata taratibu za kisheria za matumizi endelevu ya maji. Jumla ya **watumiaji maji 835** walibainishwa katika mabonde ya Pangani (**513**), Ziwa Victoria (**27**), Ziwa Tanganyika (**162**), Ruvuma na Pwani ya Kusini (**19**) Ziwa Nyasa (**24**) na Wami-Ruvu (**90**). Katika Bonde la Wami-Ruvu ilibainika kuwa, baadhi ya watumia maji ni wavamizi wanaojishughulisha na uchimbaji mdogo wa madini unaosababisha uharibifu mkubwa wa vyanzo vya maji. Wavamizi hao wamepewa agizo la kuacha kufanya shughuli hizo katika vyanzo vya maji.

(xvi) **Kusimamia Utekelezaji wa Sheria na Kutatua Migogoro ya Watumia Maji**

Miongoni mwa majukumu ya bodi za maji za mabonde ni kusuluhisha migogoro katika matumizi ya maji kwa kushirikiana na jumuiya za watumia maji na inapobidi vyombo vya sheria hutumika. Hadi kufikia mwezi Machi 2014, migogoro **29** ya watumiaji maji ilijitokeza, ambapo migogoro **21** kati ya hiyo ilipatiwa suluhu katika Mabonde ya Maji ya Pangani (**5**), Wami/Ruvu (**10**), Ziwa Victoria (**2**), Rufiji (**2**) Ziwa Nyasa (**1**), Ruvuma na Pwani ya Kusini (**1**). Migogoro mingine sita (**6**) ipo katika hatua mbalimbali za mashauriano, katika Bonde la Kati (**6**) na Ziwa Victoria (**2**). Migogoro miwili (**2**) katika Bonde la Pangani ipo mahakamani.

(xvii) **Ukarabati na ujenzi wa vituo vya kupima mwenendo na hali ya maji**

Wizara imeendelea kuimarisha vituo vya kufuutilia wingi na ubora wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi ili kuboresha upatikanaji wa takwimu na taarifa sahihi na kwa wakati. Hadi kufikia mwezi Machi 2014, jumla ya vituo **29** vya kupima mtiririko wa maji mitoni (*hydrometric stations*), vituo **14** vya hali ya hewa (*meteorological/weather stations*), vituo sita (**6**) vya ufuutiliaji maji chini ya ardhi, vituo vitatu (**3**) vya kupima maji kwenye maziwa na vituo **7** vya kupima mvua vilijengwa katika mabonde ya Wami-Ruvu, Pangani, Ziwa Rukwa, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini. Vilevile, ukarabati ulifanyika katika vituo **80** vya kupima mtiririko wa maji kwenye mito mbalimbali nchini, vituo **18** vya hali ya hewa, vituo viwili (**2**) vya ufuutiliaji maji chini ya ardhi, vituo vitatu (**3**) vya kupima maji kwenye maziwa, vituo vitano (**5**) vya kupima maji kwenye mabwawa na vituo sita (**6**) vya kupima mvua. **Kiambatisho Na. 7.**

Katika kuhakikisha upatikanaji wa takwimu sahihi za hali ya maji nchini, bodi za maji za mabonde zimekusanya na kuchanganua takwimu za hali ya maji katika vituo mbalimbali. Vituo hivyo vinajumuisha vituo **203** vya kupima mtiririko wa maji mitoni, vituo **12** vya kupima usawa wa maji katika maziwa na mabwawa, vituo **122** vya kupima mvua na vituo **29** vya kupima hali ya hewa. Takwimu hizi zinawezesha bodi za Maji za Mabonde kuandaa taarifa za hali ya maji za kila mwaka.

(xviii) ***Utekelezaji wa Mkakati wa Usimamizi wa Ubora na kuzuia uchafuzi wa maji***

Jumla ya sampuli **408** zilifanyiwa uchunguzi katika maabara mbalimbali nchini ambapo sampuli **98** kati ya sampuli **408** zilizopimwa zilionesha kuwa na vimelea vya wadudu. Aidha, Bonde la Pangani liliwasilisha sampuli **11** za majitaka kutoka katika mashamba ya mikonge, kahawa pamoja na mfumo wa uondoaji majitaka, kati ya hizo, sampuli **10** hazikukidhi viwango. Wahusika waliagizwa waboreshe mifumo yao ya kusafisha majitaka. Ugazusi ulifanyika katika bonde la kati kwenye maeneo **9** ya viwanda, migodi **46** na hoteli **3**. Katika bonde la Pangani, ugazusi ulifanyika katika mifumo ya utoaji majitaka ya viwanda **vitatu** na kuangalia utendaji kazi (*performance assessment*) wa mabwawa ya majitaka ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha. Katika maeneo ambayo vyanzo vya maji vilibainika kuwa na vijidudu, maelekezo yalitolewa kwamba maji yatibiwe ili kuondoa vijijidudu hivyo kwa lengo la kukidhi viwango vya ubora wa maji. Aidha, katika maeneo yaliyobainika kuwa na vyanzo vya maji vyenye chumvi, ilishauri vitafutwe vyanzo mbadala na yale yaliyoonekana kuwa na madini ya *fluoride*, ilisahauriwa kutumia teknolojia ya kuondoa *fluoride* kwenye maji.

(xix) ***Uandaaji wa Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji Rasilimali za Maji***

Katika mwaka 2013/2014, Wizara iliendelea na utayarishaji wa Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji katika mabonde yote tisa. Hadi kufikia Machi 2014, rasimu za mwisho za mipango katika mabonde ya Ruvuma na Pwani ya Kusini, Bonde la Kat, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa ziliendelea kufanyiwa kazi na wataalam washauri baada ya kupokea maoni na marekebisho kutoka kwa wadau. Wataalam washauri katika bonde la Ziwa Rukwa, Pangani na Rufiji wamewasilisha taarifa ya kati na maoni ya Wizara yamewasilishwa kwa Wataalam Washauri kwa ajili ya marekebisho. Katika bonde la Wami/Ruvu, taarifa ya mwisho ya mpango shirikishi wa usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji imekamilika na kuwasilishwa Wizarani mwezi Januari, 2014. Mpango shirikishi wa usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika Ziwa Victoria upo katika hatua za awali za ukusanyaji wa takwimu na taarifa muhimu kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(xx) ***Kusimamia na kushiriki kwenye miradi na Programu za Kimataifa***

Mabonde saba (**7**) kati ya tisa (**9**) yaliyopo nchini yanavuka mipaka ya nchi yetu na hivyo kuwa na ulazima wa kushirikiana na nchi **17** katika uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji. Nchi hizo ni Angola, Botswana, Namibia, Zambia, Zimbabwe, Malawi, Msambiji, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Misri, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Sudan, Sudan Kusini, Uganda na Eritrea. Ushirikiano wa kitaasisi na nchi hizo unatekelezwa kama ifuatavyo:-

• **Bonde la Mto Nile**

Jumla ya **nchi 11** zinaunda umoja wa Ushirikiano wa Nchi za Bonde la Mto Nile (*Nile Basin Initiative – NBI*) ulioanzishwa rasmi mwaka 1999. Nchi hizo ni Burundi, Eritrea, Ethiopia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Misri, Rwanda, Sudan, Sudan Kusini, Tanzania na Uganda na nchi ya Eritrea ikiwa ni mtazamaji (*observer*).

Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria

Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali za Burundi, Kenya, Rwanda na Uganda zimeendelea kutekeleza Awamu ya Pili ya Mradi wa Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria (*LVEMP II*). Nchi yetu inanufaika na Mradi huo kwa kuimarisha taasisi zinazohusika na hifadhi ya maji na samaki; ukarabati wa mifumo ya kusafisha majitaka katika miji ya Mwanza, Musoma na Bukoba. Vilevile, Halmashauri za Wilaya ya Maswa, Itilima, Busega, Bariadi, Magu, Meatu, Kwindu, Sengerema, Geita, Chato, Muleba, Karagwe, Kyerwa na Misenyi zimeingizwa kwenye awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi huo.

Hadi mwezi Machi 2014, jumla ya miradi midogo **176** ya kijamii yene thamani ya **Dola za Marekani milioni 4.5** inatekelezwa. Kati ya miradi hiyo, **48** imekamilika tayari kwa kukabidhiwa kwa jamii. Vilevile, miradi **22** mikubwa ya kijamii (*Co – Management Interventions*) yene thamani ya **Dola za Marekani milioni 5.5** imeanzishwa katika wilaya za Musoma Mjini, Maswa, Bariadi, Kwindu, Magu, Meatu na jiji la Mwanza.

- **Bonde la Mto Ruvuma**

Mradi wa Maji Shirikishi wa Bonde la Mto Ruvuma unahusisha nchi za Msumbiji na Tanzania na kuratibiwa na Sekretarieti ya *SADC*. Hapa nchini mradi unatekelezwa katika wilaya **tano (5)** za mikoa ya Mtwara na Ruvuma ambazo ni Songea Vijijini, Tunduru, Tandahimba, Nanyumbu na Mbanga. Katika mwaka 2013/2014, miradi miwili ya kijamii imeendelea kutekelezwa katika wilaya ya Tunduru ambapo jumla ya miche ya **miti 5,733** imepandwa katika vijiji vya Daraja Mbili, Nandembo, Lelolelo na Majimaji kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa ardhi na kutunza vyanzo vya maji.

Katika skimu ya umwagiliaji ya Namatuhi iliyoko Wilaya ya Songea Vijijini, mkandarasi anaendelea na kazi ya ujenzi wa mifereji midogo yene urefu wa **miti 550** na mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2014. Aidha, uchimbaji wa kisima kirefu cha mita **150** kwa ajili ya mradi wa usambazaji wa maji katika kijiji cha Mihambwe, Wilaya ya Tandahimba umekamilika. Vilevile, utekelezaji wa mradi wa kusambaza maji katika kijiji cha Mahande, Wilaya ya Mbanga umekamilika.

- **Bonde la Mto Songwe**

Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Malawi imeendelea kutekeleza Awamu ya Pili ya Programu ya kuendeleza rasilimali za Bonde la Mto Songwe. Awamu hii ya pili ya programu inahusu usanifu wa kina wa skimu ya umwagiliaji na mabwawa **matatu** kwa ajili ya kuzalisha umeme, kilimo cha umwagiliaji na kuzuia mafuriko. Jumla ya hekta **3,005** zinatarajiwa kumwagiliwa na megawati **362** za umeme kuzalishwa Aidha, Mtaalam Mshauri ataandaa mpango wa kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Kusimamia Programu na kujenga uwezo kwa watekelezaji wa programu katika ngazi za halmashauri hadi Taifa. Kazi hizi zinatarajiwa kukamilika mwezi Juni mwaka 2015.

Hadi kufikia mwezi Machi 2014, Mtaalam Mshauri amekamilisha usanifu wa awali wa mabwawa **matatu**. Aidha, mkakati wa kutoa elimu na mawasiliano umekamilika na kuanza kutekelezwa

kwenye Halmashauri za Wilaya za Mbeya na Momba kwa upande wa Tanzania, na katika wilaya za Karonga na Chitipa kwa upande wa Malawi.

- **Ziwa Tanganyika**

Wizara imeendelea kushirikiana na nchi wanachama wa Mamlaka ya Bonde la Ziwa Tanganyika ambazo ni Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (*DRC*), na Zambia katika usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji. Tanzania na *DRC* zinamiliki kwa pamoja **asilimia 86** ya Ziwa hilo. Kumekuwa na changamoto ya kushuka kwa kina cha maji ya Ziwa Tanganyika hivyo kuathiri miundombinu ya Bandari na Chanzo cha maji kwa Mji wa Kigoma. Jitihada mbalimbali zimefanyika kudhibiti hali hiyo ikiwa ni pamoja na kukamilika kwa usanifu wa kina wa banio lillobomoka kwenye mto Lukuga.

Jumla ya **Dola za Marekani milioni 65** zinahitajika kutekeleza miradi ya kudhibiti kushuka kwa kina cha ziwa hilo. Mwezi Aprili, 2014 Serikali za Tanzania na *DRC* zimesaini makubaliano kwa ajili ya kuwa na mradi wa pamoja wa kuwezesha kina cha maji cha Ziwa Tanganyika kurudi katika hali yake ya kawaida. Mradi huo utahusisha kujegwa kwa banio katika mto Lukuga na uhifadhi wa Mazingira kwenye Bonde la Ziwa Tanganyika.

- **Ziwa Chala, Ziwa Jipe na Mto Umba**

Hati ya Makubaliano (*MoU*) kati ya nchi za Tanzania na Kenya kuhusu utunzaji na uendelezaji wa ikolojia ya maziwa ya Chala na Jipe; na Mto Umba ilisainiwa mwezi Februari, 2013. Kulingana na makubaliano hayo kazi kubwa itakuwa ni kusimamia na kuendeleza rasilimali zilizoko katika maeneo hayo ili matumizi yake yawe endelevu ikiwa ni pamoja na kulinda mifumo ya ikolojia kwa ustawi wa wananchi wa nchi hizo.

Kikao cha pamoja kati ya Tanzania na Kenya kilifanyika mjini Taveta mwezi Machi 2014 na kufikia maridhiano ya mpango wa kitaalam wa kutumia maji ya Ziwa Chala kwa ajili ya matumizi ya wakazi wanaozunguka ziwa hilo uandaliwe, ikizingatiwa kuwa eneo linalozunguka ziwa hilo ni kame.

b) Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji na Usimamizi wa Mfumo wa Ikolojia

Moja ya majukumu ya Wizara ya Maji ni kuhakiki ubora na usafi wa maji katika vyanzo vya maji na mitando ya kusambaza maji kwa lengo la kulinda afya za wananchi na mazingira. Katika kutimiza jukumu hilo, kwa mwaka 2013/2014 Wizara ilipanga kuimarisha maabara **16** za kupima ubora wa maji nchini kwa kununua vifaa, samani za maabara na kemikali za maabara; kukamilisha na kuanza utekelezaji wa mkakati wa teknolojia ya *Defluoridation*; kugharamia utekelezaji wa mkakati wa usimamizi wa ubora wa maji na udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya maji na kukamilisha na kutekeleza mpango wa upatikanaji wa ithibati (*accreditation*) kwa maabara za maji. Utekelezaji wa kazi hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Ununuzi wa vifaa na madawa kwa Maabara 16 za Maji.

Katika kuziimarisha na kuzijengea uwezo Maabara za Maji nchini, Wizara imekamilisha taratibu za ununuzi wa madawa kwa kusaini mkataba na mzabuni mwezi Januari 2014. Mzabuni anatakiwa

kukamilisha uletaji wa madawa hayo ndani ya miezi 4 tangu kusainiwa kwa mkataba. Aidha, Wizara ilivunja mkataba wa ununuvi wa vifaa vya maabara mwezi Oktoba 2013 baada ya mzabuni kukiuka masharti ya mkataba. Kwa sasa *Specifications* kwa ajili ya ununuvi wa vifaa hivyo zimekamilika baada ya kufanyiwa mapitio upya na taratibu za uandaaji wa makabrasha ya zabuni zinaendelea.

(ii) **Kukamilisha na kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Teknolojia ya Defluoridation**

Mkakati wa kusambaza teknolojia ya kuondoa madini ya *fluoride* katika maji ya kunywa na kupikia (*Defluoridation Technology*) umekamilika. Mkakati huo unaainisha mbinu za kusambaza teknolojia ya kutumia mkaa wa mifupa ya ng'ombe kuondoa madini ya *fluoride* katika maji ya kunywa. Utekelezaji wa mkakati huo umeanza kwa kufanya yafuatayo:-

- Kujenga tanuru **mbili** zenyewe uwezo wa kuchoma **tani nne** za mifupa ya ng'ombe kwa mara moja. Majaribio ya kubaini ufanisi wa uchomaji wa matanuru hayo yanaendelea ambapo jaribio la kwanza kilogramu **3,820** za mifupa ya ng'ombe zilitumika. Ukusanyaji wa mifupa unaendelea kwa ajili ya kubaini ufanisi wa matanuru hayo.
- Ununuvi wa mtambo (*mould*) kwa ajili ya kuzalisha vifaa vinavyotumika kuondoa madini ya *fluoride* katika maji ya kunywa na kupikia kwa ngazi ya kaya umekamilika. Kwa sasa zoezi linaloendelea ni kufanya majaribio ya mtambo (*mould*) kuhakiki ufanisi wake katika kuzalisha vifaa **1,000** vya awali vitakavyosambazwa kwenye familia zinazoishi katika maeneo yaliyoathirika sana. Lengo la zoezi hilo ni kuhamasisha wananchi kutumia teknolojia ya kutumia mkaa wa mifupa ya ng'ombe kuondoa madini ya *fluoride* katika maji ya kunywa na kupikia kwa kipindi ambacho tafiti zinaendelea za kupatikana kwa teknolojia mbadala na rahisi kutumika vijijini.
- Ili kudhibiti ubora wa mkaa wa mifupa ya ng'ombe unaozalishwa, kituo cha utafiti cha Ngurdoto kimebuni mifuko maalum ya kuhifadhiwa mkaa huo. Kwa kuanzia utengenezaji wa mifuko **5,000** yenye ujazo wa kilogramu tano kila mmoja umekamilika.
- Katika kujenga uelewa wa wadau kuhusu matumizi ya teknolojia ya kutumia mkaa wa mifupa ya ng'ombe kuondoa madini ya *fluoride*, mwezi Novemba 2013, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilitembelea Kituo cha Utafiti wa *Fluoride* – Ngurdoto mkoani Arusha pamoja na wananchi wanaotumia vifaa vya kuondolea madini hayo katika maji ya kunywa vilivyobuniwa na kituo hicho. Lengo la ziara hiyo lilikuwa kutoa fursa kwa kamati ya bunge kuona utafiti unaofanyika na kupata taarifa ya hatua iliyofikiwa ya matumizi ya teknolojia ya kutumia chengachenga za mkaa wa mifupa ya ng'ombe (*Bone char filter media*). Wajumbe katika ziara hiyo waliridhika na jitihada zinazofanywa na Serikali katika kutatua tatizo la madini ya *fluoride* kwenye maji ya kunywa na kushauri kuwa, kuwe na mipango endelevu katika upatikanaji wa majisafi na salama kwa ajili ya maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

(iii) ***Utekelezaji wa mkakati wa usimamizi wa ubora wa maji na udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya maji***

Katika kipindi cha mwezi Julai 2013 hadi Machi 2014, kazi zilizofanyika ni pamoja na kukusanya na kuchunguza sampuli za maji **4,673** kati ya sampuli **8,000** zilizopangwa, na sampuli **630** za majitaka kati ya **1,000** zilizopangwa kukusanya na kuchunguzwa kwa mwaka.

- Kati ya sampuli **4,673**, sampuli **3,200** zilikusanya na kuchuguzwa kwa ajili ya matumizi ya majumbani na sampuli **1,473** zilikuwa kwa ajili ya matumizi mengine kama vile utafiti, viwandani, umwagiliaji na ufuatiliaji wa mwenendo wa ubora wa maji katika vyanzo.

Matokeo ya uchunguzi yalionyesha kuwa asilimia **asilimia 89.9** ya sampuli kwa ajili ya matumizi ya majumbani maji yake yanakidhi viwango vinavyokubalika. **Asilimia 10.1** ya sampuli hizo, maji yake hayakukidhi viwango vinavyokubalika kutokana na uwepo wa kiwango kikubwa cha chumvichumvi, madini-chuma (*iron*), *manganese* na *fluoride*; ambapo ushauri ultolewa kuwa maji hayo yafanyiwe *aeration*, kutumia teknolojia ya mkaa wa mifupa ya ng'ombe au kutafuta vyanzo mbadala. Sampuli kwa ajili ya matumizi mengine zilikidhi viwango kwa matumizi yaliyokusudiwa.

- Sampuli **630** za majitaka kati ya sampuli **1,000** zilizopangwa kukusanya na kipindi cha mwaka toka katika mabwawa na mitambo ya majitaka na kuchunguzwa ubora wake. Kati ya hizo, sampuli **120** zilichunguzwa kwa lengo la kuhakiki uwezo (ufanisi) wa mabwawa kusafisha majitaka na sampuli **510** zililenga kuhakiki ubora wa majitaka yanayotakiwa kumwagwa kwenye mazingira kama yanakidhi viwango vilivyowekwa. Matokeo ya uchunguzi yalibainisha kuwa **asilimia 85** ya mifumo ya mabwawa kuwa na ufanisi mkubwa wa kusafisha majitaka na hivyo kukidhi viwango vya kutokuwa na athari kwenye mazingira. **Asilimia 15** ya sampuli ilionesha kuwa mifumo hiyo haikidhi viwango vinavyotakiwa, na hivyo ushauri wa kitaalam juu ya njia bora za kuboresha mabwawa na mitambo ya kusafisha majitaka ultolewa kwa taasisi husika.

(iv) ***Kutekeleza mpango wa upatikanaji wa ithibati (accreditation) kwa maabara za maji.***

Katika mchakato wa kupata ithibati, maabara za maji zinatakiwa kushiriki kwenye zoezi la kujipima uwezo wa utendaji kazi za kimaabara (*Laboratory Performance Evaluation or Proficiency Testing*). Kupatikana kwa ithibati kutafanya Maabara zetu kutambulika kimataifa na zitakuwa zimekidhi matakwa ya Sheria Na. 11 ya mwaka 2009 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Sheria Na. 12 ya mwaka 2009 ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira na Sheria Na. 20 ya mwaka 2004 ya Usimamizi wa Mazingira.

Katika mwaka wa fedha 2013/2014, maabara za Dar es Salaam, Mwanza, Iringa, Mbeya, Tanga, Arusha, Dodoma, Mtwara, Bukoba, na Morogoro zilishiriki zoezi la kujipima uwezo wa utendaji kazi chini ya mpango wa *Southern Africa Development Community Measurement Traceability (SADCMET)* unaoratibiwa na Shirika la Maji la Namibia (*NAM WATER PT Provider-Namibia Water Corporation*) na programu ya *Global Environmental Monitoring System/Water (GEMS/Water)*. Tathmini ya matokeo ya majoribio hayo imeonyesha kuwa maabara zilizoshiriki

zimefanya vizuri kwa wastani wa **asilimia 65** kwa vielelezo (*parameters*) vya kemikali na **asilimia 92** katika upimaji wa vimelea vya vijidudu (*bacteria*) kwenye maji.

Katika jitihada zinazoendelea za maabara za maji kupata ithibati, Maabara ya Maji Mwanza imekamilisha uandaaji wa mwongozo wa utendaji kazi (*Quality Manual*) na kuwasilisha kwa taasisi inayosimamia shughuli hizo ambayo ni *Southern Africa Development Community Accreditation System (SADCAS)* kwa ajili ya kufanyiwa tathmini.

5.2.2 HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJJINI

Katika mwaka wa fedha 2013/14 Serikali ilitenga **shilingi 345,005,362,000** kwa ajili ya miradi ya maji vijijini. Kati ya fedha hizo **shilingi 215,750,840,000** ni fedha za Ndani na **shilingi 129,254,522,000** ni fedha za Nje. Hadi mwezi Machi 2014, fedha zilizotolewa kwenye miradi ya maji vijijini ni **shilingi 148,515,345,941** (sawa na **asilimia 43** ya bajeti). Kati ya fedha hizi, **shilingi 137,904,598,951** zimeelekezwa kutekeleza mradi wa vijiji **10** kwa kila Halmashauri; ambapo kati ya fedha hizo, **shilingi 34,311,371,348** (sawa na **asilimia 15.9** ya fedha za ndani) ni fedha za ndani na **shilingi 103,593,227,603** (sawa na **asilimia 80** ya fedha za nje) ni fedha za nje. Fedha zinazobaki **shilingi 10,610,746,990** zimeelekezwa kwenye miradi mingine ya maji vijijini kama vile miradi ya matokeo ya haraka (*Quickwins*), ujenzi wa mabwawa, Same-Mwanga-Korogwe, na gharama za ziada za usimamizi na ufuutiliaji wa miradi. Mchanganuo wa fedha zilizopelekwa kwenye miradi ya maji vijijini kwa mwaka wa fedha 2013/14 ni kama unavyoonekana katika **Kiambatisho Na.2**.

Kuanzia mwaka wa fedha 2013/14, miradi ya Maji na Usafi wa Mazingizra Vijijini ilianza kutekelezwa kwa utaratibu wa “Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa” (*Big Results Now – BRN*). Utaratibu huu umelenga kuongeza kasi katika utekelezaji wa miradi ili kuongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi waishio vijijini kutoka **asilimia 40** (baada ya mapitio ya BRN)² mwezi Juni, 2013 hadi kufikia **asilimia 74** ifikapo mwezi Juni, 2016. Mpango wa BRN unahu utekelezaji katika maeneo manne (4) ambayo ni Ujenzi wa miradi mipya (*new construction*), ukarabati wa miradi chakavu (*rehabilitation*), upanuzi wa miradi iliyopo (*extension*) na uendeshaji na matengenezo (*operation and maintenance*).

Ujenzi wa miradi mipya unahu ishisha miradi ya vijiji kumi kila Halmashauri pamoja na miradi ya kimkakati (*strategic projects*), wakati upanuzi na ukarabati unahu ishisha ujenzi wa miradi ya matokeo ya haraka (*Quick-win Projects*) kutoka kwenye vyanzo vya mabwawa, visima virefu, vyanzo vidogo vya juu ya ardhi, miradi ya kitaifa na miradi inayohitaji matengenezo.

Eneo la uendeshaji na matengenezo linahusu uanzishaji na uendeshaji wa vyombo vya watumiaji maji (*COWSOs*), uanzishwaji wa vituo vya kutoa huduma ya matengezo na ukusanyaji wa taarifa za utekelezaji wa miradi ya maji vijijini.

² Mapitio yaliyofanyika wakati wa maandalizi ya BRN kwa Sekta ya Maji yalionyesha kuwa maji hayatoki maeneo mengi kutoekana na miundombinu kutokfanyiwa matengenezo (*maintenance*). Mapitio haya yalionesha kuwa hali halisi ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini ni **40%** mwezi Juni, 2013 badala ya **57.8 %** iliyokuwa imeripotiwa mwezi Desemba, 2012.

Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali iliendelea kutekeleza miradi ya maji kwa ajili ya kuhudumia wananchi wa vijiji chini ya mpango wa *BRN*. Kati ya mwezi Julai, 2013 hadi mwezi Machi 2014, jumla ya miradi **248** imejengwa katika vijiji **270** kwenye Halmashauri **98**. Juhudi hizi zimeongeza idadi ya wakazi wanaopata huduma ya majisafi na salama kutoka **15,200,000 (asilimia 40)** Mwezi Juni, 2013 hadi kufikia wakazi **17,840,000 (asilimia 49)** sawa na ongezeko la wakazi wapatao **2,640,000 (asilimia 9)** wanaohudumiwa na vituo vya kuchotea maji **10,560**. Lengo la Serikali ni kuwapatia maji jumla ya wananchi **milioni 22** waishio vijiji ifikapo mwezi Juni, 2014. Aidha, vyombo vya watumia maji (*COWSOS*) **373** vimeundwa.

a). Ujenzi wa miradi mipyä

Miradi ya maji katika vijiji 10 kila halmashauri

Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa maji wa vijiji kumi kwa kila Halmashauri nchini ambao ulilenga kujenga miradi **1,473** kwenye vijiji **1,555**. Mradi huo ukikamilika, vituo vya kuchotea maji **32,274** vyenye uwezo wa kuhudumia wananchi wapatao **8,068,500** vitakuwa vimejengwa. Hadi mwezi Machi 2014, hatua zilizofikiwa katika utekelezaji ni kama ifuatavyo:

- **Miradi iliyokamilika:** miradi **228** kwenye vijiji **247** imekamilika ambapo jumla ya vituo **9,594** vya kuchotea maji vyenye uwezo wa kuhudumia watu **2,398,500** vimejengwa;
- **Miradi inayoendelea kujengwa:** miradi **538** kwenye vijiji **583** itakayokuwa na vituo **9,630** yenye uwezo wa kuhudumia watu **2,407,500** inaendelea kujengwa;
- **Mikataba iliyosainiwa:** mikataba ya ujenzi wa miradi **707** kwa ajili ya vijiji **725** itakayokuwa na vituo **13,050** vyenye uwezo wa kuhudumia watu **3,262,500** imesainiwa na utekelezaji utaendelea katika mwaka wa fedha 2014/15.

Taarifa ya kina kuhusu utekelezaji wa miradi ya Vijiji **10** ni kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na. 1**.

Miradi ya Kimkakati (Strategic Projects)

➤ **Mradi wa Maji Masoko**

Mradi ulianza kujengwa mwezi Septemba 2010 na unahusisha ujenzi wa banio la maji, chujio la maji, matanki **matatu (3)** yenye ujazo wa **lita 90,000** kila moja, vituo **122** vya kuchotea maji, ununuzi wa pampu na ulazaji wa mabomba. Mradi ukikamilika utanufaisha wakazi **15,158** wa vijiji 15 vya Bulongwe, Igeme, Ngaseke, Ntandabala, Lupando, Bujesi, Lufumbi, Busisa, Mbaka, Isabula, Lwifwa, Ikama, Itagata, Nsanga na Nsyasa. Kazi zilizofanyika hadi kufikia mwezi Machi, 2014 ni ujenzi wa mabanio (*intakes*) ya maji ya Mbaka na Kigange, uchimbaji wa mtaro na kulaza mabomba.

➤ **Mradi wa Maji wa Mwakaleli I**

Mradi huu ulianza kutekelezwa mwaka 2010 ukiwa na lengo la kujenga mabanio (*intakes*) **6**, kujenga beseni **2** za kuchuja maji (*sedimentation tank*), kujenga matanki **14** ya kuhifadhia maji,

matanki **21** ya kupunguza msukumo wa maji (*Break Pressure Tanks*), ulazaji wa mabomba yenye urefu wa **kilometra 134** na ujenzi wa vituo **184** vya kuchotea maji. Mradi huu unahudumia vijiji **15** na vitongoji vinne.

Kazi zilizofanyika hadi mwezi Machi, 2014 ni ujenzi wa mabanio **matano**, matanki **14** ya kuhifadhi maji, vituo vya kuchotea maji **184** na uchimbaji wa mifereji ya kulaza mabomba ya maji umbali wa **kilometra 120**. Kazi zilizobaki zinatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2014/2015.

➤ **Mradi wa Maji Matema**

Mradi huu ulianza kutekelezwa mwaka 2010 na unalenga kujenga chujio jipya la maji (*intake box*), kujenga tanki la kuchuja maji (*sedmantation tank*), ujenzi wa tanki la mita za ujazo **225** na kulaza mabomba yenye urefu wa **kilometra 21**. Hadi kufikia mwezi Machi 2014, ujenzi wa chujio na kituo kimoja cha kuchotea maji (Shulen) umekamilika na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji unaendelea. Mradi utakapokamilika watu wapatao **14,929** wa vijiji vya Mababu, Kilombero, Kisyosyo na Matema watapata huduma ya maji. Ujenzi wa mradi huu unatarajia kukamilika mwaka 2014/2015.

➤ **Mradi wa Maji Vijijini katika Mkoa wa Tabora**

Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Japan inatekeleza mradi wa maji katika **vijiji 20** kwenye wilaya zote **saba** za mkoa wa Tabora. Mradi una awamu mbili; awamu ya kwanza ilianza mwezi Septemba, 2009 na kukamilika mwezi Machi, 2014.

Katika awamu hiyo, kazi zilizotekeliza ni kukarabati visima virefu na vifupi **46** vya pampu za mikono katika Wilaya **6**; kuandaa Mpango wa Maji Vijijini kwa Mkoa ambao unaainisha maeneo ya kipaumbele ya kutekeleza miradi ya maji; kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi ya maji katika **vijiji 20**. Awamu ya pili ya mradi imeanza na mkandarasi amepatikana. Mradi unakadiriwa kugharimu **shilingi bilioni 25** na ukikamilika utanufaisha wananchi zaidi ya **45,000**.

Mradi wa Maji wa Same – Mwanga – Korogwe

Serikali kwa kushirikiana na *BADEA*, *OFID* na *KUWAIT FUND* inaendelea kutekeleza mradi wa Same-Mwanga-Korogwe. Mradi huo unalenga kupeleka maji katika miji ya Same na Mwanga ambayo ina tatizo kubwa la maji. Mradi huo utakapokamilika utahudumia wananchi **456,931** wa miji hiyo pamoja na vijiji **38** vilivyopo katika Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe ifikapo mwaka 2038.

Mradi huo unatekelezwa katika awamu mbili ambapo kwa awamu ya kwanza inakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 177** na itahusisha ujenzi wa miundombinu ya maji katika miji ya Same na Mwanga na vijiji 9. Kazi zitakazofanyika ni kama ifuatavyo: ujenzi wa chanzo cha maji katika Mto Pangani karibu na bwawa la Nyumba ya Mungu; mtambo wa kusukuma maji kutoka chanzo cha maji; mitambo ya kusafisha na kusukuma maji katika kijiji cha Njia Panda (Mwanga); matanki ya kuhifadhi maji katika kijiji cha Kisangara, Kiverenge na katika miji ya Same na Mwanga; bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji katika miji ya Same na Mwanga; njia ya

umeme kwenda mitambo ya kusukuma maji; kituo cha kusukuma maji cha Kisangara; bomba kuu lenye urefu wa kilomita **20.3** la kupeleka maji kwenye tanki kuu eneo la Kiverenge pamoja na mabomba ya kusafirisha na kusambaza maji kutoka Tanki la Kiverenge kwenda miji ya Same na Mwanga. Hadi kufikia mwezi Machi 2014, usanifu wa mradi umekamilika na tangazo la kumpata mkandarasi wa ujenzi litatolewa tarehe 1 mwezi Mei, 2014.

b) Miradi yenyé kuleta matokeo ya haraka

Mpango huu wa kuleta matokeo ya haraka unahusisha upanuzi, ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya maji kutoka kwenye mabwawa, visima virefu na vyanzo vya maji juu ya ardhi. Utekelezaji wakeunalenga miradi inayoweza kuhudumia zaidi ya kijiji kimoja na miradi midogo.

Miradi inayohudumia zaidi ya kijiji kimoja

➤ *Mradi wa kuvipatia maji vijiji 100 vilivyopo kandokando ya bomba kuu la mradi wa Maji wa Kahama – Shinyanga*

Kati ya vijiji **100** vilivyopangwa, miradi katika vijiji **40** imeanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2013/2014 ambavyo ni; Mwamazengo (**Misungwi**) Sangu, Kikubiji, Mwalubungwe (**Kwimba**), Kadoto, Mwasekagi, Ipango, Buduhe, Amani, Mwandtu, Mwamadilanha, Mwabenda/Mwasekagi, Mapingili, Buzinza, Mwashiningu, Bukiliguru, Ngame, Ibubu, Mwashagi, Lyamidati (**Shinyanga Vijijini**), Mwakuzuka, Izuga, Matinje, Butegwa, Sunge, Kitwana, Nyashimbi, Busangi, Igombe, Mhama, Kabondo, Magobeko, Kakulu, Nyamigege, Ntundu, Gula, Nyambura, Buchambaga, Buluma na Bubungu (**Kahama/Msalala**). Usanifu katika vijiji **31** vya Halmashauri za Shinyanga Vijijini na Msalala umekamilika. Kati ya hivyo vijiji **31**, ujenzi wa miradi katika vijiji **vinne** vya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ambavyo ni Magobeko, Nyashimbi, Kakulu na Butegwa umeanza, zabuni katika vijiji **8** zimetangazwa na taratibu za kuwapata wakandarasi kwenye vijiji **19** zinaendelea. Usanifu unaendelea kwa vijiji **9** vilivyosalia.

➤ *Mradi wa Ntomoko katika Halmashauri ya Kondoa/Chemba;*

Kati ya vijiji **18** vinavyohudumiwa na mradi wa maji wa Ntomoko, ujenzi wa miundombinu katika vijiji **4** vya Jenjeluse, Goima, Mtakuja na Mlongia upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ambazo ni Jenjeluse (**88%**), Goima (**62%**), Mtakuja (**8%**) na Mlongia (**20%**). Wakandarasi kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya maji katika vijiji **10** vya Makirinya, Kirere cha Ng'ombe, Lusangi, Hamai, Songolo, Madaha, Churuku, Kinkima, Jinjo na Jangalo wamepatikana na utafiti kwa ajili ya kuchimba visima katika vijiji vya Igunga, Itolwa, Mapango na Chandama umekamilika. Kazi ya kuchimba visima imesimamishwa ili kupisha zoezi la kuhamisha mikataba ya utekelezaji wa miradi hiyo kutoka Wilaya ya Kondoa kwenda Halmashauri ya Wilaya ya Chemba.

➤ *Mradi ya maji wa Chiwambo*

Huduma ya maji katika mradi wa Chiwambo Wilaya ya Masasi imekuwa duni kutokana na kuchakaa kwa miundombinu. Katika kuboresha huduma ya maji kwenye maeneo hayo, Wizara inaendelea na juhudzi za kukarabati miundombinu ya maji ikihusisha ulazaji wa bomba kuu la kilometra **11** kutoka kwenye chanzo cha maji cha chemchemi ya Lulindi hadi kwenye matanki ya

Nagaga, ukarabati wa bomba lenye kipenyo cha **milimita 110** kutoka Nagaga hadi Chungutwa umbali wa **kilomita 16** na kukarabati bomba lenye kipenyo cha **milimita 110** kutoka Nagaga hadi Mitesa umbali wa **kilomita 10**. Vilevile, ukarabati na upanuzi wa mradi huo utahusija ulazaji wa mabomba yenye urefu wa **kilomita 50**, ujenzi wa matanki **10** ya kuhifadhi maji na vituo vya kuchotea maji **78**. Kukamilika kwa mradi huo utanufaisha wakazi wapato **32,570** waishio kwenye vijiji 50 katika kata saba ambazo ni Lulindi (vijiji 8), Mbuyuni (vijiji 7), Namalenga (vijiji 8), Chungutwa (vijiji 11), Sindano (vijiji 5), Mchauru (vijiji 9) na Ripumburu (vijiji 2).

Hadi kufikia mwezi Machi 2014, kazi ya kulaza bomba kuu imefikia **kilometra 8**. Vilevile, bomba la milimita **200** limelazwa umbali wa **kilomita 2.5** kutoka kwenye chanzo hadi matanki ya Nagaga ili kuongeza wingi wa maji katika eneo la mradi. Aidha, bomba la **milimita 110** limelazwa kutoka Nagaga kwenda Chingutwa lenye urefu wa kilomita **mbili** na kutoka Nagaga kwenda Mitesa limelazwa kwa umbali wa **kilomita moja na nusu**. Ujenzi wa matanki **mawili** kwenye eneo la mradi umeanza na ukarabati wa matanki **manne** unaendelea. Vituo **11** vya kuchotea maji vimejengwa. Mikataba kwa ajili ya kazi za ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji kwenye vijiji vyote vya mradi huu imesainiwa.

Miradi ya kuleta matokeo ya haraka

Utekelezaji wa miradi midogo 101 yenye kuleta matokeo ya haraka ambayo inatekelezwa kwenye vijiji 142 katika Halmashauri 65 inahusu ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya maji. Hadi mwezi Machi 2014, usanifu wa miradi umekamilika. Ujenzi na usimamizi utafanywa na **Halmashauri chini ya Sekretarieti za Mkoa na utekelezaji utaendelea katika mwaka 2014/15 (Kiambatisho Na. 4 (a))**.

Miradi ya Ujenzi wa Mabwawa

Serikali inaendelea na ujenzi wa mabwawa katika maeneo mbalimbali hususan maeneo kame kwa lengo la kuwapatia wananchi huduma ya maji kwa matumizi ya nyumbani na mifugo. Hatua zilizofikiwa katika utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

- **Bwawa la Ingondin (Longido, Arusha):** ukarabati wa bwawa hilo ulikamilika mwezi Januari, 2014 kwa kuimarisha utoro wa maji ambaa awali uliathiriwa na mafuriko.
- **Bwawa la Iguluba (Iringa Vijijini):** Hadi mwezi Machi 2014 ujenzi wa bwawa umefikia **asilimia 54**. Kazi ambazo hazijakamilika ni kujenga *crest weir*, miundombinu ya mawe kuzuia mmomonyoko wa udongo; kupanda nyasi upande wa nje wa tuta na kupanga mawe upande wa ndani wa tuta, ujenzi wa miundombinu ya kutolea maji kwenye bwawa na ujenzi wa vidakio vitatu (3) vya mchanga (*sand traps*). Kazi inatarajiwa kukamilika katika mwaka 2014/15
- **Bwawa la Kawa (Nkasi, Rukwa):** Ujenzi umefikia asilimia 95. Mkandarasi aliyejewa akiendelea na ujenzi wa bwawa hilo aliondoka eneo la mradi bila ruhusa ya Mwajiri kabla ya kumalizia kazi ndogo iliyobaki. Aidha, Wizara imemwajiri Mkandarasi mwingine kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji kutoka katika bwawa hilo kupeleka maji katika vijiji vya Nkundi, Kalundi na Fyengerezya. Ujenzi wa mradi huu umesimama kwa muda ili

kupisha usanifu wa kituo cha kutibu maji. Mradi huo ukikamilika jumla ya wananchi 13,500 watanufaika na huduma ya maji. Kazi inatarajiwa kukamilka katika mwaka 2014/15

- **Bwawa la Sasajila (Chamwino, Dodoma):** Ujenzi wa bwawa hili ulisimama kutokana na Mkandarasi aliyekuwepo awali kuondoka eneo la mradi bila ya ruhusa ya Mwajiri. Wizara imemwajiri Mkandarasi mwingine ambaye alianza kazi mwezi Novemba, 2013. Hadi mwezi Machi, 2014 ujenzi wa bwawa umefikia asilimia 62.5 na kazi zilizobaki zimepangwa kukamilishwa katika mwaka 2014/2015.
- **Bwawa la Mwanjoro (Meatu, Simiyu):** Hadi mwezi Machi 2014, ujenzi wa umefikia **asilimia 78**. Ujenzi huo kwa sasa umesimama baada ya Mkandarasi kuondoka eneo la kazi bila ruhusa ya Mwajiri wala Mtaalam Mshauri. Wizara itamwajiri Mkandarasi mwingine ili kukamilisha ujenzi wa bwawa hilo katika mwaka wa fedha 2014/2015.
- Wizara imeanza kutekeleza ujenzi wa mabwawa ya **Habiya** (Itilima, Simiyu), **Sekeididi** (Kishapu, Shinyanga) na **Matwiga** (Chunya, Mbeya) ambayo ujenzi wake ulisimama baada ya Wakandarasi husika kushindwa kazi na kuondoka kwenye maeneo ya miradi. Hatua zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na kusitisha mikataba ya Wakandarasi hao na Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (DDCA) ameteuliwa kukamilisha kazi hizo. Mikataba ya kukamilisha ujenzi wa mabwawa hayo imesainiwa tarehe 28.2.2014 na ujenzi wa mabwawa utaendelea baada ya msimu wa mvua.
- **Bwawa la Kidete (Kilosa, Morogoro):** Bwawa hili lilijengwa kabla ya Uhuru kwa lengo la kuthibiti mafuriko kwenye eneo la Reli ya Kati. Bwawa lilibomolewa na mafuriko ya mwaka 2003, hivyo kuilazimu Serikali kulijenga upya. Gharama ya ujenzi ilikadiriwa kuwa **shilingi bilioni 4.48**. Ujenzi umesimama kutokana na matatizo ya kimkataba ambayo yanashughulikiwa ili ujenzi uweze kukamilishwa katika mwaka 2014/2015.
- **Bwawa la Wegero (Butiama, Mara):** Ujenzi wa bwawa ulikamilika kwa mujibu wa mkataba wa awali. Hata hivyo kuongezeka kwa shughuli za kijamii hasa kilimo kulisababisha bwawa hilo kujaa tope katika muda mfupi na kushindwa kutumika ipasavyo. Wizara ilifanya upimaji mwezi Novemba 2013, na kuonekana kuwa bwawa linaweza kufanyiwa ukarabati ili kuongeza wingi wa maji kwa **mita za ujazo 32,000**. Kazi hiyo itafanyika katika mwaka wa fedha 2014/2015.

5.2.3 UBORESHAJI WA HUDUMA ZA MAJI MIJINI

Katika mwaka wa fedha 2013/14, Serikali ilitenga **shilingi 266,996,615,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji mijini. Kati ya fedha hizo, **shilingi 87,612,837,000** ni fedha za ndani na **shilingi 179,383,778,000** ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Machi 2014, **shilingi 56,500,467,208** zimetolewa. Kati ya fedha zilizotolewa, **shilingi 33,350,000,000** (sawa na **asilimia 38** ya bajeti) ni fedha za ndani kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na.6**; na **shilingi 23,150,467,208** (sawa na **asilimia 13** ya bajeti) ni fedha za nje. Sehemu kubwa ya fedha za nje za kutekeleza miradi ya

maji mijini inapitia kwenye miradi moja kwa moja (*earmarked projects*) na ufungaji wa hesabu za matumizi hufanyika mwishoni mwa mwaka wa fedha.

Katika kipindi hicho, Serikali imeendelea kutekeleza miradi katika miji ya mikoa, wilaya, miji midogo na Miradi ya Kitaifa kwa lengo la kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira mijini. Utekelezaji wa miradi hiyo uko katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mradi wa Majisafi Singida

Utekelezaji wa mradi huu wa uboreshaji huduma ya maji umegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni; Mtandao wa usambazaji maji utakaotumia chanzo cha maji kilichopo Mwankoko, Mtandao wa usambazaji maji utakaotumia chanzo cha maji kilichopo eneo la Kisaki/Irao na Mtandao wa mabomba madogo mpaka kwa wateja.

- **Upanuzi na ukarabati wa vyanzo na miundombinu ya Maji Mjini Singida**

Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi zinazozalisha Mafuta (*OPEC*) imekamilisha utekelezaji wa Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Maji katika Mji wa Singida. Mradi huo ulihusisha uchimbaji wa visima virefu **10**, kati ya hivyo **visima 7** vilikamilika na tayari vinatumika katika maeneo ya Mwankoko **viwili** na Irao **vitano** na **visima vitatu** vilikosa maji. Aidha, ujenzi wa matanki **mawili** katika maeneo ya *Airport* na ulazaji wa mabomba ya kusafirisha maji hadi kwenye matanki na kwenye mtandao wa maji kwa eneo la Mandewa umekamilika. Mradi huo umegharimu **shilingi bilioni 32.53**. Kukamilika kwa mradi huo kumeongeza uzalishaji wa maji kufikia lita **milioni 17.76** kwa siku kutoka lita **milioni 8.214** za awali.

- **Mtandao wa Mabomba Madogo**

Mradi huo unatekelezwa katika mji wa Singida ili kuwezesha wananchi kupata huduma katika maeneo yao baada ya mradi mkubwa kukamilika. Kazi ya ulazaji wa mabomba madogo ilianza Oktoba, 2012 na hadi sasa utekelezaji wake umefikia **asilimia 56.98**. Gharama ya mradi huo ni **Shilingi 1,299,983,006** na mabomba yenye umbali wa **mita 69,925** kati ya **mita 89,970** yamelazwa. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2014.

Mradi wa Majisafi Sumbawanga

Serikali iliajiri Mkandarasi kwa ajili ya Ukarabati na Upanuzi wa Miundombinu ya Maji katika Manispaa ya Sumbawanga (*immediate works*). Mkataba wa Ujenzi wa Miundombinu ya Maji ni **Shilingi bilioni 4.94**. Mkataba wa Uchimbaji wa Visima ni **shilingi milioni 373.9** na Mkataba wa Usimamizi wa Ujenzi ni **Euro 274,445.00** sawa na **Shilingi 431,800,000**. Mradi huu unatekelezwa chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP*).

Kazi zilizopangwa na kutekelezwa katika mradi huo ni pamoja na; ukarabati wa mabomba ya usambazaji maji kwa kubadilisha mabomba yaliyochakaa yenye urefu wa **kilomita 46**; uchimbaji

wa visima virefu **nane**; ulazaji wa bomba kuu kutoka kwenye visima mpaka kwenye matanki yenyе urefu wa **kilomita 9**; ununuzi wa pampu na kuzifunga na kuvuta umeme hadi kwenye chanzo.

Kazi zilizotekelawa hadi sasa ni uchimbaji wa visima virefu nane vyenye uwezo wa kuzalisha meta za ujazo **4,000** kwa siku; ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji kilomita **46** umekamilika; bomba kuu kilomita 6.2 limelazwa; ujenzi wa *collector tank* yenyе mita za ujazo **500** umekamilika. Kwa ujumla ujenzi umekamilika.

Kukamilika kwa mradi huo kumeongeza wastani wa muda wa upatikanaji maji utaongezeka kutoka **saa 15** mpaka kufikia **saa 18**, upotevu wa maji utapungua kufikia asilimia **37**, upatikanaji wa maji utaongezeka kutoka **asilimia 62** hadi kufikia **asilimia 68** ya wakazi wa Manispaa ya Sumbawanga.

Mradi wa Majisafi Mjini Mtwara

Serikali imeendelea na ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya maji katika Manispaa ya Mtwara. Mkataba wa ujenzi ni **Shilingi bilioni 6.92** na mkataba wa usimamizi wa ujenzi ni **Dola za Marekani 1,405,865.91**. Mradi huu unatekelezwa chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya maji (*WSDP*).

Kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mradi huo ni pamoja na: ukarabati wa mtandao wa maji; kufunga pampu **8** katika visima; ulazaji wa bomba kuu la maji lenye urefu wa **kilomita 3.95**; ulazaji wa mabomba ya usambazaji yenyе urefu wa **kilomita 27**, ununuzi wa genereta, na pampu mbili za kusukuma maji na dira **500** za maji.

Kwa ujumla ujenzi umekamilika na umeongeza saa za upatikanaji wa huduma ya maji kutoka saa 12 mpaka 18 kwa siku, wingi wa maji umeongezeka toka **mita za ujazo 5,000** hadi kufikia **10,236** kwa siku, na idadi ya watu wanaopata maji imeongezeka toka **asilimia 81** hadi **asilimia 92**. Aidha, Mhandisi Mshauri aneendelea upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi mpya wa kutoa maji mto Ruvuma kwenda mji wa Mtwara na vijiji vitakavyopitiwa na bomba kuu. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2014 na ujenzi utaanza mwaka wa fedha 2014/2015.

Mradi wa Majisafi na Uondoshaji Majitaka katika Chuo Kikuu cha Dodoma

Utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Chuo Kikuu cha Dodoma utagharimu kiasi cha **Shilingi bilioni 27.7** na unahusisha kazi zifuatazo: ujenzi wa matanki makubwa **matatu** ya kuhifadhi maji *UDOM* katika vilima vya Chimwaga mita za ujazo 4,500, Luangu mita za **ujazo 4,500** na *Informatics* mita za **ujazo 3,000**; kulaza **kilomita 12.2** za mabomba makubwa ya kusafirishia maji na **kilomita 9.6** za mabomba ya kusambazia maji kwenye maeneo ya chuo (vyuo vya Sayansi ya Jamii, *Informatics*, Elimu na Afya); ujenzi wa kituo cha kusukumia maji (*pumping station*) eneo la Makulu ikiwa ni pamoja na uwekaji wa umeme (*electrical installation*). ujenzi wa **kilomita 18.5** za mtandao wa mabomba makubwa wa kusafirishia majitaka (*main trunk sewer*), na **kilomita 8** za mabomba madogomadogo ya kukusanya majitaka (*lateral sewers*); ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka katika eneo la wastani wa **hekta 108**.

Hadi kufikia mwezi Machi 2014, utekelezaji umefikia hatua zifuatazo:-

- Ujenzi wa matanki mawili yenye mita za ujazo **4,500 na 3,000** umefikia **asilimia 90** na tanki moja lenye mita za ujazo **4,500** lipo katika hatua za awali za ujenzi.

Ulazaji wa Mabomba

- Mabomba ya Usambazaji umbali **kilomita 7** kati ya **kilomita 9.6** zinazohitajika yamelazwa.
- Bomba Kuu lenye umbali kilomita 5 kati ya **kilomita 12.2** zinazohitajika zimelazwa.

Mabwawa ya Majitaka (Ponds)

- Mkandarasi anaendelea na ujenzi wa *concrete slabs* kwenye kingo za mabwawa. Hadi kufikia mwezi Machi 2014, ujenzi wa mabwawa umefikia **asilimia 35**.
- Kazi ya uchimbaji wa *storm drain* ambayo itajengwa kwa mawe (*stoney pitching*) ili kuzuia maji ya mvua yasiingie kwenye mabwawa inaendelea.

Hadi mwezi Machi 2014, utekelezaji wa mradi huo kwa ujumla umefikia **asilimia 54**. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2014. Mradi huo uliwekewa jiwe la msingi tarehe 22/03/2014 na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mizengo Peter Pinda siku ya kilele ya Maadhimisho ya Wiki ya Maji.

Mradi wa Kuboresha Huduma ya Majisafi MJINI Dodoma

Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Korea Kusini inatekeleza mradi wa uboreshaji wa huduma ya majisafi katika mji wa Dodoma kwa gharama ya **Dola za Kimarekani milioni 49.62**. Utekelezaji wa mradi huo utahusisha kazi zifuatazo: Ukarabati wa visima 21 na uchimbaji wa visima vipyta vitatu katika eneo la Mzakwe; ujenzi wa mtandao wenye urefu wa kilomita **6.5**; ujenzi wa barabara za visimani zenye urefu wa **kilomita 5**; ulazaji wa bomba kuu jipya lenye kipenyo cha **milimita 600** na lenye urefu wa **kilomita 31.2** kutoka Mzakwe hadi mjini; ujenzi wa matanki mawili yenye jumla ya mita za ujazo **12,500** na ukarabati wa mitambo ya kusukuma maji; ujenzi wa *booster station* mpya eneo la Mailimbili; ununuzi wa mitambo/vifaa vya kisasa vya kutibu maji pamoja na kujenga maabara ya kisasa ya kupima ubora wa majisafi na majitaka.

Utekelezaji wa mradi ulianza mwezi Desemba 2012 na unategemewa kukamilika mwezi Januari 2015. Hadi mwezi Machi 2014, utekelezaji wa kazi umefikia **asilimia 35** ambapo **visima 15** kati ya **visima 21** vilivyopangwa kukarabatiwa vimekamilika na **visima vipyta 2** kati ya **visima 3** vilivyopangwa kuchimbwa vimekamilika. Kwa ujumla kazi zote zikikamilika kiwango cha uzalishaji kitaongezeka kutoka **lita za ujazo milioni 32** hadi **milioni 61.5** na kuongeza muda wa upatikanaji wa huduma ya maji kutoka masaa **12** hadi **20** kwa siku.

Mradi wa Majisafi Morogoro

Serikali kwa kushirikiana na **MCC** inatekeleza mradi wa ukarabati wa miundombinu ya maji katika Manispaa ya Morogoro kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 12** Hadi Machi 2014, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 92** ambapo kazi zilizofanyika ni ukarabati wa matanki mawili na ununuzi wa pampu tatu, ulazaji wa bomba kuu la maji lenye urefu wa kilometra 1.8,

ujenzi wa chujio jipya na kitekeo cha maji Mambogo, ujenzi wa matanki mawili yenyе jumla ya mita za ujazo 550 na ukarabati wa chujio la maji katika eneo la Mafiga. Ujenzi ukikamilika unatarajiwa kuongeza uzalishaji wa maji kutoka **mita za ujazo 2,400** kwa siku mpaka **mita za ujazo 3,300** kwa siku, na hivyo kuongeza kiwango cha uzalishaji wa maji kutoka **asilimia 74** hadi kufikia **asilimia 84**. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2014.

Mradi wa Majisafi Babati

Katika mwaka wa fedha 2013/2014 Serikali iliendelea na ujenzi wa ofisi kwa ajili ya Mamlaka ya Maji mjini Babati. Mkataba wa ujenzi wa ofisi ni **shilingi bilioni 2.52** na Mkataba wa usimamizi wa ujenzi ni **Dola 449,300.00**. Mradi huo unatekelezwa chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP*). Hadi kufikia mwezi Machi 2014 utekelezaji ulifiki **asilimia 80**. Ujenzi unatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Juni 2014.

Mradi wa Maji wa Orkesumet

Katika kutekeleza mradi wa kukidhi mahitaji ya muda mrefu ya wakazi wa Orkesumet, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Nchi za Kiarabu (*BADEA*) na *OFID* inatarajia kujenga mradi wa majisafi utakaohudumia mji wa Orkesumet. Mradi huu utagharimu **Dola za Marekani Milioni 18.4** ambapo *BADEA* watatoa **Dola za Marekani Milioni 8**, *OFID* watatoa **Dola za Marekani Milioni 8** na Mchango wa Serikali kwa mradi huo ni **dola za Marekani Milioni 2.4**. Hadi kufikia mwezi Machi 2014 Mtaalam Mshauri anaendelea na kufanya mapitio (*review*) ya usanifu uliofanywa hapo awali, na kutayarisha vitabu vya zabuni kwa ajili ya kumtafuta Mkandarasi wa ujenzi. Ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2014/2015.

Mradi wa Maji wa Mugango -Kiabakari

Mradi huo unaotekelizwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*) na Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*Saudi Fund for Development - SFD*) unakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 30.69**. Kazi zitakazotekelezwa ni ujenzi wa chanzo, ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kusukuma maji, kujenga matanki matatu, kulaza mabomba kutoka Mugango, Kiabakari hadi Butiama kwa urefu wa **kilomita 32**, kukarabati mitambo ya kusukuma maji ya Kiabakari na kulaza mabomba ya mtandao wa usambazaji maji kutoka Butiama hadi Bisarye. Kukamilika kwa mradi huo kutanufaisha wananchi wapatao **80,000** waliopo katika eneo la mradi wa Kitaifa wa Mugango-Kiabakari pamoja na vijiji vilivyopo umbali wa **kilomita 12** kando ya bomba kuu.

Taratibu za kuajiri Mtaalam Mshauri wa kufanya mapitio ya usanifu na usimamizi wa mradi wa miundombinu ya maji ya mradi huo zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika mwezi Mei 2014.

Mradi wa Majisafi Bukoba

Mradi huo unahusu uboreshaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwa gharama ya **shilingi bilioni 27.535** na kazi zifuatazo zitatekelezwa: ujenzi wa chanzo cha maji; ujenzi wa chujio

la kusafisha maji; ulazaji wa bomba kuu la kusafirisha maji lenye urefu wa **kilomita 3.5** na mabomba ya kusambaza maji yenyе urefu wa kilomita **45**; Ujenzi wa matanki **2** ya kuhifadhi maji yenyе mita za ujazo **2,500** na mita za ujazo **2,200**; ujenzi wa eneo la kumwaga majitaka (*sluge digester*) pamoja na ununuzi wa magari **mawili** ya kuondosha majitaka.

Hadi mwezi Machi 2014, utekelezaji umefikia **asilimia 40** na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2014. Mradi huo ukikamilika, utaongeza uzalishaji wa maji kutoka **mita za ujazo 8,815** za sasa hadi kufikia **mita za ujazo 18,000** kwa siku ambayo inakidhi mahitaji ya maji kwa siku kwa Manispaa ya Bukoba hadi mwaka 2017.

Mradi wa Majisafi Musoma

Mradi huo unahu su uboreshaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwa gharama ya **shilingi bilioni 40.62** na kazi zifuatazo zitatekelezwa:

Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma unahu shughuli zifuatazo: ujenzi wa chanzo cha maji; ujenzi wa chujio la kusafisha maji; bomba kuu la kusafirisha maji na mabomba ya kusambaza maji; ujenzi wa matanki ya kuhifadhi maji; ujenzi wa eneo la kumwaga majitaka (*sluge digester*) pamoja na ununuzi wa magari **mawili** ya kuondosha majitaka.

Hadi mwezi Machi 2014, utekelezaji umefikia **asilimia 50** na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2014. Mradi huo ukikamilika, utaongeza uzalishaji wa maji kutoka **mita za ujazo 10,142** kwa siku ya sasa hadi kufikia **mita za ujazo 36,000** kwa siku ambayo inakidhi mahitaji ya maji kwa siku kwa Manispaa ya Musoma hadi mwaka 2025.

Mradi wa Majisafi Tabora

Ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya maji katika Manispaa ya Tabora unaendelea. Mkataba wa ujenzi ni **Dola milioni 4.841**. Mradi huu unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Uswisi (*SECO*).

Kazi zilizopangwa na kutekelezwa ni pamoja na: ukarabati wa mtandao wa maji **kilomita 27** maeneo ya mjini; ulazaji wa bomba kuu la maji lenye kipenyo cha mm 500 na lenye urefu wa **kilomita 2.7** kutoka Igombe; ununuzi wa pampu mbili za kusukuma maji pamoja na transfoma mbili; ujenzi wa matanki yenyе jumla ya **mita za ujazo 5,000**; ununuzi wa dira za maji **5,000** na uboreshaji wa chanzo pamoja na kujenga vituo vya *post chlorination* karibu na mjini.

Hadi sasa utekelezaji wa mradi huu umefikia **asilimia 96**. Ujenzi ukikamilika utaongeza uzalishaji wa maji kutoka mita za ujazo **11,000** kwa siku kwa sasa hadi kufikia mita za ujazo **15,000** kwa siku, upotevu wa maji utapungua kutoka **asilimia 42** hadi kufikia asilimia **23**, ubora wa maji utaongezeka na wateja watakaofungiwa dira za maji watafikia asilimia **100** na hivyo kupunguza malalamiko ya wateja. Kwa ujumla kiwango cha utoaji wa huduma kitaongezeka kutoka **asilimia 63** hadi **asilimia 86**. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2014.

Ukarabati wa Bwawa la Igombe

Sambamba na mradi huo, kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP*), Serikali inatekeleza mradi wa kukarabati na kupanua machujio ya maji katika kituo cha Igombe, ili kuweza kuzalisha maji mita za **ujazo 30,000 kwa siku**, ukilinganisha na mahitaji ya sasa ya **mita za ujazo 24,970 kwa siku**.

Katika awamu ya kwanza ya mradi huo, kazi zilizopangwa kufanyika katika kituo cha Igombe ni pamoja na: kufunga pampu mbili katika kituo cha kuchota maji ghafi (*Low lift station*); ujenzi wa bomba lenye kipenyo cha **milimita 400** na urefu wa **Mita 240**; kukarabati chujio la maji lililopo hivi sasa; ujenzi wa chujio jipya; kufunika matanki ya maji yanayojengwa katika mradi wa *SECO*; kufunga pampu moja kituo cha kusukuma maji kuelekea mjini Tabora (*High lift station*) na kufunga *transformer* moja kubwa.

Mkandarasi amekamilisha usanifu wa awali na unafanyiwa mapitio, hivi sasa mkandarasi anaendelea na ujenzi wa kambi na ujenzi wa mradi huo unategemea kukamilika baada ya miezi 18. Mkataba wa ujenzi ni **Dola za Marekani 4,737,837.76**, (sawa na **Shillingi Billioni 7.5**)

Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga, Kigoma na Lindi chini ya Programu ya *Millenium Development Goal Initiative*

Miradi ya majisafi na usafi wa mazingira katika manispaa za Kigoma, Lindi na Sumbawanga inatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na Umoja wa Ulaya wanachangia **Euro Milioni 51.51** kupitia *Millenium Development Goal Initiative*; pamoja na Serikali ya Ujerumanu kupitia KfW (Benki ya Maendeleo ya Ujerumanu) ambao wanatoa **Euro milioni 11.28**. Utekelezaji wa miradi hii ilianza mwezi Februari 2013 na umepangwa kukamilika mwezi Machi 2015.

a) Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga

Utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira mjini Sumbawanga unahusisha kazi zifuatazo: uchimbaji wa visima **virefu 12**; ujenzi wa *sump* yenye mita za **ujazo 1,000**; upanuzi wa chujio la maji; ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji na bomba kuu la maji; ujenzi wa matanki **manne** ya maji yenye mita za **ujazo 1,000** kila moja; ujenzi wa **vituo 327** vya kuchotea maji na ujenzi wa **mabwawa mawili** ya kutibu majitaka na ununuzi wa gari la uondoshaji wa majitaka.

Kazi zilizofanyika ni ujenzi wa matanki **3** kati ya **6**, uchimbaji wa msingi kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa ya majitaka pia umekamilika na *stone pitching* imefanyika katika mabwawa mawili. Hadi sasa **visima 20** vimechimbwa kati ya hivyo ni **visima 6** ndivyo vimepata maji na vinatoa **mita za ujazo 244** kwa saa. Kwa ujumla wastani wa utekelezaji ni **asilimia 32**.

b) Mradi wa Majisafi na usafi wa mazingira mjini Kigoma

Utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira mjini Kigoma unahusisha kazi zifuatazo: ujenzi kitekeo cha maji; ujenzi wa tanki lenye mita za **ujazo 2,000** karibu

na kitekeo pamoja na *chlorination facilities*; ujenzi wa *pumping station* yenyepampu 9; ujenzi wa matanki **5** ya maji yenyewe uwezo wa mita za **ujazo 2,000** na moja la mita za **ujazo 500**; ujenzi wa **vituo 222** vya kuchotea maji; ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji yenyewerefu wa **kilomita 122.8** na bomba kuu la lenye urefu wa **kilomita 16.9** na ujenzi wa mabwawa **2** ya kutibumajitaka na ununuzi wa gari la uondoshaji wa majitaka.

Kazi zilizofanyika mpaka sasa ni kuandaa michoro; ununuzi wa vifaa ya ujenzi; uchunguzi wa sampuli za udongo ambapo Mkandarasi amekamilisha *geophysical surveys* kwa ajili ya ujenzi wa matanki sita na sehemu ya ujenzi wa intake; ufungaji wa nondo katika tanki la Mnarani unaendelea; uchimbaji wa msingi na *blinding* katika tanki la Mbole, Gungu na Shule ya Sekondari umekamilika. Hadi sasa wastani wa utekelezaji ni **asilimia 12**.

c) Mradi wa Majisafi na usafi wa mazingira MJINI Lindi

Mradi wa Majisafi na usafi wa mazingira mjini Lindi unahusisha kuongeza vyanzo vya maji, kujenga miundombinu na mabwawa ya kutibumajitaka ambapo kazi zifuatazo zimepangwa kutekelezwani: uchimbaji wa visima **virefu 10**; ujenzi wa chujio la maji la mita za ujazo **7,500** kwasiku; ujenzi wa matanki **mawili** ya maji yenyemita za **ujazo 3,000 na 2000**; ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji na bomba kuu la maji; ujenzi wa **vituo 85** vya kuchota maji na ujenzi wa **mabwawa 2** ya kutibumajitaka na ununuzi wa gari la uondoshaji wa majitaka.

Kazi zilizofanyika hadi mwezi Machi 2014 ni uchimbaji wa visima **9** kati ya **10** vilivyopangwa; kuendelea na ujenzi wa chujio, tanki la Mtanda na Central, ujenzi wa mabwawa ya kusafisha majitaka (*wetlands*). Kwa ujumla utekelezaji wa mradi unakadirisha kufikia **asilimia 54**.

Miradi hii ikikamilka itaongeza kiwango cha upatikanaji wa maji kwa wakazi wapatao **500,000** wa miji ya **Sumbawanga, Lindi na Kigoma** na huduma ya usafi wa mazingira itaboreshwa kwa wakazi **254,000**. Mradi una uwezo wa kukidhi huduma ya maji kwa wakazi wa Manispaa hizo hadi kufikia mwaka **2020**.

d) Mradi wa kuboresha huduma ya maji na usafi wa mazingira Babati na Mtwara

Serikali kwa kushirikiana na *KfW* inatekeleza Mradi wa kuboresha huduma ya Maji na usafi wa mazingira katika miji ya Babati na Mtwara kwa gharama ya **Euro milioni 8.7**. Wizara inaendelea na taratibu za kutafuta mhandisi mshauri wa kusimamia utekelezaji wa mradi huo ambae ataainisha kazi zitakazofanyika katika mradi huo kulingana na fedha zilizopo.

e) Mradi wa Majisafi Masasi - Nachingwea

Mradi wa maji wa Masasi/Nachingwea umekamilika mwezi Julai, 2013 na unahudumia miji ya Masasi na Nachingwea pamoja na vijiji vya Likwachu na Chinongwe vilivyopo Wilaya ya Ruangwa na Chiumbati Shuleni, Chiumbati Miembeni vilivyopo wilaya ya Nachingwea. Kazi ya uunganishaji wateja na ufungaji wa dira za maji inaendelea, ambapo hadi mwezi Machi 2014 jumla ya **wateja 2,972** wameunganishwa. Vilevile, wateja wasiounaganishwa kwenye mtandao wanapata huduma kutoka kwenye **vituo 68** vilivyojengwa maeneo mbalimbali ya miji ya Masasi na Nachingwea. Mradi huu utahudumia wananchi **77,207** katika Mji wa Nachingwea na wananchi **102,699** Masasi

f) Mradi wa Majisafi Wami (Chalinze)

Mradi wa maji wa Chalinze awamu ya pili utatoa huduma ya Maji katika **vijiji 47** vyenye **watu 197,684**. Utekelezaji wa awamu hii unakadirwa kutumia jumla ya Shilingi za Tanzania **bilion 53.7**. Kazi zinazotekelawa katika awamu ya pili ni pamoja na kujenga chujio la maji lenye uwezo wa **mita za ujazo 200** kwa saa, vituo viwili nya kusukuma maji (Mbweve na Ubenazomozi), kulaza mtandao wa bomba kuu kwa urefu wa kilomita **335**, kulaza bomba la usambazaji kwa urefu wa kilomita **127**, kujenga matanki **42** ya kuhifadhia maji na vituo **371** nya kuchotea maji. Ili kuharakisha utekelezaji, mradi umegawanywa katika sehemu (*lots*) tisa (9) ambapo Serikali imeajiri Wakandarasi 7. Hadi mwezi Machi 2014 utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 93**.

Mtaalam Mshauri wa kusimamia utekelezaji wa mradi wa Chalinze awamu ya tatu anaendelea na kazi ya kufanya mapitio ya usanifu. Kazi hiyo ilianza mwezi Agosti, 2013 na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2014. Mradi huo utagharimu **Dola za Marekani milioni 49** amabapo ujenzi wa mradi huo utaanza Julai 2014 na kukamilika mwaka 2016. Kazi zitakazotekelawa ni ukarabati wa chanzo, kujenga matanki ya kuhifadhia maji katika vijiji 20, kupanua mitandao ya bomba kuu na bomba la usambazaji, kujenga tanki kubwa la kuhifadhi maji katika Mlima Mazizi na kujenga vituo nya kuchotea maji katika maeneo ambayo hayakufikiwa na ujenzi wa awamu za I na II.

g) Mradi wa Majisafi mjini Songea

Mradi huo unahusisha ukarabati wa chanzo cha maji cha mto Ruhila. Kazi itakayofanyika ni kujenga banio ili kukabiliana na upungufu wa maji wakati wa kiangazi. Gharama ya kukamilisha mradi huo ni **shilingi bilioni 2.6**. Hadi kufikia mwezi Machi 2014, kiasi cha **shilingi milioni 100** zilitumwa na ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Mei 2014.

h) Mradi wa Maji katika Mji wa Kisarawe

Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi wa maji katika mji wa Kisarawe kwa lengo la kuongeza vyanzo nya maji, pamoja na vituo nya kuchotea maji. Hadi mwezi Machi 2014 kazi zilizokamilika ni uchimbaji wa visima **vitano** maeneo ya Kwala, Mtunani, Chole-Samvula, Yombo-Lukinga I na Yombo-Lukinga II. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwaka 2014/2015.

i) Ikwiriri

Utekelezaji wa mradi wa majisafi katika mji mdogo wa Ikwiriri umekamilika na kukabidhiwa kwa wananchi mwezi Disemba 2013. Mradi huo unakadirwa kuhudumia wananchi wapatao **44,383** hadi mwaka 2025.

j) Kilosa, Turiani, Mvomero na Gairo

Serikali imeendelea na ujenzi wa miradi ya maji katika miji midogo ya Kilosa, Turiani, Mvomero na Gairo. Hadi kufikia mwezi Machi 2014, ujenzi wa miradi ya maji katika miji hiyo upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo; Kilosa (**80%**), Turiani (**77%**), Mvomero (**81%**) na Gairo (**87%**). Aidha utekelezaji umekuwa ukienda kwa kasi ndogo kutokana na wakandarasi kusimamisha kazi kwa madai ya malipo ya fidia kutokana na kucheleweshewa malipo. Kwa sasa

wakandarasi hao wanaendelea na utekelezaji ambapo kazi hizo zinatarajiwa kukamilika kabla ya Desemba 2014.

k) Mradi wa Majisafi Kibaigwa

Utekelezaji wa mradi wa majisafi katika mji wa Kibaigwa umekamilika kwa gharama ya **Shilingi bilioni 2.27** ambapo kazi zifuatazo zilifanyika ni pamoja na: uchimbaji wa visima **virefu 2**; ujenzi wa mabomba ya kusambaza maji **kilometa 26**; ujenzi wa nyumba ya mtambo wa kusukuma maji; ujenzi wa tanki la maji mita za **ujazo 1,000**; ujenzi wa karakana na nyumba ya mlinzi na ujenzi wa nyumba ya kutibu maji.

Mradi huo ulizinduliwa na Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda wakati wa Maadhimisho ya wiki ya Maji tarehe 17 Machi, 2014. Kukamilika kwa mradi huo kumeweza na **asilimia 90** ya wananchi wa mji wa Kibaigwa kupata majisafi na salama ukilinganisha na **asilimia 48** kabla ya mradi.

l) Mradi wa Majisafi Bunda

Awamu ya kwanza ya mradi huu inakadiriwa kugharimu **Shilingi bilioni 6.45** ambapo kazi zifuatazo zimepangwa kutekelezwa ni pamoja na: ulazaji wa mabomba kutoka kwenye chanzo cha Nyabehu hadi Bunda Mlimani yenye urefu wa **kilomita 25.4**; ukarabati wa chanzo cha maji eneo la Guta; ukarabati wa matanki matatu yenye ukubwa wa mita za **ujazo 225** kila moja; kununua magari mawili na kujenga Ofisi ya Mhandisi Mshauri.

Hadi mwezi Machi 2014, kazi zilizokamilika ni pamoja na ukarabati wa **matanki 2** kati ya **matanki 3** yenye mita za **ujazo 225** kila moja; Ofisi ya Mhandisi Mshauri na ununuzi wa magari mawili na ulazaji wa bomba **kilomita 9.3** kati ya **kilomita 25.4**. Kwa ujumla, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 35**. Mradi huu utakapokamilika utaongeza kiwango cha upatikanaji wa maji kutoka **asilimia 26.3** ya sasa hadi kufikia **asilimia 99** ya wakazi wote wa Bunda na vijiji ambavyo viro kwenye chanzo na maeneo linapopita bomba kuu.

m) Miradi Mipyä katika eneo la Ziwa Victoria

Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya “*European Investment Bank*” (EIB) pamoja na Shirika la Maendeleo la Ufaransa “*French Development Agency*” (AFD) inatekeleza mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira katika Jiji la Mwanza na miji ya Musoma, Bukoba, Magu, Misungwi na Lamadi. Miradi hii inakadiriwa kugharimu jumla ya **Euro milioni 104.5** ambapo Serikali itatoa **Euro Milioni 14.5**, EIB na AFD kwa pamoja wameahidi kutoa jumla ya **Euro Milioni 90**. Hadi kufikia mwezi Machi 2014, mikataba ya kifedha tayari imesainiwa na taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri wa kufanya mapitio ya usanifu wa miradi hiyo zinaendelea.

Kukamilika kwa miradi hiyo kutaongeza upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 35** hadi **asilimia 90** kwa mji wa Magu; kutoka **asilimia 5** hadi **asilimia 90** kwa mji wa Lamadi na kutoka **asilimia 45** hadi **asilimia 90** kwa mji wa Misungwi.

Aidha, katika Jiji la Mwanza mradi unategemea kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji sambamba na kuboresha usafi wa mazingira katika maeneo ya miinuko ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vyoo vya shule za msingi na maeneo ya stendi.

n) Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira katika miji ya Sengerema, Geita na Nansio chini ya program ya *Lake Victoria Water and Sanitation Initiative*

Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira katika miji ya Sengerema, Geita na Nansio unatekelezwa chini ya programu ya *LV-WATSAN* awamu ya pili na kufadhiliwa na *AfDB* sambamba na *UN-HABITAT*. Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni za vipindi vya muda mfupi na muda mrefu ambazo ni kujenga na kuboresha miundombinu ya majisafi, mifumo ya utoaji wa huduma ya usafi wa mazingira, mitaro ya maji ya mvua na kuzijengea uwezo mamlaka za maji za miji ya Sengerema, Geita na Nansio.

Utekelezaji wa mpango wa muda mfupi

Hatua zilizofikiwa katika utekelezaji ni pamoja na ununuzi wa magari matano (5): Sengerema (1), Nansio (1), Geita (2), *MWAUWASA* (2); Pikipiki (8): Sengerema(3), Geita(3), Nansio (2); Matrekta (9): Sengerema (3), Nansio (3), Geita (3) na magari makubwa ya kuzoa taka **matano**: Sengerema(2), Geita (2), Nansio (1) na magari madogo ya majitaka **matatu**: Sengerema (1), Nansio (1), Geita (1). Aidha, mamlaka hizo zimepewa vifaa vya kukusanya taka ngumu Sengerema (37), Nansio (27) na Geita (40). Mradi huo utakamilika mwezi Desemba 2014.

Utekelezaji wa mpango wa muda mrefu

Mtaalam mshauri wa kusimamia shughuli za ujenzi wa mradi huo amewasilisha taarifa ya usanifu wa mradi. Mpango wa muda mrefu utakamilika Disemba 2015

o) Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda mji wa Geita

Serikali kwa kupitia Halmashauri ya mji wa Geita na kwa kushirikiana na Mgodi wa Madini wa Geita (*Geita Gold Mining Limited – GGML*) inatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji mjini Geita. Kazi ambazo zimekamilika ni ujenzi wa chanzo, chujio la maji, kulaza bomba kuu, tanki moja lenye mita za ujazo **1,300** na bomba lenye urefu wa **mita 540** kutoka kwenye tanki na kuunganisha kwenye mtandao wa zamani kwa gharama za **Dola za Marekani Milioni 5.4**. Kazi ya ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji itatekelezwa kwa gharama ya kiasi cha **Dola za Marekani Milioni 1.4** kati ya hizo mchango wa Serikali ni **Dola za Marekani 400,000** na GGML ni **Dola za Marekani Milioni 1**. Kukamilika kwa Mradi huo kunatarajiwa kuzalisha lita **milioni 4.8** za maji kwa siku, hivyo kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 3.5** hadi **asilimia 40**.

p) Mradi wa Kuboresha Huduma ya Majisafi Mpanda

Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali ilitenga **shilingi 2,600,000,000** na tayari kiasi cha **shilingi 1,500,000,000** kimetolewa kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika mji wa Mpanda ambao ni makao makuu ya mkoa mpya wa Katavi. Utekelezaji wa mradi huo umeanza mwezi Desemba 2013 na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai 2014. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: ujenzi wa bomba kuu toka chanzo cha Ikolongo hadi Kazima kwa urefu wa **Kilomita 13.6**; upanuzi na ukarabati wa mtandao wa maji umbali wa **kilometra 48** mjini Mpanda; ujenzi wa tanki la maji la **mita za ujazo 1,000** na kufunga *solar panels nne*; ununuzi wa dira za maji na pampu ya kusukuma maji pamoja na vibanda vya walinzi.

Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 mtaro wa urefu wa **kilomita 12.4** kati **13.6** umechimbwa ambapo bomba lenye urefu wa **kilomita 1.3** limelazwa. Ujenzi wa nyumba **mbili** na tanki la ujazo wa **mita za ujazo 1,000** umeanza. Mradi huo unatajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2014, na utaongeza kiasi cha **lita 5,000** kwa siku. Idadi ya watu wapatao **50,000** watanufaika na huduma hiyo ambapo upatikanaji wa huduma ya maji utaongezeaka kutoka **asilimia 38.8** ya sasa hadi kufikia **asilimia 72** mradi utakapokamilika. Wastani wa utekelezaji wa mradi huo umefikia **asilimia 45**.

q) Mradi wa Uboreshaji wa Huduma ya Majisafi Bariadi

Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali ilitenga **shilingi 3,213,000,000** na tayari kiasi cha **shilingi 1,200,000,000** kimetolewa kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika mji wa Bariadi ambao ni makao makuu ya mkoa mpya wa Simiyu. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kuchimba visima sita na kufunga pampu; kujenga tanki la maji; kupanua mtandao wa maji; kukarabati tanki la Somanda; kuunganisha umeme kwa ajili ya visima vya Somanda, Sanungu, Isanzu na Kidinda; na ujenzi wa mtandao wa kusambaza maji Kidinda kwa kuunganisha na ujenzi wa *viosk* vinne.

Hadi kufikia mwezi Machi 2014 uchimbaji wa mtaro wenye urefu wa **kilometa 6.8** kati ya **kilomita 7.5** umechimbwa ambapo bomba la urefu wa **kilomita 2.12** limelazwa. Mradi huo utapokamilika, kiasi cha maji kitaongezeka kutoka **lita 861,000** hadi kufikia **1,560,000** kwa siku. Huduma ya upatikanaji maji itaongezeka kutoka **asilimia 17** za sasa hadi **asilimia 30**. Wastani wa utekelezaji wa mradi huo umefikia **asilimia 20**.

r) Mradi wa Uboreshaji wa Huduma ya Majisafi Njombe

Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali ilitenga **shilingi 3,500,000,000** na tayari kiasi cha **shilingi 1,200,000,000** kimetolewa kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika mji wa Njombe ambao ni makao makuu ya mkoa mpya wa Njombe. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni: ujenzi wa kitekeo cha maji cha Nyenga; ulazaji wa bomba kuu la maji kutoka chanzo cha Nyenga kwa umbali wa **kilomita 14.26**; ujenzi wa matanki **matatu** ya kuhifadhi maji yenye ukubwa wa mita za ujazo **135** kila moja pamoja na ununuzi wa mabomba na viungio vyake pamoja na mita kubwa za maji. Hadi mwezi Machi 2014, utekelezaji wa mradi huo umefikia **asilimia 20**.

s) Mradi wa Uboreshaji wa Huduma ya Majisafi Muheza

Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali imetuma **shilingi milioni 350** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma ya maji katika mji wa Muheza. Kazi zilizopangwa ni kuboresha miundombinu ya maji ya visima virefu **vitatu (3)** vilivyopo Soko la Michungwani, NHC – tank na Kwasemwaiko. Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni ununuzi na ufungaji wa pampu na viunganishi vyake, ujenzi wa Chemba 2 na vituo 2 vya kuchotea maji, uchimbaji mtaro, ulazaji wa bomba na ununuzi wa vifaa vya ujenzi na umeme. Ujenzi huo ukikamilika kwenye Kisima cha NHC-tank kitakuwa na uwezo wa kuzalisha maji **lita 2,000** kwa saa, kisima cha Kwasemwaiko kikikamilika kitakuwa na uwezo wa kuzalisha maji **lita 2,500** kwa saa, hii ni ongezeko la **lita 99,000** kwa siku.

t) Mradi wa Uboreshaji wa Huduma ya Majisafi Karatu (Mradi wa dharura)

Utekelezaji wa mradi wa maji wa dharura mjini Karatu umefikia **asilimia 80** na umeanza kutoa huduma ya maji kwa wakazi wa mji wa Karatu ambapo tayari mradi umezinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 22 Aprili 2014. Mradi huo ulikadiriwa kugharimu **Shilingi milioni 930**, ambapo hadi sasa **Shilingi milioni 620** zimetumika. Hadi mwezi Machi 2014, kazi zilizokamilika ni: ujenzi wa tanki **moja** la **mita za ujazo 225**, ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa **kilomita 2.9** linalopeleka maji kwenye tanki, ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa **kilomita 11.3**, ujenzi wa njia kuu ya umeme yenye urefu wa **kilomita 1.2** na kufunga transfoma, ufungaji wa pampu na ujenzi wa **vituo 12** vya kuchotea maji. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita 840,000** hadi **lita 3,000,000** kwa siku na kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 20** ya sasa hadi kufikia **asilimia 71**.

u) Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Victoria kwenda Mji wa Ngudu

Mradi huu unahu ujenzi wa bomba kuu linalounganishwa kwenye bomba kuu la mradi wa Kahama/Shinyanga (KASHWASA) kutoka Ziwa Victoria kuititia Tanki la Mhalo lililopo Tarafa ya Mwamashimba ambapo kazi zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:- Kufanya usanifu wa miundombinu, kujenga mtandao wa mabomba na miundombinu mingine. Mradi huo umekadiriwa kugharimu **Shilingi bilioni 3.48**. Hadi kufikia mwezi Machi 2014, utekelezaji ni kama ifuatavyo:- Usanifu wa miundombinu umekamilika, uchimbaji wa mtaro wa kulaza bomba kutoka kijiji cha Runele hadi Ngudu umefikia umbali wa **kilometra 15** kati ya **21**, ulazaji mabomba umefikia umbali wa **kilometra 13** kati ya **kilometra 15** na ukarabati wa tanki lililopo Ngudu mjini umekamilika. Kwa ujumla, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 60** na ukikamilika unatarajiwa kuhudumia wakazi wa mji wa Ngudu wapatao **27,630** na **21,329** katika vijiji **10** linakopita bomba hilo.

v) Miradi ya kuboresha huduma ya maji katika Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa

Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali imepeleka jumla ya **shilingi bilioni 6.35** kwenye miji midogo, miji ya wilaya pamoja na miradi ya kitaifa kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya maji ili kuboresha huduma ya maji katika maeneo hayo.

w) **Uboreshaji wa huduma za maji katika Jiji la Dar es salaam**

Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA) imeendelea kusimamia utoaji wa huduma katika jiji la Dar es Salaam, Kibaha na Bagamoyo. Eneo hili kwa sasa lina wakazi wapatao **milioni nne (4)**. Mahitaji ya maji yanakadirwa kuwa lita **milioni 450** kwa siku ikilinganishwa na uzalishaji wa maji kwa sasa wa lita **milioni 300** kwa siku.

Mpango Maalum wa Kuboresha Huduma ya majisafi na Majitaka eneo la DAWASA ulioanza mwezi Machi, 2011 unalenga kuongeza wingi wa maji kutoka lita **milioni 300** za sasa hadi lita **milioni 756** ili kukidhi mahitaji ya maji hadi mwaka 2025 na utafuatiwa na uboreshaji awamu nyingine kuongeza uzalishaji kufikia lita za ujazo **milioni 976** Kukidhi mahitaji hadi 2013. Mpango huo unahusisha kuboresha usambazaji wa maji, kupunguza upotevu wa maji yasiyolipiwa, kuboresha utendaji wa DAWASA na DAWASCO na kuboresha uondoshaji majitaka. Mikakati ya utekelezaji wa mpango huo ni pamoja na:-

- (i) **Kuendeleza vyanzo vya maji:** Kujenga Bwawa la Kidunda katika Wilaya ya Morogoro Vijijini, Kuchimba visima virefu vya maji katika maeneo ya Kimbiji na Mpera; na Kuchimba na kufufua visima vya maji kwenye maeneo ya Jiji yasiyokuwa na mtandao wa maji;
- (ii) **Kupanua na kujenga miundombinu ya kuzalisha, kuhifadhi na kusambaza majisafi:** Kupanua mitambo ya kuzalisha maji ya Ruvu Chini na Ruvu Juu; kujenga miundombinu ya kuhifadhi na kusambaza maji kutoka visima vya Kimbiji na Mpera; na kupunguza upotevu wa maji kwa kukarabati miundombinu iliyochakaa;
- (iii) **Kupanua na kuboresha mfumo wa uondoaji wa majitaka:** Kupanua miundombinu ya majitaka ili kuhudumia eneo kubwa zaidi; na kuongeza uwezo wa kusafisha majitaka kwa kutumia teknolojia za kisasa.
- (iv) **Kuimarisha usimamizi na utoaji wa huduma:** Kuimarisha Kanda (*zones*) za kazi zilizopo na kuongeza Kanda nyingine kwenye maeneo mapya, na kuanzisha ofisi ndogo ndani ya Kanda kwa lengo la kusogeza huduma karibu zaidi na watumia maji.

Katika kutekeleza mikakati hiyo, kazi zinazoendelea ni pamoja na:-

- **Ujenzi wa Bwawa la Kidunda**

Mtaalam Mshauri wa kutathmini athari za kimazingira na kijamii (*ESIA*) kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa, la Kidunda, barabara kuelekea eneo la ujenzi wa Bwawa, mtambo wa kufua umeme na njia ya umeme amewasilisha rasimu ya mwisho mwezi Februari 2014. Rasimu ya mwisho itawasilishwa Mei 2014. Aidha, Serikali imekamilisha taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa barabara na ujenzi unatarajiwa kuanza mara baada ya kukamilika kwa tathmini ya *ESIA* na ulipaji fidia kwa watakaoathirika na mradi. Usanifu wa bwawa umekamilika na ujenzi utaanza baada ya kukamilika kwa ujenzi wa barabara.

Aidha, Mthamini wa Serikali amewasilisha rasimu ya taarifa ya mapitio ya uthamini ambao umefanyika upya baada ya kuchelewa kwa malipo ili kukidhi matakwa ya Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999. Tathimini mpya imeonyesha fidia imeongezeka kwa **asilimia 8**. Taratibu za kupata fedha **shilingi bilioni 7.9** za kulipia fidia hiyo zinaendelea.

- **Visima Virefu vya Kimbiji na Mpera**

Mradi wa visima virefu vya Kimbiji na Mpera unahusisha uchimbaji wa visima **20** vya uzalishaji na visima **8** vya kubaini mwenendo wa maji chini ya ardhi. Hadi mwezi Machi, 2014 Mkandarasi amekamilisha maandalizi ya vitendea kazi (*equipment mobilization*) na mabomba ya mradi yanayotarajiwa kuwasili kutoka China mwezi Juni, 2014 ili kazi ianze. Uchimbaji wa visima hivyo unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2014 kwa gharama ya Dola za Kimarekani **milioni 18.4**.

Kazi ya kuchimba visima virefu **vinane** vya uchunguzi wa mwenendo wa maji chini ya ardhi inaendelea ambapo kisima **kimoja** kimekamilika katika eneo la Mwasonga na uchimbaji wa visima **viwili** unaendelea katika maeneo ya Mkuranga na Kibada. Vilevile, Mtaalam Mshauri anayetathmini athari za kimazingira na kijamii (*ESIA*) amewasilisha rasimu ya tatu ya taarifa ya *ESIA* tarehe mwezi Machi 2014 na kupelekwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kuridhiwa.

Baada ya kulipa fidia kwenye eneo la **mita 60** kuzunguka kila kisima katika maeneo ya Kimbiji na Mpera kukamilika, Serikali imekamilisha uhakiki wa fidia katika maeneo ya Luzando na Kisarawe II na ulipaji wa fidia umeanza kwa eneo litakapojengwa tanki la Kisarawe II pamoja na kwa eneo la Luzando. Vilevile, uthamini katika maeneo ya ujenzi wa njia za mabomba na barabara kuelekea kwenye visima umeanza, na maombi ya kupata Wathamini yamewasilishwa kwenye Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali.

- **Upanuzi wa Mtambo wa Ruvu Juu**

Mradi huo unahusisha upanuzi wa mtambo na ujenzi wa bomba kuu la kutoa maji Ruvu Juu hadi matanki ya Kimara na kulaza mabomba ya kusambaza maji katika maeneo ya Mlandizi hadi Kimara. Mradi huo unatarajiwa kukamilika baada ya miezi **18**. Upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu utaongeza uwezo wa mtambo kutoka mita za ujazo **82,000** kwa siku mpaka mita za ujazo **196,000** kwa siku ili kukabiliana na changamoto ya ukuaji wa kasi wa miji ya Mlandizi, Kibaha na Jiji la Dar es Salaam. Mradi huo unatekelezwa kwa mkopo nafuu wa **Dola za Kimarekani milioni 99** kutoka Serikali ya India (*Indian Line of Credit*).

Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 Wakandarasi **wawili**, mmoja wa kukarabati na kupanua mtambo wa Ruvu juu na mwingine wa kulaza bomba na kujenga matanki wameanza kazi.

- **Upanuzi wa Mradi wa Maji wa Ruvu Chini**

Serikali kwa kushirikiana na *MCC* inaendelea na kazi ya upanuzi wa mradi wa maji wa Ruvu Chini. Kazi ya upanuzi wa mtambo wa Ruvu Chini imekamilika na kwa sasa Mkandarasi anaendelea

kufanya majaribio ya mitambo. Kazi ya ulazaji wa bomba kuu kutoka Mitambo ya Ruvu Chini hadi kwenye matanki ya Chuo Kikuu cha Ardhi imefikia **kilomita 35.16** sawa na **asilimia 62.87** ya umbali wa **kilomita 55.93** na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2014. Aidha, kazi ya ujenzi wa kingo za mto Ruvu katika eneo la Kidogozero imekamilika na kwa sasa Mkandarasi yuko kwenye kipindi cha uangalizi (*defects notification period*).

- **Ukarabati na Upanuzi wa Mfumo wa Kusambaza Majisafi**

Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Mfumo wa Kusambaza Majisafi kati ya jiji la Dar es Salaam na mji wa Bagamoyo unahusisha kuunganisha wateja kutoka Tegeta hadi Mpiji na Mpiji hadi Bagamoyo. Mradi huo unajumuisha ulazaji wa mabomba ya urefu wa **kilomita 732** ya kusambaza maji yatakayounganisha wateja **3,400** na kujenga **vioski 30** kati ya Bagamoyo na Tegeta. Mtaalam Mshauri atakayesanifu na kusimamia ujenzi amepatikana na anaendelea kuandaa nyaraka za zabuni za ujenzi wa mradi.

Mradi wa kuunganisha mabomba ya usambazaji maji ya urefu wa **kilomita 300** kwenye eneo la Mbezi hadi Kiluvya unaendelea kutekelezwa. Jumla ya **wateja 10,000** wataunganishwa na **vioski 30** vitajengwa. Hapo awali, mchakato wa zabuni ya usanifu, usimamizi wa ujenzi na ujenzi ulisitishwa kutokana na uhaba wa fedha. Kwa sasa Mtaalam mshauri anaandaa nyaraka za zabuni.

Vilevile, katika kugharamia miradi hiyo ya usambazaji maji katika jiji la Dar es Salaam ili iwe endelevu, Wizara imefikia makubaliano ya awali na Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*) ili iweze kusaidia katika uwekezaji huo. Kwa sasa Mtaalam Mshauri ameanza kazi ya upembuzi yakinifu na kuandaa makadirio ya gharama za mradi ili zitumike kutayarisha Mkataba wa kifedha.

- **Uchimbaji wa visima katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam**

Utekelezaji wa miradi ya uchimbaji wa visima katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam ili kupunguza kero ya maji wakati wa kusubiri utekelezaji wa Mradi Maalum wa Kuboresha Upatikanaji wa Huduma ya Majisafi na Uondoaji Majitaka katika Jiji la Dar es Salaam unaendelea.

Hadi mwezi Machi 2014, **visima 44** vimechimbwa kati ya **visima 46** vilivyopangwa. Kati ya hivyo, **visima 21** vimekamilika na visima **nane (8)** vinatumika Kimara, katika maeneo ya Mavurunza A, Kilungule A, Kilungule B, King'ongo I, King'ongo II, King'ongo III, Saranga I na Saranga II; Visima **vitano (5)** viro Keko/Chang'ombe maeneo ya Keko Magurumbasi, Keko mwanga A, Chang'ombe A, Unubini na Chang'ombe Toroli; na kwa Sandali visima **vitatu (3)** katika maeneo ya Sandali, Mpogo na Mwembe Radu. Aidha, visima vingine **viwili (2)** vilivyokamilika vinatumika Mburahati maeneo ya *Mburahati National Housing* na Shule ya Msingi Muungano; na **kisima kimoja kimoja** katika maeneo ya Mwaninga-Kigamboni, Kipunguni na FFU yaliyoko Ukonga. Visima vingine 23 vilivyo chimbwa vinaendelea kukamilishwa.

- **Mradi wa Maji ya bomba kwenda eneo la Hospitali Mpya ya Muhimbili- Mloganzila**

Serikali imekamilisha ununuzi wa mabomba na pampu, ukarabati wa tanki la zamani kwenye kituo cha kusukuma maji na ujenzi wa mnara wa tanki jipya litakalopokea maji kutoka kwenye chanzo. Kazi zote zilikamilika mwezi **Oktoba 2013**. Uchimbaji wa mtaro wenye urefu wa **mita 1,935** umekamilika ambapo mabomba yenye urefu wa **mita 1,000** yamelazwa. Kazi ya kulaza mabomba yenye urefu wa **mita 935** zilizobaki inaendelea.

- **Mradi wa Kuboresha huduma ya maji na usafi wa mazingira Pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam**

Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ubelgiji imekamilisha utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma ya maji na usafi wa mazingira kwa wananchi waishio pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam kwa gharama ya **shilingi bilioni 15.7**. Mradi huo unahudumia wananchi wapatao **170,000** kwa kutoa huduma ya maji safi kwenye maeneo ya makazi, huduma ya vyoo bora kwenye maeneo ya shule, zahanati na masoko katika Manispaa tatu za Mkoa wa Dar es Salaam (Kinondoni, Temeke na Ilala). Mradi huo ulizinduliwa rasmi na Waziri wa Maji tarehe 12 Machi 2014.

5.2.4 KUWAJENGEA UWEZO WATUMISHI NA KUIMARISHA TAASISI

Katika kuwajengea uwezo watumishi na kuimarisha taasisi za sekta ya maji, Wizara imetekeliza kazi mbalimbali katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014:

5.2.4.1 Uratibu wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji

Katika kipindi cha miezi ya Julai 2013 hadi Machi 2014, Wizara iliendelea kuratibu programu kwa kutekeleza yafuatayo:-

- (i) Uratibu wa vikao **nane** vya kawaida vya watalaam (*Technical Working Groups*) na kikao **kimoja** cha ushauri cha wataalam (**WSWG**) vimefanyika;
- (ii) Wizara kwa kushirikiana na Sekta za Afya na Elimu, na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na Washirika wa Maendeleo ilisimamia zoezi la kukagua miradi ya maji na usafi wa mazingira kwa pamoja (*Joint Supervision Mission*) mwezi Oktoba hadi Novemba 2013. Katika zoezi hilo, miradi mbalimbali ya maji na usafi wa mazingira ilikaguliwa. Zoezi hilo lilibaini maeneo yanayohitaji ufuutiliaji wa karibu na kutoa mapendekezo ili kuboresha utekelezaji wa masuala mbalimbali katika Sekta ya Maji;
- (iii) Mwezi Novemba 2013, Wizara ilifanikisha Mkutano wa siku **mbili** wa Mwaka wa Mapitio ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*Joint Water Sector Review*). Wadau mbalimbali wapatao **200** wa sekta ya maji walihudhuria Mkutano huo. Washiriki wa Mkutano huo walitoa mapendekezo kuhusu utekelezaji wa Programu; na vilevile, kuandaa na kupitisha masuala (*undertakings*) yatakayoshughulikiwa katika kipindi kijacho cha utekelezaji wa Programu;
- (iv) Katika kuimarisha upatikanaji wa takwimu, ufuutiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango na miradi kwenye sekta ya maji, mfumo wa Kielektroniki wa Takwimu na Taarifa (*Water Sector Management Information System*) umeboreshwa na mafunzo ya matumizi ya

mfumo huo yametolewa kwa Watumishi **40** kutoka Makao Makuu ya Wizara, Halmashauri za Wilaya mpya **72**, Mikoa mipyä **8**, Mamlaka za Majisafi na Majitaka **62** na Bodi za Maji za Mabonde **18**;

- (v) Wizara iliendesha mafunzo ya matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa takwimu na utambuzi wa vituo vya kuchotea maji vijiji (Water point mapping) mwezi Machi, 2014 kwa kutumia TEHAMA kwa Watumishi **50** kutoka makao makuu ya Wizara, Wahandisi wa Maji wa Halmashauri **155**, Wahandisi wa Maji kwenye Sekretarieti za Mikoa **26**, Wasajili **163** wa Vyombo vya Watumia Maji kwenye Halmashauri na Maafisa Maji wa Mabonde **watatu (3)**;
- (vi) Katika jitihada za kuongeza kasi na ufanisi wa Programu, Serikali imeanzisha Mpango Kabambe wa “Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa” (*Big Results Now Program-BRN*) ambapo Programu ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji imejumuishwa. Kupitia Mpango huo, Wizara imeanza kutekeleza kwa kuongeza wataalam wazoeufu kutoka Wizarani kwenda kuwajengea uwezo wataalam katika ngazi ya Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri;
- (vii) Kitengo cha Uratibu wa Programu katika OWM-TAMISEMI kimeimarishwa kwa kupatiwa wahandisi na wahasibu ili kiweze kufuatilia kwa ukaribu masuala ya utekelezaji wa Programu na maandalizi ya taarifa mbalimbali za Programu. Kitengo hicho kina jukumu la kuratibu upatikanaji wa taarifa na mijadala inayohusiana na Sekta ya Maji;
- (viii) Wizara imeendelea kuboresha mifumo ya mawasiliano kwa kufunga *Server mbili* katika Ofisi za Makao Makuu ya Wizara ya Maji na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa taarifa za utekelezaji wa miradi ya maji kwa kutumia mifumo ya kielektroniki ambayo ni *Management Information System (MIS)* na *Water Point Mapping (WPM)*;
- (ix) Katika mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara ilipanga kufanya ufuatiliaji na tathimini (*Monitoring and Evaluation*) ya miradi ya maji nchini mara moja kwa kila robo mwaka. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014, ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi umefanyika katika robo ya kwanza ambapo mikoa ya Kagera, Singida, Tabora, Simiyu, Kigoma, na Shinyanga iliusika. Katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka, ufuatiliaji wa miradi ulifanyika katika mikoa ya Mara, Geita, Tanga, Kilimanjaro, Manyara, Arusha na Mwanza. Aidha, katika kuhakisha miradi ya *BRN* inatekelezwa kwa ufanisi, viongozi wa Wizara wanafanya ufuatiliaji wa miradi katika mikoa yote na taarifa zinaandaliwa kila mwezi.

5.2.4.2 Habari, Elimu na Mawasiliano

Katika kutaarifu, kufafanua na kuelimisha jamii kuhusu masuala mbalimbali yanayotekelawa na Sekta ya Maji Wizara ilishiriki kikamilifu katika maonesho ya Kilimo ya Nanenane yaliyofanyika Nzuguni mjini Dodoma mwezi Agosti 2013, ambapo vipeperushi, majarida na machapisho mbalimbali yanayohusu shughuli zinazotekelawa kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji vilisambazwa kwa jamii. Pia, elimu ya Sera ya Maji kwa lugha nyepesi ilitolewa kwa wananchi kupitia majarida na santuri za maigizo ili kuifahamu mipango na mikakati ya Wizara.

Wizara iliandaa vipindi maalum kupitia vyombo vya habari kuhusiana na hali ya maji mkoani Dodoma; mradi wa maji wa kitaifa Masasi-Nachingwea; upanuzi wa mradi wa maji wa Ruvu Chini; mradi wa maji wa Kahama-Shinyanga; na kituo cha utafiti cha kuondoa madini ya *fluoride* kwenye maji cha Ngurdoto mkoani Arusha. Aidha, katika Maadhimisho ya Wiki ya Maji yaliyofanyika kitaifa mkoani Dodoma mwezi Machi, 2014, Wizara ilitoa jumla ya machapisho **5,000** na vipindi **saba (7)** vya redio na luninga.

5.2.4.3 Ujenzi na ukarabati wa majengo ya Wizara

Wizara imeendelea na mpango wake wa kujenga jengo la Wizara (*Maji House*) na hatua iliyofikiwa ni kufanya tathmini (*Evaluation*) ya kumpata mkandarasi. Aidha, ukarabati wa majengo ya Wizara yaliyopo Dar es Salaam na Dodoma unaendelea. Vilevile ujenzi wa ukuta (*fence*) kuzunguka eneo la Bohari Kuu ya Maji na Ghala (*Warehouse*) umekamilika. Makabrasha ya zabuni ya kumpata mtaalam mshauri wa ujenzi wa ofisi ya Bohari Kuu ya Maji yameandaliwa..

5.2.4.4 Chuo cha Maendeleao na Usimamizi wa Rasilimali za Maji (WDMI)

Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji kiliendelea na jukumu lake la kujenga uwezo wa kitaalam wa fani za ufundi zinazohitajika katika utoaji wa huduma za maji na usimamizi wa rasilimali za maji. Hadi kufikia mwezi Machi 2014, Chuo kiliendelea na majukumu yake kwa kutekeleza yafuatayo:-

Utoaji wa mafunzo

Chuo kilidahili wanafunzi wa mwaka wa kwanza **412** wa stashahada (*water technicians*) na wanafunzi **69** wa shahada ya kwanza ya Uhandisi wa rasilimali za maji na umwagiliaji (*Bachelor of Engineering in Water Resources and Irrigation*) na kukifanya kuwa na jumla ya wanafunzi **1,020** wakiwemo wanafunzi wa mwaka wa pili na wa tatu. Wanafunzi **144** walihitimu mafunzo yao mwezi Novemba 2013 katika fani za uhandisi wa mifumo ya ugavi wa maji safi na uondoaji takia (*water supply and sanitation engineering*) (**80**), Utafutaji wa maji ardhini na uchimbaji wa visima vya maji (*Hydrogeology and water well drilling*) (**22**), Haidrolojia na Hali ya hewa (**26**), na Teknolojia ya maabara ya uchunguzi wa ubora wa maji (*Water Quality Laboratory technology*) (**16**).

Aidha, Chuo kilitoa ushauri juu ya ubora wa maji kwa wateja **136** waliowasilisha sampuli zao. Chuo pia kilitoa ushauri wa upatikanaji maji ardhini katika maeneo ya Makambako (Iringa), Kiwalani (Ilala), Gairo (Morogoro), Kigamboni (Temeke), Sikonge (Tabora), Kibamba (Kinondoni), Korogwe (Tanga), Ilula (Iringa) na Makongo (Rufiji). Vilevile ,washiriki **135** walipewa mafunzo ya muda mfupi (*short courses*) katika fani mbalimbali zinazohusu sekta ya maji.

Katika kuweka uwiano sawa kijinsia chuoni, Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ilifadhili wanafunzi wa kike (**52**) katika kozi ya kuwawezesha kujiunga na masomo ya stashahada (*Access Course*). Hii imewezesha kuongeza udahili wa wanafunzi wa kike kutoka **67** mwaka 2012/2013 hadi **79** katika mwaka 2013/2014.

Katika kuboresha utoaji wa huduma, mikataba ya ununuzi wa vifaa chuoni ilisainiwa. Vifaa hivyo ni kwa ajili ya maabara ya *hydraulics*, maabara ya ubora wa maji, maabara ya usambazaji maji, maabara ya hali ya hewa, na maabara ya udongo. Pia, watumishi **70** walipatiwa mafunzo ya masuala ya ununuzi, na Bodi ya Zabuni ilizinduliwa. Ili kukabiliana na upungufu wa watumishi, Chuo kilajiri watumishi wapya **8**.

5.2.4.5 Maendeleo ya Rasilimali Watu

Hadi kufikia mwezi Machi 2014, Wizara imepokea watumishi wapya **22** kutoka Sekretarieti ya Ajira. Watumishi hao ni mhasibu msaidizi **mmoja**, wahaidrolojia **watatu**, Wakemia **wanne**, Mhudumu wa Afya **mmoja**, Mafundi Sanifu **13**, ambapo kati ya hao, fani ya ujenzi **sita**, fani ya haidrolojia **wawili** na fani ya haidrojiolojia **watano**.

Katika vipindi nya mwezi Februari na Aprili 2014, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kiufundi la Ujerumani (*GIZ*), ilitoa mafunzo kwa viongozi **36** wa Wizara pamoja na baadhi ya Maafisa Watendaji Wakuu wa taasisi zilizo chini yake kwa ajili ya kuimarisha uongozi na utendaji kazi. Vilevile, mwezi Januari, 2014 watumishi **42** walipatiwa mafunzo elekezi kuhusu utumishi wa umma.

5.2.4.6 UKIMWI

Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara imetua elimu kuhusu UKIMWI kwa watumishi **580** wa Wizara. Kati ya hao, watumishi **160** walipata ushauri nasaha na kukubali kupima VVU kwa hiari ili kujua afya zao. Aidha, Dawati la UKIMWI la Wizara lilishiriki katika maonesho ya Wiki ya Maji yaliyofanyika kitaifa mjini Dodoma kuanzia tarehe 16 - 22/3/2014 kwa kutoa elimu, ushauri nasaha pamoja na upimaji wa hiari kwa jamii.

5.2.5 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KATIKA UTEKELEZAJI NA HATUA ZINAZOCHUKULIWA

Katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara ilikabiliana na changamoto mbalimbali. Changamoto zilizojitokeza na hatua zinazochukuliwa kuzikabili ni kama ifuatavyo:-

5.2.5.1 Upatikanaji wa fedha kwa wakati

Kutokana na ufinyu wa mapato ya ndani, fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo hutokana na vyanzo kama vile mikopo nafuu kwenye benki za kibishara, mikopo yenye marsharti nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo, pamoja na misaada kutoka kwa wahisani. Upatikanaji wa fedha kwenye vyanzo kama hivyo huambatana na changamoto mbalimbali kama vile hali ya uchumi wa nchi wahisani na dunia kwa ujumla, mabadiliko ya uongozi na sera za nje katika nchi hizo, nakadhalika. Kutokana na kuchelewa kupatikana kwa fedha, utekelezaji wa miradi ikiwemo miradi ya maji umekuwa ukiathirika.

Katika kuhakikisha fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo zinapatikana, Wizara inafanya mawasiliano ya karibu na wadau hususan Wizara ya Fedha na Washirika wa Maendeleo kwa kuchukua hatua zafuatazo:

- (a) Kufanya mawasiliano ya karibu na Ofisi ya Rais- Tume ya Mipango pamoja na Wizara ya Fedha kwa upande wa fedha za ndani;
- (b) Kuandaa na kuwasilisha kwa wakati Mpango Kazi (*Action Plan*) wa kutekeleza bajeti pamoja na mahitaji ya fedha kwa kila kipindi cha Robo mwaka. Mpango kazi huo ndiyo unaotumika na Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango katika utoaji wa fedha kwa upande wa Serikali.
- (c) Kuandaa na kuwasilisha kwa wakati taarifa za utekelezaji wa miradi Wizara ya Fedha, Tume ya Mipango na kwa Washirika wa Maendeleo;
- (d) Kufanya majadiliano na Washirika wa Maendeleo juu ya utoaji na matumizi ya fedha za WSDP. Majadiliano hayo yamewezesha kukubaliana kuanza utoaji wa fedha kwa kipindi cha miezi sita sita badala ya utaratibu wa kutoa fedha kidogo kidogo kulipa madeni ya wakandarasi. Hatua ya kuanza kutoa fedha za miezi sita kuanzia robo ya pili imesaidia hadi sasa *WSDP Basket Donors* kutoa fedha zote walizoahidi katika mwaka wa fedha 2013/14.

5.2.5.2 Upungufu wa Wataalam katika Sekta ya Maji

Sekta ya Maji inakabiliwa na upungufu wa wataalam **7,211** unaotokana na Serikali kutoajiri kwa muda mrefu, kuongezeka kwa idadi ya Mikoa, Wilaya, Halmashauri pamoja na kustaafuli kwa baadhi ya watumishi. Idadi ya wataalam wanaohitajika kwenye sekta ya maji katika ngazi ya Wizara, Sekretarieti za Mikoa, na Halmashauri ni **8,749** wakati Wataalam waliopo ni **1,538**. Mchanganuo wa mahitaji ya wataalam wa kada mbalimbali katika Sekta ya Maji umeainishwa katika **Kiambatisho Na. 3.**

Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara iliomba kibali cha ajira Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma mwezi Desemba, 2013. Mnamo mwezi Machi, 2014 Ofisi hiyo imetoea kibali cha nafasi **475** kwa ajili ya kuajiri Wahandisi wa maji **125** na Mafundi Sanifu **350**. Wizara kwa kushirikiana na Sekretarieti ya ajira inaendelea na taratibu za kuajiri wataalam hao. Aidha, Wizara inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kuajiri watalaam wengi zaidi wanaohitajika katika Sekta ya Maji.

Katika harakati za kukabiliana na upungufu wa wataalam hasa wahandisi wa kusimamia miradi, Wizara imewasilisha maombi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kuajiri kwa mikataba wataalam wa maji wenye uzoefu kwa ajili ya kuwajengea uwezo wataalam wapya watakaoajiriwa. Vilevile, baadhi ya wahandisi wazoefu kutoka Wizarani wamehamishiwa kwenye Sekretarieti za Mikoa ili kuongeza uwezo wa usimamizi na ufuutiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maji kwenye Halmashauri mbalimbali nchini.

5.2.5.3 Upatikanaji wa takwimu sahihi na taarifa za utekelezaji kwa wakati

Kutokana na Programu kushirikisha taasisi mbalimbali ambazo Wizara ya Maji haina mamlaka ya kiutawala moja kwa moja, limekuwepo tatizo la kupata takwimu sahihi za matumizi ya fedha ikilinganishwa na kazi zilizotekelizwa kwenye miradi ya maji katika Halmashauri mbalimbali nchini. Katika kubabiliana na changamoto hii, jududi zinaendelea kuimarisha uratibu wa

TAMISEMI na kuanzisha Ofisi 9 za Kanda ili zisimamie kikamilifu utekelezaji wa miradi ya maji ngazi ya Halmashauri.

5.2.5.4 Kuongezeka kwa idadi ya watu kusikoendana na kasi ya uwekezaji

Utoaji wa huduma ya maji unakabiliwa na changamoto ya kuongezeka kwa idadi ya watu kusikoendana na uwekezaji. Hali hiyo ni dhahiri katika maeneo ya mijini ambapo kiwango cha ongezeko watu kwa mwaka ni **asilimia 4.5** tofauti na maeneo ya vijijini ambapo wastani wa ongezeko la watu kwa mwaka kitaifa ni **asilimia 2.3**. Mathalan, Jiji la Dar es Salaam linakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji kutokana na ongezeko kubwa la watu la **asilimia 6** kwa mwaka tofauti na wastani kitaifa wa **asilimia 4.5**. Ongezeko la watu linaenda sambamba na kukua kwa shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na viwanda na kupanuka kwa ujenzi wa makazi. Kutokana na ukuaji huo wa kasi, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

- (a) Kushirikisha wananchi hususan katika maeneo ya vijijini katika hatua zote za miradi ikiwa ni pamoja na kubuni, kujenga, kusimamia, kuendesha na kuchangia gharama za uendeshaji; na
- (b) Kukarabati na kujenga miradi ya kipaumbele ambayo inatoa huduma kwa wananchi wengi zaidi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mradi wa maji wa **Vijiji 10** kwa kila Halmashauri; Mpango wa dharura wa kuboresha huduma za maji Jijini Dar es Salaam; miradi kwenye maeneo kame kama vile miradi ya maji ya Mwanga-Same-Korogwe na Masasi-Nachingwea; na kujenga mabwawa kama vile Farkwa kwa ajili ya mji wa Dodoma.

5.2.5.5 Hujuma kwenye miundombinu ya maji

Biasara ya vyuma chakavu imechangia kwa kiasi kikubwa uharibufu kwenye miundombinu ya maji hali inayoathiri upatikanaji wa huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka kwa jamii. Katika kukabiliana na changamoto hii, Serikali imekuwa ikitoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa ulinzi shirikishi katika kulinda miundombinu ya maji kuitia maonesho na shehere mbalimbali za kitaifa kuitia Wiki ya Maji na maigizo kwenye luninga na redio pamoja na usambazaji wa vipeperushi. Aidha, Mamlaka za Majisafi mijini zimeendelea kushirikiana na uongozi wa Mikoa, Jeshi la Polisi na Wananchi ili kubaini wanaojihusisha na hujuma hizo ikiwa ni pamoja na kutoa zawadi ya fedha kwa watoa taarifa. Vilevile, Wizara imetua Waraka kwa Mamlaka zote nchini kutokununua vifaa vya maji viliviyotumika kama vile mita za maji, mabomba na vipuli vya mitambo.

5.2.5.6 Mabadiliko ya tabianchi

Mabadiliko ya tabianchi yanasaababisha kutokutabirika kwa msimu na mtawanyiko wa mvua, ukame wa muda mrefu, mafuriko ya mara kwa mara hali inayoathiri ujenzi wa miundombinu ya maji na upatikanaji wa rasilimali za maji. Hatua zinazochukuliwa kukabiliana na changamoto hiyo ni pamoja na:

- (a) Kujenga mabwawa madogo na makubwa kwa ajili ya hifadhi ya maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali;

- (b) Kuimarisha ukusanyaji wa takwimu zinazohusu rasilimali za maji na mabadiliko ya tabianchi;
- (c) Kutoa mafunzo kwa wataalam na kuelimisha umma ili kuongeza weledi kuhusu mabadiliko ya tabianchi;
- (d) Kutumia utaalam asilia (*Indigenous knowledge*) katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;
- (e) Kushirikisha wadau mbalimbali katika kutunza vyanzo vyta maji kwa kuvitambua na kuviwekea mipaka;
- (f) Kupanda miti kwenye maeneo ya hifadhi za maji;
- (g) Kuzuia shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo oevu, maeneo ya milimani na katika chemichemi za maji;
- (h) Kudhibiti matumizi holela ya maji kwa kutoa kibali cha kutumia maji;
- (i) Kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vyta maji na uharibifu wa mazingira kwa kutumia Sheria za Maji na Mazingira na pia kwa kutumia sheria ndogo za Halmashauri;
- (j) Kuendeleza matumizi ya teknolojia sahihi za umwagiliaji zinazotumia maji kwa ufanisi; na
- (k) Kushirikiana na taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali zinazofanya utafiti kuhusu mabadiliko ya tabianchi kwa lengo la kufanya utafiti wa pamoja na kutathmini matokeo ya tafiti mbalimbali ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

6.0. MALENGO KATIKA KIPINDI CHA MUDA WA KATI NA MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

6.1 Muhtasari wa Malengo Makuu ya Kipindi cha Muda wa Kati (MTEF)

Malengo kwenye uendelezaji na utunzaji wa rasilimali za maji, pamoja na ubora wa maji:-

- (a) Kuongeza usalama na uwezo wa kuhifadhi maji kwa kujenga na kukarabati mabwawa;
- (b) Kuunda jumuiya mpya **102** za watumiaji maji na Kamati mpya **65** za kuhifadhi vyanzo vya Maji na kuzijengea uwezo jumuiya **81** zilizopo sasa;
- (c) Kubainisha maeneo **93** ya vyanzo vya maji kwa ajili ya kuyatangaza kuwa maeneo tengefu na kuibua vyanzo vypya **105** katika mabonde yote **9** nchini;
- (d) Kuongeza vituo vya uchunguzi wa mwenendo wa rasilimali za maji kutoka **410** vya sasa hadi **600**;
- (e) Kuziimarisha Bodi za Mabonde yote tisa na kuziwezesha kujitegemea;
- (f) Kukamilisha uandaaji wa Mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa Rasilimali za maji (*Integrated Water Resources Management & Development Plans*) katika Mabonde yote ya maji nchini; na
- (g) Kuziimarisha maabara zote **16** za maji ili ziweze kujiendesha.

Malengo kwenye kuongeza upatikanaji wa huduma za maji

- (a) Kuwapatia wananchi waishio vijijini maji safi na salam karibu na makazi yao, lengo likiwa ni kufikia **74%** ya wananchi waishio vijijini mwaka 2017, kutoka **49%** za sasa;
- (b) Kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji katika miji mikuu ya mikoa **19** kutoka in **86%** sasa hadi **95%**;
- (c) Kuongeza upatikanaji wa maji katika miji mikuu ya mikoa mipyä kutoka **53%** za sasa hadi **75%**;
- (d) Kuongeza upatikanaji wa maji katika Miradi ya Kitaifa, Miji Midogo na Miji mikuu ya Wilaya kutoka **53%** za sasa hadi **57%**; na
- (e) Kuongeza upatikanaji wa maji katika eneo linalohudumiwa na DAWASA kutoka **68%** za sasa hadi **75%**.

Malengo ya kuzijengea uwezo taasisi na watumishi (*Institutional Strengthening and Capacity Building*)

- (a) Kukamilisha maandalizi ya mpango endelevu wa mafunzo kwa watumishi na kuanza kuutekeleza mpango huo;

- (b) Kuboresha mazingira ya kufanya kazi kwa kuendelea na ukarabati wa majengo kuongeza samani, na vitendea kazi, pamoja na kuanza ujenzi wa jengo jipya la Wizara;
- (c) Kupunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa watumishi wa Wizara na Taasisi zake;
- (d) Kuimarisha uratibu wa utekelezaji wa *WSDP*; na
- (e) Kuimarisha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ili kuwezesha utekelezaji wa *WSDP*.

6.2 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2014/2015

Katika mwaka wa fedha 2014/15, kupitia Fungu 49, kiasi cha **Shilingi 140,142,684** kimepangwa kukusanya kutoka kwenye vyanzo vidogo vidogo vya mapato kama vile ada za maabara ya maji na uuzaji wa nyaraka za zabuni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 6.1**. Fedha hizo zitapelekwa kwenye mfuko mkuu wa Serikali. Aidha, jumla ya **Shilingi 2,731,000,000** zinatarajiwaa kukusanya nje ya Fungu 49 kupitia Bodi za maji za mabonde kama inavyoonekana katika **Jedwali Na 6.2**.

6.2.1 Makadirio ya Katika Makao Makuu ya Wizara

Katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Wizara imepanga kukusanya kiasi cha **shilingi 140,142,684** kama maduhuli. Mchanganuo wa makusanyo ya maduhuli hayo ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 6.1**.

Jedwali Na 6.1: Makadirio ya Makusanyo ya Fedha kwa Mwaka 2014/2015

Kifungu	Viwango Vilivyokubaliwa
1001: Idara ya Utawala	20,142,684
2003: Idara ya Huduma za Ubora wa Maji	120,000,000
JUMLA	140,142,684

6.2.2.Makadirio ya Maduhuli ya Bodi za Mabonde ya Maji

Katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 jumla ya **shilingi 2,731,000,000** zimekadiriwa kukusanya na Bodi za Mabonde ya Maji kwa majibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji **Na. 11** ya mwaka 2009, inayoziruhusu kukusanya na kutumia mapato yatokanayo na ada za kutumia maji na ada nyingine. Mchanganuo wa makusanyo ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 6.2**

Jedwali 6.2: Makusanyo ya Maduhuli ya Bodi za Mabonde ya Maji

Na	Bonde	Makadirio
1.	Pangani	370,000,000
2.	Wami/Ruvu	320,000,000
3.	Mto Rufiji	580,000,000
4.	Ruvuma na Pwani ya Kusini	150,000,000
5.	Ziwa Nyasa	430,000,000
6.	Bonde la Kati	200,000,000

Na	Bonde	Makadirio
7.	Ziwa Rukwa	246,000,000
8.	Ziwa Tanganyika	85,000,000
9.	Ziwa Victoria	350,000,000
Jumla		2,731,000,000

6.3 Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara ya Maji 2014/2015

Katika mwaka wa fedha 2014/2015, jumla ya **Shilingi 30,899,443,000** zimekasimiwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 15,514,444,000** sawa na **asilimia 50.2** ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo (*OC*), na **Shilingi 15,384,999,000** sawa na **asilimia 49.8** ni kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi (*PE*).

Jedwali Na. 6.3: Muhtasari wa Bajeti ya Matumizi ya kawaida katika Vifungu vya Wizara kwa mwaka 2014/2015

Kifungu	Bajeti ya OC	Bajeti ya Mishahara	Jumla ya Matumizi ya Kawaida
1001 – Idara ya Utawala na Rasilimali Watu	1,948,705,000	1,997,468,400	3,946,173,400
1002 - Kitengo cha Fedha na Uhasibu	599,199,000	801,589,200	1,400,788,200
1003 – Idara ya Sera na Mipango	2,125,917,000 ³	393,249,600	2,519,166,600
1004 - Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano	310,686,000	58,422,000	369,108,000
1005 - Kitengo cha Sheria	323,560,000	140,958,900	464,518,900
1006 - Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi	567,019,000	319,486,800	886,505,800
1007 - Kitengo cha Mfumo wa Habari	320,285,000	142,560,500	462,845,500
1008 - Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani	495,243,000	146,129,400	641,372,400
2001 – Idara ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji	952,889,000	5,339,756,800	6,292,645,800
2002 - Bohari Kuu ya Maji	223,012,000	167,064,000	390,076,000
2003 – Idara ya Huduma za Ubora wa Maji	363,458,000	1,663,136,100	2,026,594,100
3001 – Idara ya Huduma za Majisafi na Uondoaji wa Majitaka Mijini	4,840,408,000	1,440,150,000	6,280,558,000
4001 – Idara ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini	2,047,305,000	765,262,500	2,812,565,500
4002 – Kitengo cha Uratibu wa Programu	396,758,000	0	396,758,000
5001 – Taasisi ya Usimamizi na Maendeleo ya Maji (Wakala)	0	227,493,800	227,493,800
6001 – Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa	0	759,429,000	759,429,000
Jumla ndogo	15,514,444,000	14,362,157,000	29,876,601,000
MISHAHARA YA WAKALA			
Kifungu 5001 – Taasisi ya Usimamizi na Maendeleo ya Maji (Wakala)	0	1,022,842,000	1,022,842,000
Jumla Kuu (OC +Mishahara)	15,514,444,000	15,384,999,000	30,899,443,000

³ Kati ya fedha hizo, kiasi cha **shilingi 1,052,595,000** ni kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa DDCA na WMDI

6.3.1 Malengo ya Kipindi cha Muda wa Kati, Kazi zitakazoteklezwa na Gharama Kifungu kwa Kifungu kwa Mwaka 2014/2015

Malengo ya kipindi cha muda wa kati, kazi zitakazoteklezwa na gharama kifungu kwa kifungu kwa mwaka 2014/2015 yameainishwa kama ifuatavyo:

6.3.1.1 Kifungu 1001 – Utawala

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazoteklezwa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
1	Kuboresha huduma na kupunguza maambukizi ya UKIMWI	<p><i>Kupunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa watumishi wa Wizara na Taasisi zake kufikia kiwango cha chini kabisa kitaifa hadi kufikia Juni 2017</i></p> <p><i>Kutoa mafunzo kwa watumishi kuhusu masuala ya UKIMWI.</i></p> <p><i>Kutoa posho maalum ya chakula kwa watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI ili kupata lishe bora.</i></p> <p><i>Kugharamia vikao vya kamati ya UKIMWI.</i></p>	<p>0</p> <p>26,095,000</p> <p>26,095,000</p>
2	Kuhakikisha Mkakati wa Taifa wa Kupambana na rushwa unatekelezwa.	<p><i>Watumishi wa Wizara wanapatiwa mafunzo ya namna ya kupambana na kuzuia rushwa hadi kufikia Juni 2017.</i></p> <p><i>Kujenga uelewa kwa watumishi wa Wizara juu ya adhari za rushwa.</i></p> <p><i>Kusambaza sheria, kanuni, miongozo na vipeperushi.</i></p> <p><i>Kuwezesha mikutano ya kamati ya maadili.</i></p> <p><i>Kuendesha mafunzo ya maadili ya Utumishi wa Umma kwa watumishi wapya.</i></p>	<p>1,235,000</p> <p>2,605,000</p> <p>1,675,000</p> <p>1,760,000</p>
3	Kuboresha mazingira ya kazi ili kuongeza ufanisi na ubora wa huduma zinazotolewa	<p><i>Kuboresha mazingira ya kazi ili kuongeza ufanisi na ubora wa huduma zinazotolewa</i></p> <p><i>Kugharamia shughuli za uendeshaji na stahili za watumishi.</i></p> <p><i>Kugharamia uendeshaji wa jenereta na magari.</i></p> <p><i>Kuwawezesha watumishi kushiriki michezo ya SHIMIWI</i></p>	<p>1,302,495,000</p> <p>33,125,000</p> <p>29,240,000</p>

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazotekelawa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
		Kuajiri watumishi wapya na kuwapandisha madaraja watumishi waliopo kwa kuzingatia sifa zao.	2,000,000
		Kugharamia safari za kikazi za Viongozi na Watumishi ndani na nje ya nchi.	240,900,000
		Kukiwezesha chama cha wafanyakazi kushiriki katika Maadhimisho ya Sikuu ya Wafanyakazi- Mei Mosi.	166,025,000
		Kuwezesha shughuli za Bunge	125,350,000
		<i>Kuendeleza na kutekeleza programu ya kujenga uwezo wa watumishi hadi kufikia 2017</i>	
		Kuwezesha utekelezaji wa mipango ya kuwajengea uwezo watumishi	16,200,000
Jumla –Matumizi Mengineyo (OC)			1,948,705,000
Jumla – Mishahara (PE)			1,997,468,400
Jumla – Kifungu 1001			3,946,173,400

6.3.1.2 Kifungu 1002 – Uhasibu na Fedha

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazotekelawa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
1.	Kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.	<i>Kuimarisha usimamizi na udhibit wa matumizi ya fedha za umma kila mwaka</i>	
		Kuandaa na kutoa ripoti za mapato na matumizi ya fedha kila robo mwaka kwa kuzingatia kanuni na sheria za fedha	32,180,000
		Kuandaa malipo ya taasisi zinazotekeliza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji na kazi za Wizara ya Maji.	28,800,000
		Kuandaa taarifa za Kamati ya Bunge ya Fedha za Umma.	43,600,000

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazoteklezwa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)	
		Kusimamia na kufuatilia taarifa za kifedha kwa watekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.	59,450,000	
2.	Kuboresha mazingira ya kazi ili kuongeza ufanisi na ubora wa huduma zinazotolewa	<i>Kuhakikisha mazingira ya kazi na maslahi ya wafanyakazi yanaboreshwani.</i>		
		Kugharamia vikao vya kamati ya ukaguzi.	4,100,000	
		Kugharamia shughuli za uendeshajji na stahili za watumishi	322,970,000	
		<i>Kujwajengea uwezo watumishi wa Idara ya Uhasibu kila mwaka</i>		
		Kushiriki katika vikao vya kimataifa kila mwaka.	33,150,000	
		<i>Kuboresha usimamizi na uandaaji wa hesabu za fedha hadi kufikia 2017</i>		
		Kutoa mafunzo juu ya masuala mbalimbali ya kiuhasibu.	14,499,000	
		Kuandaa ripoti za kifedha kila robo mwaka, nusu mwaka, na za mwaka.	15,200,000	
		<i>Kuandaa appropriation accounts</i>	19,750,000	
		Kuratibu hoja za ukaguzi kutoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.	25,500,000	
Jumla –Matumizi Mengineyo (OC)			599,199,000	
Jumla – Mishahara (PE)			801,589,200	
Jumla – Kifungu 1002			1,400,788,200	

6.3.1.3 Kifungu 1003 – Sera na Mipango

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazoteklezwa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
1	Kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.	<i>Kuhakikisha kuwa Taasisi za Sekta ya Maji zinawezeshwa ili zitoe huduma stahiki na kuanza kujitegemea ifikapo 2017.</i>	
		Kuziwezesha DDCA na WMDI	1,052,595,000

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazoteklezwa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
2.	Kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.	<p><i>Kubaini maeneo ya kufanya mageuzi (reforms) katika Sekta ya Maji na kuyatekeleza ifikapo mwaka 2017.</i></p> <p>Kufuatilia na kutathimini utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.</p> <p>Kuandaa taarifa za utekelezaji za Wizara kwa vipindi vyatofu robo mwaka, nusu mwaka na mwaka.</p> <p>Kuandaa bajeti ya mwaka na mpango kazi.</p> <p>Kuratibu na kuandaa nyaraka za Baraza la Mawaziri na kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya masuala ya muungano.</p> <p>Kuratibu na kuandaa ripoti za utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na Kamati za Kudumu za Bunge.</p> <p>Kushiriki katika mikutano ya kikanda (<i>EAC, SADC, ZAMCOM, na NBI</i>), na Kuratibu masuala ya <i>PPP</i>.</p> <p>Kuandaa Mpango Mkakati wa Wizara (<i>Strategic Plan</i>)</p> <p>Kuandaa hotuba ya bajeti ya Wizara.</p>	179,000,000 30,250,000 152,750,000 50,000,000 30,000,000 20,350,000 126,500,000 167,500,000
	Kuboresha mazingira ya kazi ili kuongeza ufanisi na ubora wa huduma zinazotolewa	<i>Watumishi wa Idara ya Sera na Mipango wanapatiwa ujuzi unaohitajika kufanikisha majukumu yao kiufasaha hadi kufikia Juni 2017</i>	
3.		<p>Kugharamia mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi ndani ya nchi.</p> <p>Kugharamia mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi nje ya nchi.</p> <p>Kugharamia mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi.</p>	44,442,500 40,000,000 30,000,000

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazotekelzwa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
		<i>Kuweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa watumishi wa Idara ya Sera na Mipango.</i>	
Jumla – Matumizi Mengineyo (OC)			2,125,917,000
Jumla – Mishahara (PE)			393,249,600
Jumla – Kifungu 1003			2,519,166,600

6.3.1.4 Kifungu 1004 – Habari, Elimu na Mawasiliano

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazotekelzwa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
1.	Kuboresha mazingira ya kazi ili kuongeza ufanisi na ubora wa huduma zinazotolewa	<i>Watumishi kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano wanapatiwa mbinu bora za mawasiliano hadi kufikia Juni 2017</i>	
<i>Kuwezesha watumishi kupata mafunzo ya muda mfupi nchini</i>			28,500,000
<i>Kuwezesha watumishi kupata mafunzo ya muda mrefu nje ya nchi</i>			27,000,000
<i>Kuboresha mazingira ya kazi na ustawi wa watumishi wa Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano kila mwaka</i>			
<i>Kugharamia shughuli za uendeshaji na stahili za watumishi</i>			81,956,000
<i>Kuboresha maktaba na ununuvi wa vitabu</i>			50,280,000
<i>Kufanya ufuutiliaji na kukusanya taarifa mbalimbali Wizarani na miradi ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji nchini</i>			122,950,000
Jumla – Matumizi Mengineyo (OC)			310,686,000
Jumla – Mishahara (PE)			58,422,000
Jumla – Kifungu 1004			369,108,000

6.3.1.5 Kifungu 1005 – Sheria

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazoteklezwa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
1.	Kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.	<p><i>Kutoa huduma za kisheria kwa taasisi za Sekta ya maji.</i></p> <p>Kupitia, kusimamia na kutekeleza mikataba ya kimataifa kuhusu rasilimali za maji shirikishi</p> <p><i>Kutoa ushauri wa kisheria kwa taasisi zinazoteklezwa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.</i></p> <p>Kufanya mapitio ya sheria na kutafsiri kanuni za utekelezaji wa sheria za maji.</p> <p>Kuendesha mashitaka na kufuatilia kesi mahakamani.</p> <p><i>Kutoa elimu juu ya sheria ya maji kwa taasisi zinazoteklezwa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji</i></p> <p><i>Kutoa mafunzo juu ya sheria za maji kwa taasisi zinazoteklezwa WSDP</i></p> <p>Kuwezesha utekelezaji wa mipango ya kuwajengea uwezo watumishi (<i>CD plans</i>).</p>	17,200,000 27,900,000 69,500,000 19,250,000 72,610,000 33,400,000
2.	Kuboresha mazingira ya kazi ili kuongeza ufanisi na ubora wa huduma zinazotolewa	<p><i>Kuboresha mazingira ya kazi na ustawi wa watumishi wa Kitengo cha Sheria kila mwaka</i></p> <p>Kugharamia shughuli za uendeshaji na stahili za watumishi</p>	83,700,000
Jumla – Matumizi Mengineyo (OC)			323,560,000
Jumla – Mishahara (PE)			140,958,900
Jumla – Kifungu 1005			464,518,900

6.3.1.6 Kifungu 1006 – Usimamizi wa Ununuzi

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazoteklezwa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
1.	Kuhakikisha makundi yote ya jamii vijiji na mijini yanapata huduma ya majisafi na salama pamoja na usafi wa mazingira	<p><i>Taratibu za manunuvi na usimamizi wa mikataba zinaboresha hadi kufikia Juni 2017</i></p> <p>Kusimamia na kuratibu ununuvi na vifaa na kutoa ushauri wa kitaalam.</p> <p>Kufanikisha usimamizi na uhakiki wa vifaa vya Wizara na Taasisi</p> <p>Kuthaminisha na kuziwekeea alama samani na vitendea kazi na kuboresha kitabu cha kumbukumbu</p>	255,000,000 24,136,000 14,196,000
2.	Kuboresha mazingira ya kazi ili kuongeza ufanisi na ubora wa huduma zinazotolewa	<p><i>Kuweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa watumishi wa Kitengo cha Usimamizi wa Manunuvi .</i></p> <p>Kutoa ushauri wa kitaalam juu ya manunuvi na usimamizi wa mikataba Wizarani na katika Taasisi zinazoteklezwa WSDP</p> <p>Kugharamia shughuli za uendeshaji na stahili za watumishi</p> <p>Kugharamia mafunzo juu ya manunuvi na usimamizi wa mikataba kwa watumishi</p> <p>Kukamilisha maboresho pamoja na kufunga vifaa vipyta katika chumba cha kutunza kumbukumbu</p>	31,010,000 157,680,000 80,350,000 4,647,000
Jumla –Matumizi Mengineyo (OC)			567,019,000
Jumla – Mishahara (PE)			319,486,800
Jumla – Kifungu 1006			886,505,800

6.3.1.7 Kifungu 1007 – Mfumo wa Taarifa za Kimenejimenti

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazoteklezwa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
1.	Kuboresha mazingira ya kazi ili	<i>Kuhakikisha TEKNOHAMA ya Wizara kwa ajili</i>	

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazotekelezwa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
	kuongeza ufanisi na ubora wa huduma zinazotolewa	<i>ya kutunza taarifa pamoja na kutoa huduma inaboresha hadi kufikia Juni 2017</i>	
		Kuboresha mfumo wa mawasiliano wa Wizara.	30,000,000
		Kuboresha benki ya takwimu ya sekta ya maji.	80,350,000
		Kutekeleza mipango ya kuwajengea uwezo watumishi.	53,200,000
		<i>Kuweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa watumishi wa Kitengo cha Mfumo wa Taarifa za Kimenejimenti.</i>	
		Kugharamia shughuli za uendeshaji na stahili za watumishi	80,735,000
		Kuboresha na kutunza vifaa vya TEKNOHAMA	76,000,000
Jumla –Matumizi Mengineyo (OC)			320,285,000
Jumla – Mishahara (PE)			142,560,500
Jumla – Kifungu 1007			462,845,500

6.3.1.8 Kifungu 1008 – Ukaguzi wa Ndani

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazotekelezwa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
1.	Kuhakikisha makundi yote ya jamii vijiji na mijini yanapata huduma ya majisafi na salama pamoja na usafi wa mazingira	<i>Kukagua kumbukumbu za fedha za Wizara kwa kuzingatia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2001.</i>	
		Kuhakikisha menejimenti ya Wizara inatekeleza mfumo wa ndani wa udhibiti wa fedha.	49,799,000
		Kufanya ukaguzi kwa Taasisi zinazotekeliza WSDP	61,400,000
		Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya Risk Management Register ambayo imeanza kutumika na Wizara ya Maji	11,200,000

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazotekelzwa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
		Kufanya ukaguzi wa ndani wa kitaalam kwa Taasisi zinazotekelza <i>WSDP</i>	42,260,000
		Kufanya ukaguzi wa thamani ya fedha kwa Taasisi zinazotekelza <i>WSDP</i>	67,200,000
		Kufanya ukaguzi wa ndani wa manunuzi na usimamizi wa mikataba kwa Taasisi zinazotekelza <i>WSDP</i>	38,110,000
2.	Kuboresha mazingira ya kazi ili kuongeza ufanisi na ubora wa huduma zinazotolewa	<p><i>Watumishi wote Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani wanapatiwa mbinu muhimu za ukaguzi hadi kufikia Juni 2017</i></p> <p>Kugharamia mafunzo ya wakaguzi wa ndani</p> <p>Kuwezesha watumishi wa kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kuhudhuria mikutano na makongamano ya kimataifa ya wakaguzi wa ndani</p> <p><i>Kuweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa watumishi wa Idara ya Ukaguzi wa Ndani.</i></p> <p>Kugharamia shughuli za uendeshaji na stahili za watumishi</p> <p>Kuiwezesha Kamati ya Ukaguzi ya Wizara</p>	73,800,000 39,800,000 78,200,000 33,474,000
Jumla –Matumizi Mengineyo (OC)			495,243,000
Jumla – Mishahara (PE)			146,129,400
Jumla – Kifungu 1008			641,372,400

6.3.1.9 Kifungu 2001 – Usimamizi Rasilimali za Maji

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazotekelzwa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
1.	Kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.	<p><i>Kutoa msaada wa kiutawala kwa bodi za mabonde ya Maji yote 9.</i></p> <p>Kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa</p>	10,500,000

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazoteklezwa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
		WSDP katika ofisi za maji za mabonde .	
		Kuwezesha Bodi ya Maji ya Taifa kutekeleza majukumu yake	8,600,000
		Kuratibu utunzaji na udhibiti wa rasilimali za maji.	48,400,000
		Kugharamia maandalizi ya takwimu kwa ajili ya Benki ya Taifa ya Takwimu ya Rasilimali za Maji na kusambaza taarifa kwa wadau.	26,500,000
		Kusajili, kukagua na kufuatilia uchunguzi wa rasilimali za maji chini ya ardhi na kampuni za uchimbaji visima.	6,900,000
		Kuratibu na kusimamia maandalizi ya Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali Maji katika mabonde	20,250,000
		Kuratibu programu za kitaifa na za kikanda kuhusu usimamizi wa maji shiriki.	99,590,000
		Kukagua mifumo ya utiririshaji majitaka katika viwanda na migodi.	10,650,000
		Kuwezesha uandaaji wa taarifa mbalimbali za rasilimali za maji	14,650,000
2.	Kuboresha mazingira ya kazi ili kuongeza ufanisi na ubora wa huduma zinazotolewa	<i>Kuweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa watumishi wa Idara ya Rasilimali za Maji kitaifa na katika mabonde hadi kufikia Juni 2017</i>	
		Kutekeleza mpango wa kuwajengea uwezo watumishi	110,000,000
		Kugharamia shughuli za uendeshaji na stahili za watumishi	596,849,000
Jumla –Matumizi Mengineyo (OC)			952,889,000
Jumla – Mishahara (PE)			5,339,756,800

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazoteklezwa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
Jumla – Kifungu 2001			6,292,645,800

6.3.1.10 Kifungu 2002 – Bohari Kuu ya Maji

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazoteklezwa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
1.	Kuhakikisha makundi yote ya jamii vijijini na mijini yanapata huduma ya majisafi na salama pamoja na usafi wa mazingira	<i>Kuhakikisha vifaa na nyenzo za kutekeleza miradi ya maji nchini vinapatikana kulingana na mahitaji na kwa muda unaotakiwa.</i>	
		Kuboresha uhifadhi na usambazaji wa vifaa, nyenzo na zana za kitaalam kwenye maeneo ya miradi ya maji nchini.	19,320,000
2.	Kuboresha mazingira ya kazi ili kuongeza ufanisi na ubora wa huduma zinazotolewa	<i>Kuweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa watumishi wa Bohari Kuu ya Maji.</i>	
		Kugharamia shughuli za uendeshaji na stahili za watumishi	156,292,000
		Kuwezesha utekelezaji wa mipango ya kuwajengea uwezo watumishi.	47,400,000
Jumla –Matumizi Mengineyo (OC)			223,012,000
Jumla – Mishahara (PE)			167,064,000
Jumla – Kifungu 2002			390,076,000

6.3.1.11 Kifungu 2003 –Huduma za Ubora wa Maji

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazoteklezwa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
1.	Kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.	<i>Sampuli 24,000 na 3,000 za maji na majitaka zinakusanya na kufanyiwa uchunguzi hadi kufikia Juni 2017</i>	
		Kupima vielelezo vyta awali, kukusanya na kufanya uchunguzi wa sampuli 8,000 za maji.	24,700,000

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazoteklezwa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
		<p>Kukusanya na kufanya uchunguzi wa sampuli 1,000 za majitaka na kutoa ushauri juu ya kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji</p> <p><i>Mkakati na technolojia ya kuondoa madini ya fluoride kwenye maji unatekelezwa katika mikoa 7 hadi kufikia Juni 2017</i></p>	15,350,000
		<p>Kufanya utafiti wa madini ya <i>fluoride</i> katika vyanzo vya maji juu na chini ya ardhi katika wilaya za Rungwe, Tarime and Rufiji</p>	3,850,000
		<p>Kusambaza matokeo ya utafiti juu ya matumizi ya mkaa wa mifupa ya ng'ombe kuondoa madini ya <i>fluoride</i> kwenye maji katika mikoa ya Arusha, Manyara, Mwanza, Singida, Mara, Mbeya na Kilimanjaro.</p>	3,100,000
		<p><i>Kutekeleza program ya kuhakiki ubora wa maji katika maabara 16 hadi kufikia Juni 2017</i></p>	
		<p>Kushiriki katika mazoezi ya kujipima uwezo kwa maabara zote 16 za maji na maabara zingine ndani na nje ya nchi.</p>	13,350,000
		<p>Kuwezesha maabara za maji katika kusimamia vizuri kemikali na kemikali taka</p>	21,500,000
2.	Kuboresha mazingira ya kazi ili kuongeza ufanisi na ubora wa huduma zinazotolewa	<p><i>Kuweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa watumishi 104 wa Idara ya Huduma ya Maabara za Maji</i></p> <p>Kugharamia shughuli za uendeshaji na stahili za watumishi</p> <p>Kugharamia shughuli za uendeshaji katika maabara 15 za maji nchini</p>	224,608,000 45,000,000

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazotekelezwa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
		Kugharamia shughuli za uendeshaji katika kituo cha utafiti Ngurdoto	12,000,000
Jumla –Matumizi Mengineyo (OC)			363,458,000
Jumla – Mishahara (PE)			1,663,136,100
Jumla – Kifungu 2003			2,026,594,100

6.3.1.12 Kifungu 3001 – Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazotekelezwa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)	
1.	Kuhakikisha makundi yote ya jamii vijiji na mijini yanapata huduma ya majisafi na salama pamoja na usafi wa mazingira	<i>Kuziwezesha Mamlaka za Maji mijini ili ziweze kujitegemea.</i>		
		Kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa WSDP ngazi ya mamlaka.	127,650,000	
		Kuandaa na kusambaza miongozo inayohusu usambazaji wa huduma ya maji na uondoaji wa majitaka ngazi ya mamlaka za maji.	67,320,000	
		Kuwezesha uendeshaji wa miradi ya kitaifa na mamlaka za maji za daraja B na C kwa kugharamia sehemu ya bili za umeme.	3,944,000,000	
		Kuratibu na kufuatilia kamati ya mikopo	68,800,000	
2.	Kuboresha mazingira ya kazi ili kuongeza ufanisi na ubora wa huduma zinazotolewa	<i>Kuweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa watumishi wa Idara ya Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini.</i>		
		Kutekeleza mipango ya kuwajengea uwezo watumishi.	93,855,000	
		Kugharamia shughuli za uendeshaji na stahili za watumishi	538,783,000	
Jumla –Matumizi Mengineyo (OC)			4,840,408,000	
Jumla – Mishahara (PE)			1,440,150,000	
Jumla – Kifungu 3001			6,280,558,000	

6.3.1.13 Kifungu 4001 – Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazoteklezwa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
1.	Kuhakikisha makundi yote ya jamii vijijini na mijini yanapata huduma ya majisafi na salama pamoja na usafi wa mazingira	<p><i>Kuongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama vijijini kutoka asilimia 49 kwa mwaka 2013 hadi asilimia 74 kwa mwaka 2017</i></p> <p>Kusimamia na kutathmini utekelezaji wa <i>WSDP</i> ngazi ya Serikali za mitaa.</p> <p>Kutoa miongozo kwa Serikali za Mitaa na Sekretarieti za mikoa kuhusu uendelezaji na usimamizi wa miradi ya maji.</p> <p>Kutoa ushauri wa kitaalam kwa Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji.</p> <p>Kusambaza taarifa muhimu ili kufanikisha utekelezaji wa <i>WSDP</i>.</p> <p><i>Kuwajengea uwezo watumishi wa Idara ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, Sekretariet za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kutekeleza miradi ili kufanikisha malengo ya kutoa huduma za Maji vijijini</i></p> <p>Kugharamia mafunzo kwa watumishi wa Idara ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini</p> <p>Kutoa mafunzo ya usanifu na ujenzi wa miradi, usimamizi wa mikataba <i>MIS/EPICOR, WPM</i> na usafi wa mazingira</p>	229,150,000 40,750,000 65,800,000 45,500,000 551,000,000 572,400,000
2.	Kuboresha mazingira ya kazi ili kuongeza ufanisi na ubora wa huduma zinazotolewa	<p><i>Kuweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa watumishi wa Idara ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini.</i></p> <p>Kugharamia shughuli za uendeshaji na stahili za watumishi</p>	542,705,000

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazotekelawa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
Jumla –Matumizi Mengineyo (OC)			2,047,305,000
Jumla – Mishahara (PE)			765,262,500
Jumla – Kifungu 4001			2,812,567,500

6.3.1.14 Kifungu 4002: Uratibu wa Programu

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazotekelawa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
1.	Kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.	<i>Kuratibu na kufuatilia kazi zinazofanyika katika kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji hadi kufikia Juni 2017</i>	
		Kugharamia uandaaji wa taarifa za utekelezaji na taarifa ya mwaka ya hali halisi ya Sekta ya Maji (<i>Water Sector status Report</i>)	35,550,000
		Kuratibu Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji	28,200,000
		Kuratibu kazi zinazoimarisha usafi wa mazingira na afya jamii	25,825,000
		Kugharamia mikutano ya ushirikiano kati ya Sekta zinazotekelawa <i>WSDP</i>	28,150,000
		Kugharamia vikao vya <i>TWG, WSWG, JWSR</i> na <i>WSSC</i>	59,400,000
		Kuratibu <i>JSM</i> pamoja na ukaguzi wa kitaalam	22,350,000
		Kushiriki katika maadhimisho ya matukio ya kitaifa kama vile Nanenane	16,140,000
2.	Kuboresha mazingira ya kazi ili kuongeza ufanisi na ubora wa huduma zinazotolewa	<i>Watumiishi wote wa Kitengo cha Uratibu wa Programu wanapatiwa mbinu za kuratibu na kupata matokeo mazuri ya program</i>	
		Kugharamia mafunzo ya muda mfupi kwa watumiishi	84,024,000
		Kugharamia mafunzo ya muda mrefu kwa watumiishi	25,000,000

Na.	Madhumuni	Malengo na Kazi zitakazotekelzwa	Kiasi Kilichotengwa (Sh.)
		Kugharamia shughuli za uendeshaji na stahili za watumishi	72,119,000
Jumla – Matumizi Mengineyo (OC)			396,758,000
Jumla – Mishahara (PE)			0
Jumla – Kifungu 4002			396,758,000

6.4 MAKADIRIO YA BAJETI YA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2014/2015

Katika mwaka wa fedha 2014/2015, fedha zinazohitajika kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni **Shilingi 490,007,032,000**. Kati ya fedha hizo jumla ya **Shilingi 312,066,164,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 177,940,868,000** ni fedha za nje kupitia Fungu 49 –Wizara ya Maji. Fedha hizo zimetengwa kugharamia miradi ya kipaumbele kitaifa ikiwemo miradi ya kutekeleza Mpango wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa (BRN) kwa Sekta ya Maji katika Sekta ndogo ya maji Vijijini. Aidha, kipaumbele kimewekwa zaidi kwenye miradi ya kimkakati ikiwemo uboreshaji wa huduma ya maji Jijini Dar es Salaam, mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda kwenye Miji na Vijiji vilivyopo karibu na bomba kuu la Kahama Shinyanga. Vilevile, huduma ya maji kwenye miji midogo yenye shida kubwa ya maji imezingatiwa katika bajeti hii. Sambamba na miradi ya usambazaji maji, kipaumbele kimetolewa kwenye miradi na kazi zinazohusu uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji; pamoja na uboreshaji wa maabara za maji nchini.

6.4.1 Mgawanyo wa Bajeti ya Maendeleo Kiprogramu

Mgawanyo wa Fedha za Bajeti zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika kila Programu Ndogo ya WSDP kwa kipindi cha mwaka 2014/2015 ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 6.5**

Jedwali Na.6.5: Mgawanyo wa Bajeti ya Maendeleo Katika Programu

Na.	Programu	Makadirio ya Bajeti (Shilingi)				
		Fedha za Ndani	Fedha za Ndani (%)	Fedha za Nje	Fedha za Nje (%)	Jumla
1	Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji	26,500,000,000	9	31,217,534,000	18	57,717,534,000
2	Programu ya	166,816,164,000	53	30,293,416,000	17	197,109,580,000

Na.	Programu	Makadirio ya Bajeti (Shilingi)				
		Fedha za Ndani	Fedha za Ndani (%)	Fedha za Nje	Fedha za Nje (%)	Jumla
	huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini	0		⁴ 73,870,000,000		
3	Programu ya Maji safi na Majitaka Mijini	104,750,000,000	34	102,913,868,000	58	207,663,868,000
4	Programu ya Kuimarisha Taasisi za Sekta ya Maji na Kujenga Uwezo	14,000,000,000	4	13,516,050,000	7	27,516,050,000
JUMLA		312,066,164,000		177,940,868,000		490,007,032,000

